# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Tano



Taasisi ya Elimu Tanzania

Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tano



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 42

Jina la Chapisho: Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 816 - 7

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Mwezi Oktoba Mwaka 20 18 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Darasa la Tano katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

Dkt. Edicome Cornel Shirima
Kaimu Kamishna wa Elimu.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

Kiswahil STD 5 New.indd 1 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018

Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978-9976-61-816-7

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170 /+255 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



Kiswahil STD 5 New.indd 2 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

Ukurasa

**Utangulizi**.....v

**Shukurani**.....vi

**Sura ya Kwanza**
Vitendawili.....1

**Sura ya Pili**
Ngonjera.....9

**Sura ya Tatu**
Nahau.....21

**Sura ya Nne**
Kauli zetu.....29

**Sura ya Tano**
Insha.....36

**Sura ya Sita**
Kutambua nafsi.....44

**Sura ya Saba**
Wanyama wafugwao.....53

**Sura ya Nane**
Wanyama wa porini.....60

**Sura ya Tisa**
Maua.....68

**Sura ya Kumi**
Shughuli za kila siku.....76

**Sura ya Kumi na Moja**
Hali ya hewa.....83

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 3 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi na Mbili**
Familia yetu....................93

**Sura ya Kumi na Tatu**
Barua rasmi....................101

**Sura ya Kumi na Nne**
Igizo....................106

**Sura ya Kumi na Tano**
Shairi....................115

**Sura ya Kumi na Sita**
Kuipenda nchi....................122

**Sura ya Kumi na Saba**
Utenzi....................131

**Sura ya Kumi na Nane**
Kupata taarifa muhimu....................137

**Sura ya Kumi na Tisa**
Sifa za wanyama....................148

**Sura ya Ishirini**
Miti yetu....................161

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 4 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha tatu katika mfululizo wa vitabu vya Kiswahili kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Darasa la Tano.

Kitabu hiki kitakuza uwezo wako wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika Kiswahili. Pia, kitakuwezesha kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Vilevile, kitakujengea uwezo wa kupanga mawazo yako kwa mpangilio na mtiririko unaotakiwa.

Kitabu kina hadithi, habari, mashairi, ngonjera, utenzi, igizo na majigambo. Vyote hivyo vitakuwezesha kujifunza kwa ufasaha. Pia, kina maswali ya kupima ufahamu wako kutokana na ulichokisikiliza, ulichokiona au ulichokisoma. Vilevile, kina mazoezi mbalimbali yatakayokuwezesha kujenga ujuzi wako wa somo la Kiswahili.

Soma kwa makini kitabu hiki ili kuweza kujenga ujuzi wako wa kumudu somo la Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 5 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

**Waandishi:** Rose S. Chipindula, Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Dkt. Adventina A. Buberwa, Dkt. Mgogo Yangson, Agnes S. Maguga, Faraja J. Mwendamseke, Winifrida J. Mutagwaba, Ester K. Koroti, Marko M. Julius na Oscar A. Ndalibamale.

**Wahariri:** Mussa R. Kaoneka (BAKITA), Luinasia E. Kombe (Mwenyekiti wa jopo) na Jopo la wahariri.

**Msanifu:** Anton K. Asukile

**Wachoraji:** Alama Arts and Media Production Limited

**Mratibu:** Rose S. Chipindula

Pia, TET inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba

**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 6 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Vitendawili

*Katika sura hii, utajifunza kutega na kutegua vitendawili. Pia, utaweza kuvihusisha vitendawili hivyo na vitu vilivyomo katika mazingira yanayokuzunguka.*

**Fikiri**

1. Unaelewa nini kuhusu vitendawili?
2. Umewahi kutega na kutegua vitendawili?
3. Je, kuna uhusiano kati ya kitendawili na jibu lake?

**Ufahamu**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Mtego wa vitendawili

Nzige, Panya na Kiwavi walikuwa marafiki walioshirikiana kwa mambo mabaya. Mara nyingi viumbe hawa walivamia mashamba ya binadamu na kufanya uharibifu wa mazao. Wali**leta kero** kubwa.

Binadamu alifanya mbinu nyingi ili kuwaangamiza viumbe hao lakini mbinu zake hazikú**fua dafu**. Siku moja Mzee Ngedere alikwenda kwa binadamu kuomba kazi ya kuwaangamiza Nzige, Panya na Kiwavi.

Binadamu alicheka sana kwa kumdharau Mzee Ngedere. Mzee Ngedere akasema, “Usinicheke, ninaweza kuwakamata na hata kuwaangamiza viumbe wale waharibifu kama utaniamini.” Binadamu akamjibu, “Mimi nimehangaika **miaka nenda miaka rudi** sijaweza kuwakamata, wewe utawezaje na uzee wako?”

“Mbona una**kata tamaa,** hujui kama **uzee ni dawa**? Mimi ninawajua viumbe hao; hupenda sana mafumbo. Nitawakamata kirahisi sana kwa mtego wa vitendawili.” Mzee Ngedere alieleza.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 1 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

"Utahitaji malipo gani?" Binadamu aliuliza. Mzee Ngedere akamjibu kuwa atajilipa kwa kuchukua mazao anayoyataka shambani kwa binadamu.

Binadamu alimruhusu Mzee Ngedere. Mzee Ngedere akaandaa tangazo kuwa kutakuwa na shindano la kutegua vitendawili. Aliahidi zawadi ya shamba na **ghala** la chakula kizuri kwa atakayetegua kitendawili chake kwa usahihi.

Nzige, Panya na Kiwavi walilipata tangazo hilo wakiwa wame**jibanza** mafichoni. Nzige akawauliza wenzake, "Rafiki zangu, hivi mnaujua utamu wa vitendawili?" Kiwavi akajibu, "Mimi naujua. Vitendawili ni vitamu kuliko hata chakula. Twendeni nikawaoneshe uhodari wangu wa kutegua vitendawili."

Panya naye hakuwa nyuma, akasema, "Hilo shamba na ghala lazima nivipate mimi. Nitafaidi utamu wa vitendawili na nitajipatia ghala la vyakula vizuri."

"Hebu **tusiandikie mate na wino ungalipo**, twendeni tukashindane." Kiwavi aliwahimiza wenzake. Wote waka**chapa mguu** kuelekea kwenye jukwaa la kufanyia shindano. Wanyama na wadudu wengine walipowaona panya na wenzake wakiingia ukumbini kwa **mbwembwe,** waliwashangilia kwa nguvu. Akina Panya wakajipanga nyuma na kuwa wa mwisho mwisho ili vitendawili vigumu zaidi viishe.



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 2 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kipepeo, Nyoka, Nyuki, Ndege na Mjusi ndio waliotangulia. Wote wakashindwa kutegua vitendawili vya Mzee Ngedere. Hatimaye ikawadia zamu ya Kiwavi. Alijinyonganyonga kwa **madaha** akapanda jukwaani na kusubiri kitendawili.

"Kitendawili?" Mzee Ngedere alisema. Kiwavi akajibu, "Tega."

"**Nikikutana na adui yangu nanyong'onyea**. Nipatie jibu na maana yake." Mzee Ngedere alitega. Kiwavi ali**chemsha bongo** akajibu haraka bila kupoteza muda. "Jibu lake **ugonjwa**. Maana yake ni kuwa ugonjwa umefananishwa na adui; ugonjwa ni adui mkubwa wa viumbe. Binadamu akikutana na ugonjwa, anakuwa mnyonge. Hata sisi viumbe wengine vivyo hivyo." Mzee Ngedere akamwambia, "Umepata!"

Panya alisogea akarukaruka kwa **mikogo** jukwaani. Mzee Ngedere akamtegea kitendawili chake, "**Adui tumemzingira lakini hatumuwezi**." Panya akajibu, "Jibu lake ni **moto**. Maana yake ni kuwa joto la moto litawapata na kuwaweza hata mkiwa wengi kiasi gani. Moto umefananishwa na adui ambaye watu wamemzunguka kana kwamba wanamshambulia." Mzee Ngedere akamwambia, "Umepata."

Baada ya Panya kupata kitendawili, Nzige akawa wa mwisho kutegua kitendawili chake. Mzee Ngedere akatega akisema, "**Ukumbuu wa babu mrefu**." Nzige aliyainuainua mabawa yake kwa **mbwembwe** na kutoa sauti ya nti! Nti! Nti! Kisha akajibu, "**Njia**. Maana yake ni kwamba njia ni ndefu kama ukumbuu. Kitendawili hiki kinafananisha urefu wa njia na mshipi."

Mzee Ngedere aliwapongeza marafiki hao watatu kwa kutegua vitendawili na kuvipatia maana zake kwa usahihi. Akawaomba waende kwenye chumba cha mapumziko ili wasubiri hatua ya pili. Waliingia kwenye chumba kilichoandaliwa chakula kizuri wakaanza kula. **Siku za mwizi ni arobaini,** na **ujanja mwingi mbele kiza**. Walipo**gutuka** wakajikuta wamekwishafungiwa humo, huku nje binadamu akiwatazama kwa **dhihaka**. Wakadhani ni **kiinimacho**. Kumbe Mzee Ngedere alikuwa ame**kula njama** kuwakamata kwa **hila** na hilo lilikuwa gereza la waharibifu wa mazao.

**Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli**. Binadamu alimshukuru Mzee Ngedere kwa msaada wake. Mzee Ngedere akarejea mlimani ingawa wakati mwingine huenda kwenye mashamba ya binadamu na kula mazao. Hufanya hivyo kwa ajili ya kuchukua malipo yake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Nzige, Panya na Kiwavi walivamia mashamba ya binadamu ili kufanya nini?
2. Binadamu alijaribu kuwaangamiza Panya na wenzake kwa muda gani bila mafanikio?
3. Kwa nini binadamu alimcheka Mzee Ngedere aliposema anaweza kuwakamata akina panya?
4. Taja zawadi mbili ambazo Mzee Ngedere aliahidi kumpa mshindi wa kutegua vitendawili.
5. Kwa nini akina Panya walijipanga nyuma ya washiriki wengine?
6. Nani aliyewaambia wenzake wasiandikie mate na wino ungalipo?
7. Ngedere alitumia mbinu gani kuwakamata Nzige, Panya na Kiwavi?
8. Binadamu alimlipa nini Mzee Ngedere kwa kazi ya kuwakamata akina Panya?
9. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Eleza maana ya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. ghala
2. jibanza
3. gutuka
4. hila
5. mbwembwe
6. dhihaka
7. mikogo
8. kiinimacho
9. madaha

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo kama zilivyotumika kwenye habari uliyosoma.**

**Mfano:** Kufa kishujaa - *ni kupambana kwa nguvu zote mpaka mwisho hata kama utashindwa*

1. fua dafu
2. chapa mguu
3. kata tamaa
4. chemsha bongo
5. kula njama

## Zoezi la 4 Misemo

**Fafanua maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumika kwenye habari uliyoisoma.**

1. miaka nenda miaka rudi
2. uzee ni dawa
3. leta kero

## Zoezi la 5 Vitendawili

**A. Tegua vitendawili vifuatavyo:**

**Mfano:** Akitokea watu wote humuona - *jua*

(i) Ajenga ingawa hana mikono.
(ii) Wakikua mama yao huwatupa mbali kwa kishindo.
(iii) Kondoo wetu ana nyama nje na ngozi ndani.
(iv) Teketeke huzaa gumugumu na gumugumu huzaa teketeke.
(v) Akitembea huringa hata akiwa hatarini.
(vi) Nina wanangu watatu akitoka mmoja wawili hawafanyi kazi.
(vii) Kipara cha babu kinafuka moshi.
(viii) Wali wa mama mtamu.
(ix) Hana adabu wala staha kwa watu.
(x) Fuu fuu funua, fuu fuu funika.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Tega vitendawili kutokana na picha zifuatazo:**

(i)



(ii)



(iii)



(iv)



(v)



(vi)





Kiswahil STD 5 New.indd 6 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

**Mfano**: Pole pole ………………

*Pole pole ndio mwendo.*

1. Mtaka yote kwa pupa …………
2. ………………, sharti ainame.
3. …………….. yasiyo na ncha.
4. Akufaaye kwa dhiki ………………
5. Hakuna masika ………………
6. Siku za mwizi ……………….
7. ………………, mbele kiza.

## Zoezi la 7 Mazoezi ya lugha

**A. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Mzee Ngedere ana busara.

*Mzee Ngedere hana busara.*

(i) Panya, Nzige na Kiwavi walishirikiana kwa mambo mema.

(ii) Binadamu ataweza kumkamata Panya na wenzake.

(iii) Viumbe hawa hupenda mafumbo.

(iv) Ngedere alikula njama kuwakamata wezi.

(v) Mjusi atashinda shindano la vitendawili.

(vi) Binadamu amemshukuru Mzee Ngedere.

(vii) Wanyama wote ni hodari wa kutegua vitendawili.

(viii) Nzige na binadamu ni marafiki.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika KWELI au SI KWELI.**

(i) Nzige, Panya, Kiwavi na Ngedere walikuwa marafiki wakubwa. ________

(ii) Binadamu alimlipa Mzee Ngedere ghala la chakula kinono. ________

(iii) Nyoka hakuweza kutegua kitendawili alichotegewa. ________

(iv) Panya alisema atafaidi vitendawili na kuchukua ghala la chakula. ________

(v) Binadamu aliwakamata Panya, Kiwavi na Nzige kwa mtego wa vitendawili. ________

(vi) Kiwavi aliingia ukumbini kwa mbwembwe. ________

(vii) Mzee Ngedere hula mazao kwenye shamba la binadamu ili kujilipa ujira. ________

(viii) Binadamu alikuwa amekata tamaa ya kuwakamata Kiwavi, Nzige na Panya. ________

## Zoezi la 8 Utungaji

**Andika insha yenye maneno kati ya hamsini na sabini (50 - 70) kwa kutumia vitendawili vifuatavyo:**

1. Kondoo wetu ana nyama nje na ngozi ndani. *firigisi*
2. Mbwa mwitu wamemzunguka kumlinda. *ulimi*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Ngonjera

*Katika sura hii, utasoma ngonjera inayohusu kipindupindu. Utajifunza kutamba ngonjera kwa usahihi. Pia, utaweza kutaja wahusika katika ngonjera na kutunga ngonjera. Vilevile, utaeleza umuhimu wa ngonjera.*

**Fikiri**

1. Je, umeshawahi kutamba ngonjera?
2. Ngonjera inafanana na nini?

**Ufahamu**

*Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Kipindupindu

**Hekima:** *Hodi hodi naingia,*
*Ujumbe nakuletea,*
*Habari kukupatia,*
*Yasije yakakukuta.*

**Bahati:** *Ujumbe gani waleta,*
*Au waleta matata,*
*Au 'mekuja ku**teta**,*
*Maneno kutia chumvi?*

**Hekima:** *Kuna **janga** latutesa,*
*Kutokana na makosa,*
*Kabwela na maofisa,*
*Janga linatumaliza.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Bahati:** *Nimeshituka moyoni,*
*Umetaja janga geni,*
*Hilo nalo janga gani,*
*Tusojua darasani?*

**Hekima:** *Kipindupindu si siri,*
*Jinale tulikariri,*
*Uchafu chanzo tukiri,*
*Choo, chakula na maji.*

*Kujisaidia ovyo,*
*Kutapisha vyoo ovyo,*
*Kulakula ovyoovyo,*
*Na kunywa maji machafu.*

**Bahati:** *Sijapata kuelewa,*
*Nisile nilichopewa,*
*Chakula cha mgahawa,*
*Kwani tatizo li wapi?*

**Hekima:** *Tukila **uchochoro**ni,*
*Usafi u mashakani,*
*Si salama **abadani**,*
*Vyakula twala **viporo**.*

*Dalili zake yakini,*
*Kutapika bila **soni**,*
*Kuhara mara sitini,*
*Na ku**dhoofika** mwili.*

*Na kuumwa miguuni,*
*Macho kuingia ndani,*
*Kukosa nguvu mwilini,*
*Kama atakaye kufa.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Bahati:**
*Jamani sasa na**kiri**,*
*Tumo katika hatari,*
*Janga hilo huathiri,*
*Uhai kuutishia.*

*Ndugu tuelezeeni,*
***Madhila** tuondoeni,*
*Tunusurike jamani,*
*Baa lilotuandama.*

**Hekima:**
*Usafi ni kinga yetu,*
*Tusafishe vyoo vyetu,*
*Tuchemshe maji yetu,*
*Chakula tule cha moto.*

*Safisha matunda yako,*
*Unawe mikono yako,*
*Sabuni ndiyo kiboko,*
*Wadudu kutokomeza.*

*Tukomeshe mambukizi,*
*Tudumishe nguvu kazi,*
*Tuyafanye mapinduzi,*
*Taifa lineemeke.*

**Hekima na Bahati:**
*Twapenda kuwausia,*
*Watu mpate sikia,*
*Usafi kuzingatia,*
*Kudumisha afya zetu.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Taja wahusika katika ngonjera hii.
2. Kipindupindu husababishwa na nini?
3. Dalili za ugonjwa wa kipindupindu ni zipi?
4. Nini kifanyike ili kuzuia kipindupindu?
5. Katika ngonjera hii, nani alikuwa haelewi kuhusu kipindupindu?
6. Kwa nini msimuliaji anawaambia watu wasafishe matunda na kunawa mikono kwa sabuni?
7. Bahati alikiri kwamba kipindupindu kitafanya nini?
8. Maneno "Taifa lineemeke" katika ubeti wa pili kutoka mwisho yana maana gani?
9. Msimuliaji wa ngonjera aliwashauri watu wafanye nini ili kutokomeza kipindupindu?
10. Umejifunza nini kutokana na ngonjera uliyoisoma?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. kipindupindu
2. viporo
3. janga
4. dhoofika
5. madhila
6. soni
7. kiri
8. teta
9. uchochoro
10. abadani

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 12 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo:**

1. ...... kwamba..........

   **Mfano:** *Bahati alisema kwamba kipindupindu ni hatari.*

2. ..................lakini...................

   **Mfano:** *Alicheza vizuri lakini hakufunga.*

3. ..................kutokana na……………

   **Mfano:** *Aliugua kipindupindu kutokana na kula vyakula vichafu.*

4. ..........kwa niaba.....................

   **Mfano:** *Aliomba msamaha kwa niaba ya wanafunzi wenzake.*

## Zoezi la 4 Nahau

**Tunga sentensi kwa kutumia nahau zifuatazo:**

**Mfano:** pata jiko – *Mzee Kiboyo alipata jiko akiwa na umri mkubwa.*

1. tia chumvi
2. piga uvivu
3. lala tanga
4. zunguka mbuyu
5. kufa kiofisa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Vitendawili

**Tumia picha zifuatazo kutegua vitendawili ulivyopewa.**













FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Ajihami bila silaha. __________
2. Adui tumemzingira lakini hatumuwezi. __________
3. Mbwa mwitu wamemzunguka kumlinda. __________
4. Baba tajiri wa mashuka, watoto wanalala bila ya kujifunika. __________
5. Askari wangu ni mpole lakini adui wanamhara. __________
6. Pita huko na mimi nipite huku tukutane kwa mjomba. __________

## Zoezi la 6 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Mkaidi ………………
2. ……………… ni mateke.
3. Mkuki kwa nguruwe, ……………
4. ………………., angali mbichi.
5. Kuuliza .......................

## Zoezi la 7 Mazoezi ya lugha

**A. Andika maneno yafuatayo kwa kirefu.**

**Mfano:** jinale - *jina lake*
babake - *baba yake*

(i) tusojua __________
(ii) lilotuandama __________
(iii) dalilize __________
(iv) mwishowe __________
(v) mamake __________
(vi) mambukizi __________
(vii) mekuja __________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 15 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku.**

kana, lia, nawiri, patana, joto,
raha, uongo, nuru, zama

(i) dhoofu ________

(ii) baridi ________

(iii) madhila ________

(iv) kosana ________

(v) kiri ________

(vi) cheka ________

(vii) ukweli ________

(viii) elea ________

(ix) giza ________

**C. Andika KWELI au SI KWELI katika sentensi zifuatazo:**

(i) Kipindupindu ni ugonjwa wa vipele vya ngozi. ________

(ii) Kipindupindu ni ugonjwa unaotibika. __________

(iii) Kipindupindu ni ugonjwa unaoambukiza. __________

(iv) Watoto wadogo tu ndio wanaougua ugonjwa wa kipindupindu. ________

(v) Watu wanaoishi katika mazingira safi hupata ugonjwa wa kipindupindu. ___________

(vi) Kula hovyo barabarani ni tabia mbaya. ________

(vii) Kula vyakula vya moto kunapunguza maambukizi ya kipindupindu. __________

(viii) Kuhara na kutapika ni baadhi ya dalili za kipindupindu. ________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 16 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopita.**

**Mfano:** Bustani za mboga zinatunzwa vizuri.
*Bustani za mboga zilitunzwa vizuri.*

(i) Mtoto mwenye adabu anafanya kazi kwa bidii.

(ii) Mama anakwenda shambani kwake.

(iii) Vijana wanajitahidi kulima.

(iv) Kipindupindu kinaua watu wengi.

(v) Sisi tunafanya kazi kwa kushirikiana.

(vi) Mtu mwenye busara anakuja kwenye mkutano.

(vii) Zaina atauza maandazi.

(viii) Basi litaingia alfajiri.

(ix) Walimu wa Darasa la Tano wanarudi shuleni.

(x) Watoto hao wanajitahidi kusoma kwa bidii.

**E. Chagua jibu lililo sahihi kwa kuandika herufi katika kisanduku.**

(i) Ngonjera uliyoisoma ina beti ngapi?

(a) kumi na nne
(b) nane
(c) kumi na sita
(d) nne

(ii) Idadi ya mizani katika mstari wa kila ubeti wa ngonjera uliyoisoma ni:

(a) kumi na sita
(b) nane
(c) nne
(d) kumi na nne

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Vina katika ubeti wa kwanza na wa pili ni:

(a) **a** na **ta**

(b) **ia** na **eta**

(c) **ho** na **u**

(d) **mbe** na **di**

(iv) Kila ubeti wa ngonjera uliyoisoma una mistari mingapi?

(a) kumi na nne

(b) nane

(c) kumi na sita

(d) minne

(v) Alama gani ya uandishi imetumika mara nyingi zaidi kwenye mistari ya mwisho wa beti za ngonjera uliyoisoma?

(a) alama ya mkato

(b) alama ya kuuliza

(c) alama ya nukta

(d) alama ya mshangao

(vi) Hekima alitamba beti ngapi?

(a) 8

(b) 10

(c) 11

(d) 5

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 18 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F.** **Katika jedwali lifuatalo, kamilisha maneno ya sehemu B ili yaendane na ya sehemu A.**

**Mfano:** kitabu _kubwa

*kitabu kikubwa*

| Sehemu A | | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | ng'ombe | __nene |
| (ii) | macho | __kali |
| (iii) | watu | __zuri |
| (iv) | mataifa | __kubwa |
| (v) | walimu | __cheshi |
| (vi) | mwaka | __ingine |
| (vii) | kiatu | __kubwa |
| (viii) | mchanga | __ingi |
| (ix) | kitabu | __eusi |
| (x) | mtoto | __pole |

**G.** **Andika maneno yenye maana sawa na maneno yaliyotolewa.**

**Mfano:** motokaa – *gari*

(i) kauzu ________

(ii) fedha ________

(iii) bakora ________

(iv) treni ________

(v) msichana ________

(vi) mwana ________

(vii) msalani ________

(viii) abadani ________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8 Utungaji

**A. Kamilisha habari hii kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku.**

| |
|---|
| akawaona, wanaoga, ilijaa, akawaambia, wadudu, waliondoka, wakavaa, aliondoka, kichocho, machafu, kutambua |

Watoto walikuwa (1)__________na kuogelea kwenye dimbwi karibu na nyumbani kwao. Walizama na kuibuka kwenye yale maji (2) ______. Miili yao (3) ________matope. Haikuwa rahisi (4) ________sura zao. Bibi Loshi alipokuwa anapita pale (5) __________ wale watoto, "Loo! Nyie watoto mtaleta balaa! Maji hayo yana (6) ________wengi. Tokeni haraka." Wale watoto walitoka (7)________nguo zao. Bibi Loshi (8) ______, "Humo ndani mna wadudu wanaosababisha (9) _________, homa ya matumbo na magonjwa mengine. Ondokeni wajukuu zangu." Wale watoto (10) ______. Pia bibi Loshi (11) ________akaendelea na safari yake.

**B. Tunga ngonjera yenye beti mbili kuhusu nzi.**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 20 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Nahau

*Katika sura hii, utajifunza kutumia nahau katika habari fupi na kueleza maana zake pamoja na umuhimu wake. Pia, utaweza kueleza taswira inayoakisiwa na nahau.*

### Fikiri

1. Mama huyu anafanya nini?
2. Kwa nini anafanya hivyo?




FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 21 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ufahamu**

***Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.***

## Jongoo na nyoka

Hapo zamani za kale, Jongoo na Nyoka walikuwa marafiki. Jongoo katika maumbile yake alijaliwa kuwa na macho lakini hakuwa na miguu. Tofauti na Jongoo, Nyoka alijaliwa kuwa na miguu lakini hakuwa na macho. Marafiki hawa walifanya kazi **bega kwa bega**. Jongoo na Nyoka walikuwa na rafiki yao aliyeitwa Mwewe. Siku moja Jongoo na Nyoka walienda kumtembelea Mwewe. Nyoka alitembea polepole japokuwa alikuwa na miguu mingi. Alifanya hivyo kwa kuogopa kuji**kwaa.** Jongoo alikuwa anatembea harakaharaka kwa sababu alikuwa anaona kila kitu.



Walipofika nyumbani kwa Mwewe, walikuta ndege wengi wamekusanyika wakiwa wanalia. Nyoka alisikia sauti lakini hakuona kitu chochote. Nyoka alitamani sana kuwa na macho ili aone kinachoendelea. Nyoka aliuliza, "Kuna nini hapa?" Kunguru alimjibu, "Mtoto wa Mwewe ame**aga dunia**." Nyoka aliuliza tena, "Mbona sikuelewi?" Kunguru alijibu, "Mtoto wa Mwewe amefariki." Nyoka na Jongoo walishitushwa na taarifa hiyo.

Waliingia ndani; wakamkuta Mwewe ame**shika tama**. Walim**fariji** Mwewe kwa kumkumbatia huku machozi yakiwalengalenga. Walikaa hapo wakiendelea kumfariji hadi siku ya ku**anua matanga**. Wakarudi nyumbani kuendelea na maisha yao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baada ya miaka kadhaa kupita, Jongoo aliugua. Alitumia kila aina ya dawa lakini hakupata **ahueni**. Nyoka alimuonea huruma. Akamwambia, "Rafiki yangu, babu yangu ame**kula chumvi nyingi**. Yeye ana uwezo wa kuku**tibu** haraka." Jongoo alishangaa kusikia hivyo. Aliuliza, "Mbona humu ndani tuna chumvi nyingi na kila siku tunaitumia?" Nyoka akamjibu, "Sina maana hiyo rafiki yangu. Nina maana kuwa babu ameishi miaka mingi. Hivyo naamini atakuponya."

Baada ya Jongoo kusikia hivyo, ali**kata shauri** na kumwambia nyoka aende kumleta babu yake. Nyoka alikubali ila alimwambia atachelewa kufika kwa sababu hana macho. Hivyo, alimwambia, "Kama hutajali tubadilishane. Wewe unipe macho, na mimi nikupe miguu. Nikipata macho nitamleta babu haraka." Jongoo alimwambia, "Basi chukua macho yangu na wewe unipe miguu yako." Nyoka aliondoka haraka kwa furaha maana aliona kila kitu kinachoendelea duniani. Alifika kwa babu yake akamwambia kuwa rafiki yake anaumwa sana hadi ame**kufa moyo**. Hivyo, aliomba aende haraka nyumbani kwake akamtibu. Wakiwa njiani, nyoka alimwambia babu yake am**shawishi** jongoo amwachie macho na yeye abaki na miguu. Babu alikubali.

Walipofika walimkuta Jongoo ame**lala fofofo**. Walimwamsha, kisha babu alimpima. Akasema, "Unaumwa ugonjwa hatari. Nitakuchanja kisha nitakupa dawa. Halafu nitakupaka mafuta ya ku**meremeta** hatimaye utapona. Utakuwa unang'aa wakati wote." Jongoo baada ya kuelezwa kuhusu tiba, aliuliza gharama za **matibabu**. Babu alimweleza kwamba gharama ni kubwa sana hivyo asingeweza kulipa. Babu alimwambia ili amsaidie amwachie mjukuu wake macho na yeye abaki na miguu. Jongoo aliwaza sana. Kwa kuwa aliona ana**chungulia kaburi,** akakubali ili atibiwe. Babu yake nyoka akaanza kumtibu.

Baada ya mwezi mmoja, Jongoo alipona kabisa. Alipopona, akatamani awe na macho yake kama mwanzo. Jongoo akamwambia Nyoka amrudishie macho yake na yeye achukue miguu yake. Nyoka akakataa na kumwambia kuwa, kama akimrudishia macho yake, ugonjwa utamrudia. Jongoo akalalamika, "Rafiki yangu, napata shida hata maadui siwaoni." Nyoka akamwambia, "Ngoja nikupe mbinu ya kujikinga na maadui. Ukihisi kitu usichokijua jikunje mwili wote." Tangu wakati huo, nyoka ana macho na hutembelea tumbo, na jongoo ana miguu.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 23 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Jongoo na Nyoka walikwenda kumtembelea nani?
2. Hapo mwanzo nani alikuwa anatembea harakaharaka na kuona kila kitu?
3. Kunguru aliwajibu nini Nyoka na Jongoo?
4. Nyoka na Jongoo walimfariji mwewe hadi lini?
5. Nani aliugua?
6. Jongoo na Nyoka walibadilishana nini?
7. Nani alimtibu Jongoo?
8. Alimtibu kwa makubaliano gani?
9. Baada ya kupona, Jongoo alidai nini?
10. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. kwaa
2. fariji
3. ahueni
4. tibu
5. matibabu
6. shawishi
7. meremeta

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo kwa kutumia miundo ifuatayo:**

1. __po__ .....................
   **Mfano:** *Wali<u>po</u>fika, walimkuta mama yao amelala fofofo.*

2. ............japokuwa ..........
   **Mfano:** *Juma alikwenda shuleni <u>japokuwa</u> alikuwa anaumwa.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 24 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Mbona…………
**Mfano:** *<u>Mbona</u> hupendi kusoma?*

4. Kama hutajali……………
**Mfano:** *<u>Kama hutajali</u> nipikie wali usiku.*

5. Hatimaye………………
**Mfano:** *<u>Hatimaye</u> mgeni rasmi alifika ukumbini*.

6. …………….. kisha ……………
**Mfano:** *Tuliwatazama wao, <u>kisha</u> tukaondoka*.

## Zoezi la 4 Nahau

**Toa maana ya nahau zifuatazo:**

1. bega kwa bega
2. kula chumvi nyingi
3. kata shauri
4. anua tanga
5. kufa moyo
6. chungulia kaburi
7. shika tama
8. aga dunia

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Andika umoja na wingi wa maneno yafuatayo:**

| | **Mfano: Umoja** | **wingi** |
|---|---|---|
| | mkono | *mikono* |
| | jiko | *majiko* |
| (i) | mguu | ________ |
| (ii) | ________ | macho |
| (iii) | ndege | ________ |
| (iv) | ________ | wadudu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | |
|---|---|---|
| (v) | rafiki | ________ |
| (vi) | chumvi | ________ |
| (vii) | ________ | magonjwa |
| (viii) | mkia | ________ |
| (ix) | jongoo | ________ |
| (x) | ________ | mabega |

## B. Kanusha sentensi zifuatazo:

**Mfano:** Watoto wanapenda wali.
*Watoto hawapendi wali.*

(i) Jongoo anatembea kwa tumbo.

(ii) Mwewe na nyoka walibadilishana macho na miguu.

(iii) Babu atamtibu nyoka.

(iv) Nyoka alifiwa na mtoto wake.

(v) Mwewe na kunguru walikuwa marafiki.

(vi) Mwanafunzi anachelewa darasani.

(vii) Mwalimu anafundisha masomo yote.

(viii) Mbwa alimkimbiza paka.

(ix) Mama atanituma sokoni.

(x) Mimi nilienda shambani kulima.

## C. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

**Mfano:** furaha - *huzuni*

| | | |
|---|---|---|
| (i) | ziba | ________ |
| (ii) | ugua | ________ |
| (iii) | kubali | ________ |
| (iv) | haraka | ________ |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) nenda ________

(vi) wema ________

(vii) ujasiri ________

(viii) mtiifu ________

**D. Andika KWELI au SI KWELI katika sentensi zifuatazo:**

(i) Maneno yanaundwa na konsonanti peke yake. ______

(ii) Nahau hazina maana yoyote. ________

(iii) Mbwa ni mnyama anayebweka. ________

(iv) Ndege ni chombo kinachosafiri angani. ________

(v) Gerezani ni mahali wanapowekwa wafungwa. ______

(vi) Nzige ni wadudu wenye sumu kali. ________

(vii) Vipepeo hupenda kurukaruka kwenye maua. ______

(viii) Panya ni waharibifu wa mazao. ________

FOR ONLINE USE ONLY

**E. Andika sentensi zifuatazo katika wakati uliopo.**

(i) Mwalimu atatufundisha vizuri wanafunzi wake.

(ii) Wao watalima shamba kubwa.

(iii) Kinyozi alininyoa vizuri.

(iv) Bibi alinifurahisha sana kwa hadithi zake nzuri.

(v) Mkulima amevuna mazao mengi.

(vi) Kiwavi alitembea kwa mbwembwe.

(vii) Mzee Ngedere amekula chumvi nyingi.

(viii) Watoto hucheza michezo mingi.



Kiswahil STD 5 New.indd 27 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Tunga sentensi kumi na nne (14) kwa kutumia jedwali lifuatalo:**

| | |
|---|---|
| kijana | walicheza vizuri |
| vijana | umechemshwa |
| kikombe | vimegongana kabatini |
| vikombe | kilivunjwa na mtoto |
| kiongozi | aliwashauri wananchi |
| viongozi | vilichanika |
| kitabu | kilisomwa na wanafunzi |
| vitabu | imeangushwa na upepo |
| mti | umekatwa |
| miti | yamekomaa |
| mwembe | |
| miembe | |
| mhindi | |
| mahindi | |

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 6 Utungaji

**Malizia hadithi hii kwa maneno yasiyopungua sabini (70). Tumia nahau zifuatazo:**

1. kata tamaa
2. ponea chupuchupu

Palikuwa na mzee mmoja aliyeitwa Mzee Mkungu. Aliishi katika Kijiji cha Itunja. Kijiji hiki kilikuwa karibu na pori. Mzee huyo alisifika kwa kilimo cha ndizi. Hata hivyo, mzee huyo alisumbuliwa sana na ngedere waliokuwa wanakula ndizi shambani mwake. Siku moja ngedere aliamka kuelekea shambani kwa mzee Mkungu. Alipofika alianza kuchapa mguu huku akiangaliangalia kama walinzi walikuwa karibu na shamba hilo. Bila kujua kuwa walinzi walikuwa wamejificha, ali……….



Kiswahil STD 5 New.indd 28 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Kauli zetu

*Katika sura hii, utajifunza kauli halisi na kauli taarifa. Pia, utajifunza kutunga sentensi kwa kutumia kauli hizo.*

**Fikiri**

1. Ulishawahi kutoa taarifa yoyote?
2. Taarifa hiyo uliitoa kwa nani?

**Ufahamu**

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

### Fabu apata zawadi

Fabu, Bera na Raja ni wanafunzi waliokuwa wanasoma katika Shule ya Msingi Ngindo. Wote wanasoma Darasa la Tano. Wanafunzi hawa waliishi katika kijiji kimoja kilichopo karibu na shule yao. Fabu alikuwa **bingwa** wa kuamka mapema kuliko Bera na Raja. Hivyo, mara nyingi aliwahi shuleni kuliko wenzake. Kila alipofika shuleni, aliwahi namba, kisha kuanza kufanya usafi wa eneo lake. Eneo lake lilionekana safi wakati wote. Pia, alikuwa akiwahi kurudi nyumbani mara tu baada ya kuruhusiwa shuleni. Vilevile, Fabu aliwa**heshimu** na kuwatii wazazi, walimu na watu wote waliomzunguka.

Tofauti na Fabu, Bera na Raja walikuwa wakichelewa kuamka. Hivyo, walichelewa kufika shuleni na mara nyingi walikosa namba. Maeneo yao ya shuleni yalionekana machafu. Wakati mwingine walikuta vipindi vimeanza. Baada ya kumaliza vipindi walichelewa kurudi nyumbani. Kutokana na tabia yao mara nyingi walipewa adhabu. Fabu alisikitishwa sana na kitendo hicho. Ali**azimia** moyoni kwamba siku moja atawauliza wenzake kwa nini walikuwa wakichelewa shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku moja Fabu, Bera na Raja wakiwa njiani kuelekea nyumbani, Fabu aliamua kuuliza swali lake lililokuwa likim**sumbua** kwa muda mrefu. Fabu aliuliza, "Marafiki zangu, kwa nini huwa mnachelewa kufika shuleni?" Bera na Raja wakiwa wametazamana walimjibu kwa dharau, "Heee….! Wewe vipi? Kwa nini unauliza?" Fabu alijibu kwa upole, "Samahani, kama nimewaudhi. Nilitaka kujua kwa sababu mara nyingi naona mnapewa **adhabu**. Kwani ninyi mnapenda adhabu?" Kusikia hivyo, Bera na Raja walitazama chini kisha wakajibu kwa pamoja, "Hapana ila huwa tunachelewa kuamka." Fabu aliwaonea huruma akawaambia kuwa kesho yake atawapitia asubuhi na mapema. Bera na Raja walikubali.

Siku iliyofuata, Fabu aliamka mapema na kwenda kuwapitia wenzake kama alivyoahidi. Waliongozana kuelekea shuleni. Wakiwa njiani, walikutana na Mzee Shibuni. Fabu alimsalimia lakini Bera na Raja hawakumsalimia. Mzee Shibuni aliwatazama akasema, "Nyie wanangu, mbona hamnisalimii? Muwe na **adabu** kama Fabu." Bera na Raja walinyamaza kimya. Mzee Shibuni aliamua kuondoka. Baada ya muda mfupi waliwasili shuleni. Walipata namba, kisha wakaenda kufanya usafi kwenye maeneo yao. Siku hiyo Bera na Raja hawakupewa adhabu. Walimshukuru Fabu kwa kuwapitia mapema.

Kadiri siku zilivyosogea, Fabu aliendelea kuwa mtiifu, mwenye adabu na bidii katika masomo yake. Kutokana na bidii na tabia yake njema, Fabu alikuwa akifanya vizuri katika masomo yake. Walimu walimpenda sana kutokana na bidii katika masomo na tabia yake njema. Hivyo, Fabu alisifika sana shuleni hapo kwa usafi, nidhamu bora, na kufanya vizuri katika masomo yake. Kwa kuwa shule yao ilikuwa inasisitiza masuala hayo, walikuwa wanatoa zawadi kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika maeneo mbalimbali wakati wa kufunga shule.

Siku ya kufunga shule ilipowadia, wanafunzi na walimu walikusanyika pamoja. Ilipofika wakati wa kutoa zawadi, mwalimu mkuu alianza kusoma majina ya wanafunzi waliofanya vizuri. Wanafunzi mbalimbali walipewa zawadi. Fabu, tofauti na wanafunzi wengine, alijipatia zawadi tatu tofauti. Mwalimu mkuu alimtaja Fabu kuwa ndiye aliyeongoza katika nidhamu, usafi, na ufaulu kwenye masomo yote. Wanafunzi wenzake na walimu walimshangilia kwa **nderemo** na **vifijo** kwa kupata zawadi hizo. Mwalimu



Kiswahil STD 5 New.indd 30 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mkuu alimu**usia** Fabu aendelee kufanya hivyo na wengine waige mfano huo. Fabu alifurahi sana na aliendelea kuwa na bidii siku zote.



## Zoezi la 1 Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Fabu, Bera na Raja ni wanafunzi wa shule gani?
2. Nani alikuwa anawahi shuleni kuliko wenzake?
3. Fabu alikuwa na tabia gani?
4. Bera na Raja walikuwa na tabia gani?
5. Katika habari uliyoisoma, ungependa kuwa kama nani? Kwa nini?
6. Swali gani lilikuwa likimsumbua Fabu?
7. Mzee Shibuni aliwaambia nini Bera na Raja?
8. Fabu alipata zawadi gani?
9. Kwa nini Fabu alipata zawadi nyingi?
10. Habari uliyoisoma inakufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. bingwa
2. heshimu
3. azimia
4. sumbua
5. adhabu
6. adabu
7. usia
8. nderemo
9. vifijo

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. ..........**kwamba**.............................

   **Mfano:** *Fabu alisema* ***kwamba*** *atafaulu masomo yote.*

2. ..........................**kuwa**.........................

   **Mfano:** *Mzee Shibuni aliwashauri* ***kuwa*** *wawe na adabu kama Fabu.*

3. .................. **kwa ajili ya**....................

   **Mfano:** *Mwalimu mkuu alinunua zawadi* ***kwa ajili ya*** *wanafunzi waliofanya vizuri.*

## Zoezi la 4 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila nahau.**

**Mfano:** kata tamaa - *poteza matarajio ya kupata kitu*

*Buchoti aliondoka mahali pale haraka akiwa ame****kata tamaa.***

*Nili****kata tamaa*** *ya kufika mapema baada ya kuchelewa treni.*

1. kaza kamba
2. piga mguu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. kata tamaa

4. piga maji

5. vunjika moyo

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Badili kauli halisi zifuatazo kuwa kauli taarifa.**

**Mfano:** Bera aliwaambia, "Nitajitahidi kuwahi kesho."
*Bera aliwaambia kwamba angejitahidi kuwahi siku iliyofuata.*

(i) Raja alituambia, "Siwezi kufanya usafi."
(ii) Mwalimu mkuu alisema, "Fabu ni mfano wa kuigwa."
(iii) Wote walijibu, "Tunapenda kula matunda."
(iv) Dada aliniambia, "Ninaomba maji ya kunywa."
(v) Baba alisema, "Tutakwenda kumsalimia mjomba."
(vi) Dereva alisema, "Gari limeishiwa mafuta."
(vii) Mwalimu alituasa, "Chezeni kwa uangalifu msiumizane."
(viii) Fabu aliuliza, "Kwa nini mnachelewa?"

**B. Badili kauli taarifa zifuatazo kuwa kauli halisi.**

**Mfano:** Kabude alisema kuwa hawezi kuja kwetu.
*Kabude alisema, "Siwezi kuja kwenu."*

(i) Mwalimu alisema kwamba angefundisha masomo yote.
(ii) Mzee alisema kwamba Tanzania ni nchi nzuri.
(iii) Kaka alisema kuwa angeanzisha bustani.
(iv) Chambi alisema kwamba angechimba mfereji wake mwenyewe.
(v) Baba alisema kuwa angenunua gari.
(vi) Mwalimu alihoji kujua nani alikuwa amefungua mlango.
(vii) Baba alisema kuwa sisi ni watoto wazuri.
(viii) Dada alituambia tusisogee karibu na moto.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 33 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C.** **Andika kauli halisi nne na kauli taarifa nne kutokana na habari uliyoisoma.**

**D.** **Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Bera alipata zawadi ya usafi.
*Bera hakupata zawadi ya usafi.*

(i) Bera na Raja ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Ngindo.
(ii) Mwanafunzi alijiandaa kupata zawadi siku ya kufunga shule.
(iii) Walimu na wanafunzi walimpongeza Bera kwa kupata zawadi.
(iv) Wanafunzi hawa wanafanya vizuri katika masomo yao.
(v) Wazazi wake walimpenda sana kutokana na tabia yake njema.
(vi) Huyu ndiye Kiranja Mkuu wa shule.
(vii) Usiku niliona mbalamwezi.
(viii) Mvua hunyesha kila asubuhi.
(ix) Jongoo hutembea kwa maringo.
(x) Kitabu chetu kina rangi ya kijani.

**E.** **Badili sentensi zifuatazo kuwa katika umoja.**

**Mfano:** Machungwa yameiva sana.
*Chungwa limeiva sana.*

(i) Wanafunzi walisoma vitabu vya hadithi.
(ii) Wazazi walifurahi kuwaona watoto wanacheza.
(iii) Wanafunzi wenzake walishangilia.
(iv) Wananchi wamechimba kisima.
(v) Majengo yamepakwa rangi nzuri.
(vi) Miti imepukutisha majani.
(vii) Meno yangu yanang'aa.
(viii) Kondoo wamevunjika miguu.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 34 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Tunga sentensi kumi kutokana na jedwali lililopo hapa chini.**

| | | |
|---|---|---|
| Mwalimu alituusia | | alikuwa darasani. |
| Fabu alijibu | | alikwenda sokoni. |
| Bera alimwambia | kwamba | tuwahi shuleni siku ya Jumatatu. |
| Raja alisema | kuwa | alienda shambani. |
| Nyakabi alitusihi | | ni muhimu kusoma kwa bidii. |
| | | alifanya usafi wa mazingira ya shule. |
| | | Jumatano ni siku ya usafi. |

## Zoezi la 6 Utungaji

**Kamilisha habari kwa kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku.**

kuwa, maelekezo, hongera, niliamka, wazazi, msimamizi, mama, chumba, mtihani, namba, vyote, kuelekea

Siku ya kufanya mtihani wa Darasa la Nne, (1) ________ mapema sana. Nilijiandaa na kupanga vifaa vyangu (2) ________ vya kutumia wakati wa mtihani. Baada ya hapo, nilienda kuwasalimia (3) ________ wangu. Nikasema, "Shikamoo!" Waliniitikia kwa furaha. Wakaniambia, "Jitahidi kufanya mtihani kwa umakini." Baada ya hapo niliwaaga na (4) ________ shuleni. Wanafunzi wenzangu walikuwa wameshafika. Mwalimu wa darasa alituita sote. Akatuambia, "Kumbukeni kuandika (5) ________ ya mtihani kwenye kila ukurasa." Muda mfupi baadaye, (6) ________ wa mtihani alifika akiwa na mitihani. Alipokelewa na mwalimu wetu kisha alioneshwa (7) ______ cha mtihani. Alikiangalia na kukikagua chumba hicho. Msimamizi akatuambia, "Ingieni darasani muda wa kuanza (8) _______ umekaribia." Tuliingia darasani kisha alituruhusu kuanza kufanya mtihani. Nilikumbuka maneno aliyosema mwalimu wa darasa kwamba soma (9) ________ yote kabla ya kuandika chochote. Ilipofika mchana, (10) ______ aliniletea chakula shuleni. Aliniuliza, "Je, mtihani ulikuwa mgumu?" Nilimjibu (11) _____ mtihani haukuwa mgumu sana. Niliporudi nyumbani, mama alinipokea kwa furaha. Akaniambia (12) _______ kwa kufanya mtihani.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Insha

*Katika sura hii utajifunza maana ya insha, hatua za uandishi wa insha na muundo wake. Pia, utaweza kuandika insha.*

**Fikiri**

1. Umewahi kuandika insha?
2. Ilikuwa inahusu jambo gani?

**Ufahamu**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Maisha ya Kanenge

Kanenge ni mwanafunzi wa Darasa la Tano katika Shule ya Msingi Ndondome. Alikuwa akiishi na shangazi yake tangu akiwa mdogo. Kila siku alikuwa anajiuliza moyoni mwake lini atapelekwa kwa wazazi wake. Siku moja ali**kaza moyo**; akamuuliza shangazi yake, “Kwa nini ninaishi kwako badala ya kuishi kwa wazazi wangu?” Shangazi alimjibu, “Kanenge tulia, ipo siku utajua.” Kanenge hakuridhishwa na jibu hilo lakini alinyamaza.

Shangazi aliendelea kupika jikoni. Aliwaza sana kuhusu swali aliloulizwa na Kanenge. Moyoni mwake alikuwa akijua ukweli kuwa Kanenge ni mtoto **yatima**. Wazazi wake walifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI. Kanenge pia ni mw**athirika** wa ugonjwa huo. Shangazi aliendelea ku**tafakari** njia nzuri ya kufikisha ujumbe huo kwa Kanenge.

Siku hiyo jioni, Kanenge alionekana hana furaha. Shangazi yake alimuuliza, “Kwa nini leo unaonekana mnyonge?” Kanenge alijibu, “Ninaumwa mwili mzima pia nahisi baridi kali sana.” Shangazi alimpatia vidonge viwili akamwambia, “Meza vidonge hivi kwa ajili ya kutuliza maumivu. Kesho asubuhi tutakwenda hospitalini.” Kanenge alimshukuru shangazi yake, alimeza vidonge hivyo, kisha akaenda kulala.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 36 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kesho yake asubuhi, shangazi aliwahi chumbani kwa Kanenge kumjulia hali. Kanenge alimwambia kuwa usiku alipata homa kali sana. Shangazi alimpa pole na kumshauri waende hospitalini. Walipofika hospitalini, waliingia katika chumba cha daktari. Kanenge alipewa nafasi ya kueleza matatizo ya afya yake. Kutokana na maelezo yake, daktari alipendekeza Kanenge afanyiwe pia vipimo vya maambukizo ya **virusi** vya UKIMWI. Hivyo, aliomba **ridhaa** kwa shangazi na kwa Kanenge mwenyewe. Wote walikubali. Kabla ya kuchukuliwa kipimo, daktari aliweka wazi kuhusu utaratibu wa kipimo hicho. Baada ya hapo, Kanenge alielekezwa chumba cha maabara. Akachukuliwa damu na haja ndogo.

Baadaye waliitwa kwenda kuchukua majibu. Kabla ya kutoa majibu, daktari aliwakumbusha tena maelezo aliyowapatia kabla ya kuchukuliwa vipimo. Baada ya hapo alisema vipimo vimeonesha kuwa Kanenge ana maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Kanenge alishituka aliposikia majibu hayo. Alilia kwa uchungu sana. Shangazi na daktari walimbembeleza kwa maneno yenye faraja. Baadaye Kanenge aliacha kulia. Daktari alisema, “Kesho ni siku ya kliniki kwa ajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Umlete akutane na watalaamu kwa ajili ya kupewa ushauri **nasaha**.”

Shangazi na Kanenge waliondoka kuelekea nyumbani. Walipofika nyumbani Kanenge alianza kulia tena. Alikuwa mtu mwenye mawazo mengi, sura ilidhoofu na alikuwa na dalili zote za mtu aliyekata tamaa ya maisha. Shangazi alijaribu kumbembeleza lakini Kanenge hakuonesha badiliko lolote. Muda wa kuandaa chakula ulipofika, shangazi alikwenda jikoni kupika. Kanenge akiwa sebuleni peke yake alifungua redio akaanza kusikiliza.

Ilipofika saa saba, alisikia mtangazaji akisema, “Karibuni ndugu wasikilizaji katika kipindi cha afya zetu. Mtaalamu wa afya atatufundisha kuhusu jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI.” Taarifa hiyo ilipenya katika masikio ya Kanenge, akasogea na kukaa karibu na redio. Mtaalamu alieleza mambo mengi yanayohusiana na jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI. Kipindi kilipokwisha, Kanenge alikimbia kuelekea jikoni, huku akiita kwa sauti ya furaha, “Shangazi! Shangazi! Shangaziiiiiii! Nakuita mbona husikii?” Shangazi alishtuka, akauliza kwa mshangao, “Kanenge umepatwa na nini tena?” Kanenge alijibu, “Nimepata taarifa njema sana redioni zinazohusu maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Napenda nikuambie.” Shangazi alikubali waketi sebuleni kwa ajili ya mazungumzo hayo.

Shangazi alifurahi baada ya kuona Kanenge yupo katika hali ya uchangamfu na mwenye sura ya tabasamu. Alimpatia nafasi Kanenge ili aongee. Kanenge



Kiswahil STD 5 New.indd 37 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

alisema, “Mtaalamu wa afya amezungumzia maana ya neno UKIMWI ni kifupi cha Upungufu wa Kinga Mwilini. Dalili zake ni homa kali za mara kwa mara, uzito kupungua, kuharisha, ngozi kusinyaa, mwili kukosa nguvu, kukosa hamu ya kula na vidonda mwilini. Njia zinazosababisha kuenea kwa ugonjwa huo ni kama vile kuchangia vitu vyenye ncha kali, yaani wembe, pini, sindano na kuchangia mswaki.”

Aliendelea kueleza kuwa mtu mwenye virusi vya UKIMWI anaweza akaishi kwa muda mrefu ikiwa atazingatia ushauri wa daktari. Mgonjwa anapaswa kula chakula bora, kuhudhuria kliniki, kutumia dawa kwa wakati pamoja na kujiepusha na maambukizo mapya. Kanenge alishusha pumzi akamtazama shangazi kwa jicho la upole kama ishara ya kumpa nafasi ya kuzungumza.



Shangazi alisema, “Pole sana Kanenge; wewe ni mtoto yatima wazazi wako walifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI. Ulipata maambukizo kwa bahati mbaya wakati wa kuzaliwa. Lakini usijali nitaendelea kukuhudumia kwa kukupatia mahitaji yako yote na kukupeleka hospitalini siku za kliniki.” Maelezo hayo yalimfurahisha sana Kanenge. Alimkumbatia shangazi yake, kisha akasema, “Asante sana kwa kunijali.” Shangazi akajibu, “Usijali, wahenga walisema **damu ni nzito kuliko maji**.”



Kiswahil STD 5 New.indd 38 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku iliyofuata shangazi alimpeleka Kanenge hospitalini. Walipewa ratiba ya siku za kuhudhuria kliniki. Baada ya kuimarika kwa afya yake, Kanenge aliendelea na masomo yake. Aliongeza bidii zaidi katika masomo, akafaulu mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi. Akaendelea na masomo ya sekondari hadi kidato cha sita. Baadaye alisoma na kuhitimu shahada yake ya kwanza. Kisha akaajiriwa kama mkurugenzi mkuu katika kiwanda cha maziwa kilichopo katika jiji la Shamnda. Hivi sasa ana familia yenye watoto watatu.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kanenge alikuwa anaishi na nani?
2. Habari uliyoisoma inahusu ugonjwa gani?
3. Kwa nini Kanenge aliambiwa arudi hospitalini?
4. Kanenge anafanya kazi gani?
5. Kwa nini Kanenge alilia akiwa hospitalini?
6. Taja dalili mbili za mtu anayeumwa ugonjwa wa UKIMWI.
7. Taja njia mbili zinazosababisha maambukizo ya virusi vya UKIMWI.
8. Andika kirefu cha neno UKIMWI.
9. Kanenge alipata elimu ya UKIMWI kupitia chombo gani cha habari?
10. Umejifunza nini kutokana na insha uliyoisoma?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. yatima
2. nasaha
3. athirika
4. ridhaa
5. tafakari
6. virusi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Nahau

**Tunga sentensi mbili kwa kila nahau.**

1. kaza moyo
2. kata roho
3. piga vijembe
4. kaa kitako
5. achia ngazi

## Zoezi la 4 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. ……………ni nzito kuliko maji.
2. Yaliyopita si ndwele, ……………….
3. Aliye juu, ……………………
4. ………………. si mtoro.
5. Mkono mtupu …………………...

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Onesha sentensi zenye kauli halisi au kauli taarifa.**

**Mfano:** Rafiki yangu aliniambia, "Ninasoma somo nilipendalo." _Kauli halisi_

Alisema kwamba hakukuelewa. _Kauli taarifa_

(i) Amesema kwamba hawezi kuja shuleni. ___________

(ii) "Tunakwenda sokoni," tulimwambia mama. _______

(iii) Mwalimu alisema kwamba tuwe makini. ________

(iv) Wanafunzi wote walijibu, "Tumemaliza kuandika zoezi." _____

(v) Dereva alituambia kuwa abiria wote tufunge mikanda kwa usalama wetu. _________

(vi) Ni muhimu kufahamu kuwa elimu haina mwisho. ________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) "Msicheze barabarani," kaka alituambia. ________

(viii) Shangazi aliniuliza, "Unaumwa nini?"______

(ix) Wote waliazimia kuwa wangejenga nyumba bora mwaka uliofuata. __________

(x) "Unatakiwa uanze kliniki," daktari alimwambia. _______

**B. Weka herufi kubwa mahali panapostahili katika sentensi zifuatazo:**

(i) baba alimuagiza ashura arudi mapema nyumbani.

(ii) hazole hajawahi kufika katika jiji la dodoma.

(iii) njalambaya hajamsalimia mama leo.

(iv) ameelekea upande wa kaskazini.

(v) mwalimu wetu ni mwenyeji wa wilaya ya butiama.

(vi) mimi nitasoma chuo cha ualimu butimba.

(vii) mto rufiji umefurika.

(viii) seni atanitembelea siku ya jumamosi.

(ix) mbuga ya serengeti ina wanyama wengi sana.

(x) shule zitafungwa mwezi novemba.

**C. Kuandika kinyume cha maneno yafuatayo:**

(i) ajuza ___________

(ii) injika ___________

(iii) joto ___________

(iv) ukaidi ___________

(v) cheka ___________

(vi) kimbia ___________

(vii) funua ___________

(viii) kosa ___________

(ix) chelewa ___________

(x) bandua ___________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Oanisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

| Sehemu A | | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | ajuza | (a) magonjwa |
| (ii) | balaa | (b) salamu za pole anazopewa mfiwa |
| (iii) | dharura | (c) madhara |
| (iv) | maafa | (d) burudisha |
| (v) | dhiki | (e) hali ya mazoea ya kufanya jambo fulani |
| (vi) | maradhi | (f) hatari |
| (vii) | tabia | (g) shida |
| (viii) | faragha | (h) mahali panapompa mtu nafasi kuzungumza kwa usiri |
| (ix) | rambirambi | (i) jambo lililotokea bila kutarajia |
| (x) | tumbuiza | (j) mwanamke mzee |

**E. Oanisha sehemu A na sehemu B ili kuleta maana.**

| Sehemu A | | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | Sisi ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Chiloko. Siku moja tuliandaa mchezo wa kirafiki. Tuliwaalika wenzetu wa Shule ya Msingi Chibuna. | (a) kiini cha insha |
| (ii) | Mchezo wa kirafiki | (b) kichwa cha insha |
| (iii) | Hadi mwisho wa mchezo hakuna timu iliyoona lango la mwenzake. | (c) hitimisho |
| (iv) | Siku ya mchezo ilipofika filimbi ilipulizwa wachezaji tukaingia uwanjani, na tukaanza kucheza. Mchezo ulianza kwa nguvu, na umati wa watu ulikuwa ukitushangilia. | (d) utangulizi |

## Zoezi la 6 Ufupisho

**Fupisha insha ya Maisha ya Kanenge kwa maneno yasiyozidi sabini (70).**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 42 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7 Utungaji

**Panga insha kwa kufuata mtiririko mzuri wa matukio. Tumia vifungu vya maneno A – D vilivyochanganywa. Kichwa cha habari kiwe "Bibi atembelewa na mjukuu wake."**

A. Siku moja alitembelewa na mjukuu wake aitwaye Shandola. Bibi alimpokea kwa furaha akasema, "Karibu sana mjukuu wangu. Lo! Siamini macho yangu kama leo nimepata mgeni hapa nyumbani kwangu." Shandola aliitikia, "Usijali bibi, nimeona leo nije kufurahi nawe katika mji huu wenye asali na maziwa." Baada ya salamu, alipewa kikombe cha maziwa ya mgando na viazi vya kuchemsha. Shandola alifurahi sana kula chakula hicho.

B. Bibi Semuyeka alikuwa anaishi katika kijiji cha Isenya. Alikuwa anaishi peke yake baada ya kufiwa na mume wake. Aliachiwa utajiri wa mifugo na mashamba ya mahindi, maharage, na migomba.

C. Jioni ilipofika, Shandola alimuaga bibi yake. Akamuahidi kumtembelea kila anapopata nafasi na kumsaidia kazi zitakazokuwepo. Bibi yake alimfungia zawadi za ndizi na maziwa. Wakaagana kisha akaondoka kurudi nyumbani kwao.

D. Baada ya kula aliingia jikoni, akakusanya vyombo vyote vichafu na kuviosha. Alifagia nyumba pamoja na uwanja wa bibi yake. Akakusanya nguo chafu na kuzifua. Bibi yake alimshukuru kwa kicheko cha furaha na kusema, "Ama kweli wahenga husema **mgeni njoo mwenyeji apone.** Umefanya mambo mazuri sana mjukuu wangu."

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 43 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Kutambua nafsi

*Katika sura hii, utasoma habari kuhusu "Sisi na wao." Kutokana na habari hiyo, utaweza kujifunza kuhusu nafsi zote tatu kwa kuzingatia umoja na wingi. Pia, utajifunza namna ya kutumia nafsi hizo katika sentensi au kifungu cha habari.*

**Fikiri**

Chunguza sentensi zifuatazo, kisha taja aina ya nafsi katika kila sentensi.

(a) Wewe uliondoka nyumbani mapema.

(b) Mimi nilifaulu mtihani wa Darasa la Nne vizuri sana.

(c) Yeye amefua nguo zake zote.

**Ufahamu**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Sisi na wao

Mimi ni Fikira. Nina marafiki wanne, Choki, Zuna, Ndina na Nito. Sisi ni wanafunzi wa Darasa la Tano katika Shule ya Msingi Idona. Tuna marafiki wengine katika Shule ya Msingi Chokoni. Wao ni Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau. Tulizoea kujiita "sisi" na kuwaita marafiki zetu "wao." Nao walizoea kujiita "sisi" na kutuita sisi "wao." Sisi na wao tunaishi vijiji jirani. Sisi tunaishi katika kijiji cha Mkulicho. Wao wanaishi katika kijiji cha Mkocho. Sisi na wao ni washindani wa michezo wa siku nyingi.

Wakati wa likizo ya mwezi wa kumi na mbili tuliamua kufanya mashindano ya michezo mbalimbali. Mashindano hayo yalifanyika katika kijiji chetu. Sisi na wao tulishiriki katika mashindano hayo.

Kulikuwa na michezo mitano. Michezo hiyo ni kukimbiza kuku, kukimbia, kuvuta kamba, mpira wa miguu na kuruka kamba. Mimi nilipenda sana



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kukimbiza kuku na kuvuta kamba. Zuna alipenda kukimbiza kuku na kucheza mpira wa miguu. Yeye siku hiyo ali**kuwa na shauku** sana ya kukimbiza kuku. Watu wali**furika** kuja kuangalia mashindano kati yetu. Miongoni mwa hao watu alikuwepo pia babu kikongwe. Kila kikundi kiliingia uwanjani kwa mikogo. Mara tukasikia sauti ya babu **kikongwe** ikisema, "Ninyi wajukuu zangu, kumbukeni umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu." Sisi na wao tulianza kushindana kukimbiza kuku.



Kila kundi lilikimbiza kuku kwa ustadi mkubwa. Babu kikongwe alituangalia sana huku aki**tabasamu**. Katika mashindano hayo, Dano ndiye aliyekuwa anakaribia kumkamata kuku. Sisi tulianza kukata tamaa. Hata hivyo, mimi nilikuwa namfuata nyuma yake. Nikasikia wenzangu wakiniambia, "Wewe kazana! Kazana! Kazana." Nikapata nguvu za ajabu, nikaongeza mbio, hadi nikaweza kumkamata kuku. Sisi tukaanza kushangilia kwa furaha, huku wenzangu wakinipigia makofi. Mimi nikawaambia wenzangu, "Ninyi mmenitia moyo kwa kuniambia nikazane." Choki, Zuna, Ndina na Nito walifurahi sana huku wakirukaruka. Wakanibeba juujuu wakisema, "Wewe umekuwa mfano wa kuigwa na unastahili **pongezi**."

Baada ya hapo, mimi, Choki, Zuna, Ndina na Nito tulipumzika pembeni pamoja na babu kikongwe tukiongea na kufurahi. Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau walikuwa wamekaa pembeni wakituangalia huku wakionesha



Kiswahil STD 5 New.indd 45 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huzuni. Walikuwa hawana furaha kwa sababu hawakushinda mchezo wa kukimbiza kuku. Babu kikongwe akawaita wakaja pale tulipokaa. Babu kikongwe akawaambia, “**Asiyekubali kushindwa si mshindani.** Furahini tu wajukuu zangu.”

Sisi na wao tukaanza kuongea pamoja. Sisi tulibeba vyakula kama maziwa na mihogo. Wao walibeba vyakula kama mayai, viazi na nyama. Sisi tulitamani vyakula vyao na wao walitamani vyakula vyetu. Tuliamua tule chakula kwa pamoja. Mimi nilikula sana hadi nikaanza kutapika. Rafiki zangu wakanicheka sana. Babu kikongwe akawakemea kwa kunicheka. Ila akaniambia, “Unapokula, ukijisikia umeshiba, usiendelee kula kwa tamaa.”

Baada ya kumaliza kula, mimi nilitamani kuondoka pamoja na Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau. Hii ilitokana na utamu wa vyakula vyao. Choki, Zuna, Ndina na Nito walinikataza. Babu kikongwe akaniambia, “Wewe mjukuu wangu sio vizuri kuondoka nao. Ni vema urudi nyumbani mapema.” Mimi niliamua kuondoka nao. Tulifika kijiji cha Mkocho giza likiwa limeanza kuingia. Wazazi wao waliniambia nirudi nyumbani kwetu. Nikaanza kurudi nyumbani kukiwa na giza **totoro**. Njiani nilikuwa naogopa, nikawa nakimbia. Ghafla nikakanyaga kitu kilichoteleza. Nikaanguka chini, huku nikipiga kelele, “Mama wee! Mama wee nakufa.” Nilihisi alikuwa nyoka. Kumbe lilikuwa ni ganda la ndizi.

Nilipofika nyumbani niliwakuta wazazi wangu wamekasirika sana. Nikawaomba **msamaha**. Baba akasema, “Usirudie tena, na hutashiriki mashindano ya michezo mwaka mzima.” Mama akasema, “Ama kweli **samaki mkunje angali mbichi**.” Niliwaahidi sitarudia tena, halafu nikawasimulia **kisa** chote.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kina nani walikuwa washindani wa michezo siku nyingi?
2. Marafiki hao walikutana wakati wa likizo kufanya nini?
3. Taja aina za michezo iliyokuwepo siku hiyo.
4. Rafiki zake Fikira walimwambia nini Fikira wakati wanakimbiza kuku?
5. Kwa nini Fikira aliwafuata Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau kijijini kwao?



Kiswahil STD 5 New.indd 46 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Babu kikongwe aliwaambia nini Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau?
7. Fikira alipewa adhabu gani na baba yake?
8. Kwa nini Fikira alipewa adhabu?
9. Fikira alipofika nyumbani kwa wazazi wake alifanya nini?
10. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. furika
2. kikongwe
3. tabasamu
4. pongezi
5. totoro
6. msamaha
7. kisa

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. ………_ngali_……………._ngali_……..

   **Mfano:** *Kibua angalisoma kwa bidii angalifaulu vizuri sana.*

2. ……………….mara …………..

   **Mfano:** *Sikutochi alikuwa anatembea mara akakimbizwa na mbwa.*

3. ………………..ila …………………

   **Mfano:** *Alikuwa anaumwa ila alikula vizuri.*

4. Hatimaye ……………………………..

   **Mfano:** *Hatimaye maji yaliongezeka baada ya mvua kunyesha.*

5. ……………..._ngeli_ …………_ngeli_………

   **Mfano:** *Wao wangelicheza kwa bidii wangelishinda mashindano.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 47 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

**Mfano:** *Ajidhaniaye amesimama aangalie asianguke.*

*Chovya chovya humaliza buyu la asali.*

1. Asiyekubali kushindwa……………………………
2. ……………................... angali mbichi.
3. Hakuna marefu ……………………………………
4. Ukicheka na ngedere, ……………………………
5. Umoja ni nguvu, …………………………………..

## Zoezi la 5 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo:**

1. kata mtama
2. enda mwayo
3. piga jeki
4. vunja mbavu
5. kata kamba

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

**A. Pigia mstari neno linalowakilisha nafsi katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** *Mimi ninacheza mpira.*

(i) Wewe unaimba vizuri.

(ii) Yeye anasoma kwa bidii.

(iii) Ninyi mnakula chakula.

(iv) Wao wanaruka kamba.

(v) Sisi tunacheka sana.

(vi) Mimi na wewe ni marafiki sana.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Sisi tunapika na wao wanalima.

(viii) Ninyi na wao mtakuja kesho.

(ix) Mwalimu anatupenda sisi.

(x) Siamini kama mimi ndiye mshindi.

**B. Jaza nafsi sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi kwenye sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** ____ tunalima bustani kubwa ya nyanya.

*Sisi tunalima bustani kubwa ya nyanya.*

(i) ___ ninakula chakula.

(ii) ___ anaimba wimbo mzuri.

(iii) ___ wanacheza vizuri sana.

(iv) ___ mnaruka juu.

(v) ___ unalia kwa sauti.

(vi) ___ tutarudi keshokutwa.

**C. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** Bwina _____**lienda** nyumbani mapema.

*Bwina **alienda** nyumbani mapema.*

(i) Juma ___**naenda** nyumbani.

(ii) Wao ___**nacheza** vibaya.

(iii) Mimi ___**licheza** vizuri sana.

(iv) Sisi ____**lishinda** mashindano.

(v) Wewe __**lichelewa** kurudi nyumbani.

(vi) Ninyi ___**liwahi** kufika.

(vii) Yeye ___**lichapwa** na baba yake.

(viii) Sisi na wao ___**lifurahi** pamoja.

(ix) Watoto ___**nacheza** mpira vizuri.

(x) Mwalimu ___**litusisitiza** tusome kwa bidii.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 49 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Sisi tunacheza mpira.
*Sisi hatuchezi mpira.*

(i) Mimi ninapiga kelele.

(ii) Wewe unapiga makofi.

(iii) Ninyi mnapiga piano.

(iv) Wao wanaimba wimbo.

(v) Yeye anaingia darasani.

(vi) Mwalimu anawaangalia wanafunzi.

**E. Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku.**

(i) ______ ninakwenda shuleni kila siku.

(a) Wewe
(b) Sisi
(c) Mimi
(d) Yeye

(ii) Baba amelima shamba kubwa sana. Katika neno "amelima" silabi inayoonesha nafsi ni ipi?

(a) li
(b) me
(c) ma
(d) a

(iii) Tunaimba kabla ya kuondoka shuleni. Katika neno "tunaimba" silabi inayoonesha nafsi ni ipi?

(a) tu
(b) a
(c) na
(d) tu pamoja na na

(iv) Wingi wa neno "unywele" ni:

(a) manywele.
(b) unywele.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 50 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) nywele.
(d) minywele.

(v) Sentensi "Mwalimu anaingia darasani kila siku" ukanushi wake ni:
(a) Mwalimu hatoingia darasani kila siku.
(b) Mwalimu haingii darasani kila siku.
(c) Mwalimu hutoingia darasani kila siku.
(d) Mwalimu hawataingia darasani kila siku.

(vi) Wao walikuwa hawana furaha. Taja aina ya nafsi katika sentensi hii.
(a) Nafsi ya pili wingi
(b) Nafsi ya kwanza wingi
(c) Nafsi ya tatu wingi
(d) Nafsi ya tatu umoja

(vii) ______________ mlikuwa washindi.
(a) Sisi
(b) Yeye
(c) Wao
(d) Ninyi

(viii) Wingi wa neno "mimi" ni:
(a) wao
(b) sisi
(c) ninyi
(d) wengi

**F. Soma sentensi zifuatazo, kisha zibadilishe ziwe katika nafsi ya pili wingi.**

**Mfano:** Wao wanacheza mpira wa miguu.
*Ninyi mnacheza mpira wa miguu.*

Wewe unalia nini?
*Ninyi mnalia nini?*

(i) Wao ni wanafunzi wa Darasa la Sita.
(ii) Wanasoma Shule ya Msingi Mbugano.
(iii) Siku moja wakiwa darasani mvua kubwa yenye upepo mkali ilianza kunyesha.
(iv) Ghafla paa la darasa lao liliezuliwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 51 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Wao walishtuka sana; wakaanza kukimbia nje.
(vi) Wakati wanakimbia nje, paa liliwaangukia baadhi yao na kuwaumiza.
(vii) Walioumia walipelekwa hospitalini haraka.
(viii) Walitibiwa na kurudi nyumbani.

## Zoezi la 7 Utungaji

**Malizia kuandika habari ifuatayo kwa maneno kati ya sabini hadi themanini (70 – 80).**

Jina langu naitwa Bwina. Ninasoma Darasa la Tano. Ninacheza ngoma vizuri. Nilichaguliwa kucheza ngoma siku ya mahafali ya Darasa la Saba. Nilijiandaa kucheza vizuri siku hiyo. Siku ilipofika ni…...............

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 52 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Wanyama wafugwao

*Katika sura hii, utasoma hadithi inayohusu kisa cha wanyama kuishi na binadamu. Pia, utaweza kusimulia hadithi. Vilevile, utajifunza majina na faida za wanyama wafugwao na vyakula wanavyokula.*

**Fikiri**

1. Je, nyumbani kwenu mnafuga wanyama?
2. Taja majina ya wanyama mnaowafuga.
3. Je, wanawapa faida gani?

**Ufahamu**

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Kisa cha wanyama kuishi na binadamu

Hapo zamani za kale, wanyama wote waliishi porini. Walikuwa wakishirikiana kutafuta chakula. Simba alikuwa anashirikiana na ng'ombe, mbuzi, kondoo, mbwa, paka na punda. Walikuwa marafiki wa karibu sana. Waliishi kama ndugu wa kuzaliwa.

Walikubaliana kutafuta chakula kwa zamu, huku wengine wakibaki nyumbani kulinda watoto wao wasiliwe na maadui. Chakula kilikuwa kinapatikana kwa shida sana. Ilifika zamu ya simba kwenda kutafuta chakula. Aliwaaga wenzake na kuondoka kwenda porini. Huku nyuma, ng'ombe aliwashawishi wenzake kwa kusema, "Jamani, naona maisha ya huku porini yanazidi kuwa magumu siku hadi siku. Tuondoke twende tukaishi kwa binadamu." Mbwa akauliza, "Hawa watoto wa simba tutawafanyaje?'' Ng'ombe akajibu, "Tuwatoroke.''

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wote walikubali. Ng'ombe akawaambia, "Mkisikia sauti yangu moo... moo... moo..., kila mmoja akimbie na watoto wake.'' Watoto wa simba watakuwa wamelala. Baada ya muda mfupi ng'ombe alifanya hivyo, na wanyama wote wakakimbia. Simba aliporudi kutoka mawindoni hakuwakuta wenzake. Akashituka alipowaona wanawe wamebaki peke yao. Akapiga ukelele wa majonzi "Mamaaa! Uuuwi! Watoto wangu watacheza na nani?'' Alitazama huku na huku hakuona rafiki yake hata mmoja. Alilia sana kwa uchungu. Aliendelea kuwatafuta lakini hakufanikiwa kuwaona.

Ng'ombe na wenzake wakiwa njiani kuelekea kwa binadamu, walianza kuzungumza. Paka alisema, "Tutafanya nini ili binadamu aweze kutukaribisha nyumbani kwake?'' Punda akasema, "Kila mmoja aeleze atamsaidia nini binadamu." Ng'ombe akasema, "Mimi nitamwambia binadamu kwamba nitampatia maziwa, **siagi** na **samli**. Pia, nitamsaidia kulima mashamba na kumpatia **samadi**."

Punda akasema, "Mimi nitamsaidia kubeba mizigo na kulima mashamba kwa jembe la ku**kokota**.''

Mbwa akasema, "Mimi nitamlindia nyumba mchana na usiku." Pia, nitalinda mashamba yake dhidi ya wanyama waharibifu. Nitakula chakula kidogo anachokula yeye."

Paka akasema, "Mimi nitamwambia binadamu kwamba nitalinda mazao yake dhidi ya panya wanaoharibu mazao. Nitalala kwenye ghala la kuhifadhia mazao. Nitakula baadhi ya vyakula anavyokula yeye."

Kondoo na mbuzi wao walisema, "Sisi tutamwambia binadamu kwamba tutampatia maziwa. Chakula chetu ni majani. Atatujengea **zizi** moja."

Baada ya mazungumzo hayo, usiku uliingia. Walikuwa wamechoka wakalala **pango**ni. Alfajiri waliendelea na safari yao ya kwenda kwa binadamu. Binadamu alipowaona, alishtuka na kuogopa. Akasema, "Ondokeni! Ondokeni ninyi wanyama." Wanyama wakambembeleza wakiomba awasikilize kwanza."



Kiswahil STD 5 New.indd 54 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Aliendelea kwa kuwauliza “Mnataka niwasaidie nini?” Ng’ombe akajibu, “Sisi tunaomba tuishi na wewe. Tumechoka maisha ya porini. Unavyotuona hapa tunahitaji msaada wako.” Aliuliza tena, “Mtanisaidia nini endapo mtaishi na mimi?” Walijieleza kama walivyojadiliana wakiwa njiani.

Baada ya kusikia maelezo ya kila mnyama, akawauliza tena, “Je, hamtanidhuru?” Walijibu, “Hapana hatutakudhuru. Tutakuwa watiifu siku zote.” Binadamu akawakubalia. Akasema, “Nimesikia maelezo ya kila mmoja wenu. Hivyo, kuanzia sasa tutaishi pamoja. Kila mnyama atekeleze kile alichoahidi kukifanya bila manung’uniko.” Wote walifurahi kuanza kuishi na binadamu. Mpaka sasa wanyama hao wanaishi na binadamu. Walikubaliana wasiwe wanaongea kabisa isipokuwa kama watakuwa na tatizo watoe mlio tu.



Kiswahil STD 5 New.indd 55 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo kutokana na hadithi uliyoisoma.**

1. Simba aliishi na wanyama gani?
2. Nani aliyewashawishi wenzake kwenda kuishi kwa binadamu?
3. Kwa nini wanyama waliamua kwenda kuishi na binadamu?
4. Wakati wanyama wanatoroka, watoto wa simba walikuwa wanafanya nini?
5. Paka alisema atamsaidia nini binadamu?
6. Nani alisema atamsaidia binadamu kubeba mizigo?
7. Walipokuwa njiani usiku wanyama hao walilala wapi?
8. Nani alielekeza wanyama wafanye kazi bila manung'uniko?
9. Binadamu aliwauliza nini wanyama?
10. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. pango
2. pembe
3. zizi
4. samadi
5. kokota

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 56 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Nahau

**Oanisha maneno ya sehemu A na sehemu B katika jedwali lifuatalo:**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) aga dunia | (a) fanya kila njia |
| (ii) tia fora | (b) fanya kazi pamoja |
| (iii) uma sikio | (c) shangaa |
| (iv) fanya juu chini | (d) fanya kwa uvivu |
| (v) vunja urafiki | (e) fundishwa nidhamu |
| (vi) zaa matunda | (f) pata faida |
| (vii) shika adabu | (g) pita kiasi kwa uzuri au shinda kwa uzuri |
| (viii) zembea kazi | (h) nong'oneza |
| (ix) bega kwa bega | (i) kufa |
| (x) pigwa butwaa | (j) maliza kazi |
| | (k) ruhusu watu waende |
| | (l) kata uhusiano |

## Zoezi la 4 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Mshika mbili ……………..
2. ………… harabu ya nzima.
3. Bandu bandu ……………..
4. ………… ndiye rafiki wa kweli.
5. Baniani mbaya, ……………
6. ……… ungali maji.
7. ………….., vimeundwa.
8. Bora lawama, ……………..
9. Fimbo ya mbali ……………..
10. ………….. nafuu ya mchukuzi.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 57 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A.** **Katika orodha ya wanyama wafuatao andika wanyama wafugwao.**

nyangumi, paka, twiga, swala, ng'ombe, chui, kondoo, kifaru, tembo, nyati, punda, sungura, kiboko, mbwa, nguchiro, fisi, ngedere, mbuzi, nyani

**B. Chora wanyama watatu wanaofugwa unaowafahamu.**

**C. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati ujao.**

(i) Ngoma zinafikisha ujumbe kwa jamii.
(ii) Leo ni sikukuu ya wakulima.
(iii) Mwalimu alimpongeza mwanafunzi kwa kufaulu masomo yake.
(iv) Wanafunzi wanatembelea mbuga za wanyama.
(v) Mama anakwenda kazini.
(vi) Safari ilipoanza tulifurahi sana.
(vii) Mkuu wa shule alitoa shukurani kwa mgeni rasmi.
(viii) Waliimba nyimbo za shangwe.
(ix) Shule yetu imeshika nafasi ya kwanza katika masomo yote.
(x) Shangazi aliniletea zawadi.

**D. Tunga sentensi kumi kutokana na jedwali lifuatalo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Pale | kijijini<br>nyumbani<br>shuleni<br>mtaani<br>sokoni | palikuwa na | duka kubwa<br>mti mkubwa<br>visima vya maji<br>wanyama wa kufugwa<br>watoto wengi |

**E. Andika umoja na wingi katika maneno yafuatayo:**

**Mfano:** chuma - _vyuma_

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (i) | ____________ | wanyama |
| (ii) | ____________ | masega |



Kiswahil STD 5 New.indd 58 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) kidari ____________
(iv) maji ____________
(v) ____________ michezo
(vi) mtemi ____________
(vii) mwanafunzi ____________
(viii) paka ____________
(ix) mto ____________
(x) ____________ vituo

**F. Herufi zifuatazo zimechanganywa. Zipange ili zilete maneno sahihi.**

**Mfano:** ngede - *ndege*
wamb - *mbwa*
kaap - *paka*

(i) mbeto ____________
(ii) mbagu ____________
(iii) wigat ____________
(iv) neon ____________
(v) rigin ____________
(vi) ukis ____________
(vii) moot ____________
(viii) tabuki ____________
(ix) mubiz ____________
(x) panud ____________

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 6 Utungaji

**Tunga hadithi fupi inayomhusu mnyama mmoja anayefugwa ukieleza faida zake na chakula anachokula.**



Kiswahil STD 5 New.indd 59 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Wanyama wa porini

*Katika sura hii, utajifunza kuhusu wanyama mbalimbali wa porini, utataja majina ya wanyama hao na sifa zao. Pia, utasoma, utasimulia na utaandika hadithi kwa mtiririko sahihi wa matukio.*

**Fikiri**

1. Je, ulishawahi kuwaona wanyama wa porini?
2. Uliwaona wapi?
3. Uliwaona wanyama gani?

**Ufahamu**

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Mkutano wa wanyama

Hapo zamani za kale, wanyama wote waliishi pamoja porini. Walishirikiana katika kazi mbalimbali. Mfalme wao alikuwa Tembo. Walimpenda sana kutokana na busara zake. Kwa muda mrefu waliishi kwa ku**tangatanga** na kupata chakula kwa taabu. Mfalme wao alifikiria sana kuhusu kutatua tatizo hilo. Alipata wazo kuwa awaite wanyama wote kujadili namna ya kutatua tatizo hilo. Alimwita Simba na kumuagiza, “Nenda ukawaalike wanyama wote kwa ajili ya mkutano wa kesho.”

Simba alijibu, “Nitatekeleza mfalme wetu.” Simba aliondoka na kunguruma u! Uuu! Uuu…! Kisha akasema kwa sauti nene, “Tangazo maalumu! Kesho, wanyama wote tunatakiwa kufika kwa mfalme wetu Tembo. Tutajadili namna ya kupata chakula. Asikose mnyama hata mmoja, uu... uu... uuu...!” Wanyama wote walipata taarifa hiyo. Kesho yake, wanyama wote walikutana kwa mfalme. Walikuwepo Simba, Fisi, Nyani, Ngedere, Swala, Nyati, Kifaru, Kiboko, Chui na wanyama wengine.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mkutano ukaanza. Mfalme akasema, “Ndugu zangu, mnaona tunavyopata shida ya chakula?” Wanyama wote wakaitikia, “Ndiyooo...!” Mfalme akaendelea, “Sasa nimewaita ili tujadili tatizo hili.” Mjadala ulianza. Kila mnyama alitoa wazo lake. Nguchiro alisema, “Tushikamane kwa umoja wetu tulime shamba la pamoja. Mvua ikinyesha tupande mazao. Tutatumia samadi ili mazao yetu yastawi vizuri. Tutavuna na kuyahifadhi katika ghala.” Wanyama wote walikubaliana na wazo hilo.



Mfalme akasema, “Nawashukuru sana kwa kutambua tatizo letu na kulipatia ufumbuzi. Ardhi yetu ina **rutuba** ya kutosha. Wahenga wetu walinena kwamba **umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu**. Kwa hiyo, kila mmoja wetu aandae jembe, shoka na panga ili kesho tuanze kulima.” Siku ilipofika, wanyama wote walifika shambani. Mfalme akamwambia Twiga, “Kwa kuwa wewe ni mrefu kuliko wanyama wote, angalia ni mnyama yupi hakufika na utoe taarifa.” Twiga aliangalia huku na huko na kugundua kuwa Kiboko hakufika.

Wanyama walifanikiwa kulima shamba kubwa. Mvua iliponyesha walipanda mazao mbalimbali. Walipomaliza kupanda, mfalme Tembo akasema, “Kwa kuwa Kiboko hakushiriki kabisa tutamfukuza maana hana ushirikiano na sisi. Tuwe na zamu ya kulinda shamba letu.” Wakakubaliana na mawazo



Kiswahil STD 5 New.indd 61 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya mfalme. Siku ya kwanza Simba alianza kulinda akasema, “Akija Kiboko nitam**finyangafinyanga**.” Wanyama wakacheka hahaha! Wanyama wengine wakaondoka. Muda mfupi Kiboko alifika akamsalimia Simba, “Habari ya leo ndugu?” Simba alikaa kimya. Kiboko akasema, “Nywele zako zimekaa **shaghalabaghala** naomba nikusuke. Mimi ni **msusi** mzuri. Wanyama wote watakupenda na utachaguliwa kuwa mfalme baada ya Tembo ku**staafu**.'' Simba alifurahi kusikia atapendeza na kurithi ufalme.

Kiboko akamwambia, “Twende pale juu ya mti nianze kukusuka.'' Walikwenda juu ya mti. Akaanza kumsuka huku akifunga manyoya yake kwenye mti. Alipomaliza kumfunga, akamwambia, “Sasa naenda kula mazao na kuyaharibu.” Kiboko akashuka chini; Simba akabaki ana**ning'ini**a juu ya mti. Alipiga yowe wanyama wenzake wakakimbia kuja kumsaidia. Walimkuta Simba ananing'inia juu ya mti. Wakamsaidia kumtoa. Aliwasimulia kisa chote.

Siku iliyofuata, wanyama walitawanyika kuzunguka shamba zima wakimsubiri Kiboko. Walijificha katika majani wakiwa na silaha. Siku hiyo kiboko hakutokea. Hawakukata tamaa. Waliendelea kulinda mazao yao siku hadi siku.

Baada ya siku kadhaa kupita, Kiboko alienda tena katika shamba la wanyama. Alifika shambani na kuangalia huku na huko, lakini hakuona kitu. Wakati huo wanyama walikuwa wamejificha wakimsubiria Kiboko aingie shambani ndipo wamkamate. Alipoingia shambani, ghafla wanyama wakatokea pande zote wakiwa na silaha.

Kiboko aliangalia namna ya kuwatoroka lakini akashindwa kwa sababu wanyama walimzingira. Walimkamata na kumpeleka kwa Mfalme Tembo. Mfalme akasema, “Ndugu yangu **siku za mwizi ni arobaini.** Adhabu yako ni kuondoka huku nchi kavu ukaishi majini kuanzia sasa. Ninaamuru jeshi langu likupeleke ziwani au mtoni, ukaishi huko siku zote za maisha yako.” Hadi leo Kiboko anaishi majini na hutoka nje wakati wa usiku kutafuta chakula. Mchana anaogopa kutoka nje kwa hofu ya kukamatwa na wanyama.



Kiswahil STD 5 New.indd 62 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo kutokana na hadithi uliyoisoma.**

1. Nani alikuwa mfalme wa wanyama?
2. Mfalme alimwita nani kutoa tangazo la mkutano?
3. Mnyama yupi ni mrefu kuliko wanyama wengine?
4. Mnyama yupi hakufika kwenye mkutano?
5. Nani alitoa wazo la kulima shamba?
6. Wanyama walilima mazao ya aina gani?
7. Mazao waliyoyavuna waliyahifadhi wapi?
8. Mnyama gani alining'inizwa juu ya mti?
9. Mnyama gani alifukuzwa nchi kavu?
10. Kwa nini alifukuzwa nchi kavu?
11. Hadithi hii inakufundisha nini?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. tangatanga
2. finyanga
3. shaghalabaghala
4. msusi
5. staafu
6. ning'inia
7. rutuba

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Ndege mjanja ………………
2. Tamaa mbele, ……………..
3. ……………… hajikwai.
4. …………. yavuta heri.
5. Usipoziba ufa, ……………..
6. Si vyote ving'aavyo …………..
7. ……………. halikuli likakwisha.
8. ………………. si mkulima.
9. Ndege hutua kwenye mti, ……………..
10. …………… halina ubani.

## Zoezi la 4 Vitendawili

**Tegua vitendawili vifuatavyo:**

1. Daima hunifuata nyuma, nikimfuata hunikimbia. ________
2. Anaoga sana lakini hatakati.___________
3. Mwanangu akichanganyika na wenzake simtambui. _____
4. Hesabu yake haina faida._______________
5. Kila ukiwakuta wamejiandaa kupigana. _______________
6. Kisima cha mfalme hakikauki. _____________
7. Maji ya kisima changu hayanyweki .__________
8. Watoto wa Mungu hawahesabiki. ______________
9. Ukoo wetu hauishiwi safari._________________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 64 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Nahau

**Toa maana ya nahau zifuatazo:**

**Mfano:** zunguka mbuyu - *kupokea rushwa*

1. mwaga unga……………
2. ana ndimi mbili……………
3. mezea mate……………
4. piga mbiu…………
5. kaa chonjo……………
6. shika mkia…………..
7. tia chumvi……………
8. angua kicheko…………

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha maneno yenye maana sawa kutoka sehemu A na B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) nyati | (a) aibu |
| (ii) maringo | (b) sherehe |
| (iii) paka | (c) boma au banda la wanyama |
| (iv) samadi | (d) munyu |
| (v) zizi | (e) majivuno |
| (vi) nasaha | (f) neema |
| (vii) chumvi | (g) mawaidha |
| (viii) fedheha | (h) mbogo |
| (ix) riziki | (i) mbolea ya kinyesi cha wanyama |
| (x) tafrija | (j) nyau |

**B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

(i) kizuri ______________

(ii) mbali ______________

(iii) tamu ______________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 65 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) huzuni ____________

(v) zomea ____________

(vi) tandika ____________

(vii) uza ____________

(viii) fuma ____________

(ix) ongea ____________

(x) shika ____________

**C. Pigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.**

**Mfano**: mbu, <u>mbuzi,</u> mbung'o, nzi, kunguni

mahindi, kunde, <u>miwa</u>, maharage, njegere

(i) ng'ombe, nyani, chui, njiwa, kondoo

(ii) ukucha, kidole, mkono, kiwiko, uso

(iii) bata, mbuni, nyoka, chiriku, kunguru

(iv) rede, dama, ukuti, karata, chupa

(v) shati, blanketi, kofia, suruali, kaptura

(vi) wali, ugali, chai, pilau, kande

(vii) fisi, chui, simba, ng'ombe, nyani

(viii) kambare, kaa, perege, sangara, kibua

**D. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku.**

| kilele, mshahara, kidari, yatima, semadari, karne, mbuni, chui, tetekuwanga, almasi |
|---|

**Mfano:** Chukua kwa nguvu ________

*Chukua kwa nguvu <u>nyakua.</u>*

(i) ______ ni aina ya ugonjwa unaoambukiza.

(ii) Mnyama mkali mwenye madoamadoa anayeishi porini _____

(iii) Miaka mia moja ________

(iv) Sehemu ya juu kabisa ya mlima_________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 66 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Ndege mkubwa zaidi na mwenye mbio sana_____

(vi) Mtoto aliyefiwa na wazazi_______

(vii) Aina ya kitanda________

(viii) Aina ya madini magumu yanayopatikana ardhini____

## Zoezi la 7 Ufupisho

**Fupisha hadithi ya "Mkutano wa wanyama" kwa maneno yasiyozidi sabini (70).**

## Zoezi la 8 Utungaji

**Simulia ziara katika mbuga yoyote ya wanyama kwa kufuatu mtiririko wa picha zifuatazo, kisha uandike hadithi fupi.**






Kiswahil STD 5 New.indd 67 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Maua

*Katika sura hii, utasoma shairi linalohusu maua. Utajifunza kuhusu majina ya maua, sifa zake, utunzaji na umuhimu wake. Pia, utatunga shairi fupi kulingana na vitu vinavyokuzunguka katika mazingira yako.*

### Fikiri

1. Je, unapenda maua?
2. Unapenda maua gani?
3. Uliona wapi maua?

### Ufahamu

*Soma na ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.*

#### Bustani ya maua

1. *Enyi jicho la taifa, **tunu** kuwaandalia,*
*Motomoto zenu sifa, darasa hili sikia,*
*Yangu haya maarifa, kinga mikono pokea,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

2. *Maua hupatikana, kila kona duniani,*
*Yapo yenye kupatana, yakipandwa **masikani**,*
*Ua hutambulikana, kwa pua au **uoni**,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*



Kiswahil STD 5 New.indd 68 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. *Miti ina utajiri, wa maua mbalimbali,*
*Na matunda hu**shamiri**, karibu hata kwa mbali,*
*Wanyama ndege wakiri, hufurahia **manzili**,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

4. *Twatambua kwa majina, **ua sa' sita** murua,*
*Rangi zake kuziona, machoni zinavutia,*
*Ma**waridi** kupangana, rangize kugombania,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

5. ***Asumini** nalo ua, jioni linachanua,*
*Harufu nzuri kutoa, popote linanukia,*
***Shada** kutengenezea, na nywele kuzifungia,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

6. *Lingine ua la **mwafu**, mafuta kutengeneza,*
*Huvutia kwa harufu, ni nzuri ya kupendeza,*
***Mkayakaya** nasifu, ua lake huangaza,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

7. *Matunzo yalo muhimu, palizi hata mbolea,*
*Maji yasiwe adimu, kumbuka ku**pogolea**,*
*Na viwavi wasidumu, kuisitisha **ghasia**,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

8. *Faida kujipatia, ni nyingi kupitiliza,*
*Bayana kukutajia, utajiri natangaza,*
*Wapambaji hununua, ili kumbi kupendeza,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 69 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

9. ***Ghaibuni*** *twapeleka, na wao huyanunua,*
***Dola*** *nyingi twazishika, uchumi kuunyanyua,*
*Epuka kuhangaika, sasa ajira pokea,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

10. *Wito wangu sasa kwenu, jembe na mbegu mshike,*
*Shuleni kumbuka kwenu, maua mahali pake,*
*Maua* ***fahari*** *yenu, na kanuni mzishike,*
*Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.*

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Shairi ulilosoma linahusu nini?
2. Taja majina matatu ya maua yaliyomo katika shairi ulilosoma.
3. Taja aina mbili za wadudu wanaopenda kutembelea sehemu zenye maua.
4. Ua la asumini hutumika kufanyia nini?
5. Maua yana faida gani?
6. Ubeti wa saba unazungumzia nini?
7. Mdudu gani ametajwa kuwa ni hatari kwenye maua?
8. Maua yanapopelekwa ughaibuni taifa hupata nini?
9. Kwa nini mwandishi anasema maua ni kitu bora?
10. Umejifunza nini kutokana na shairi hili?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. tunu
2. fahari
3. pogolea
4. ughaibuni
5. dola
6. ghasia
7. shamiri

## Zoezi la 3 Miundo

**Soma miundo ifuatayo, kisha tunga sentensi tatu kwa kila muundo.**

1. …….........vingi…………
   **Mfano:** *Mwalimu ameleta vitabu vingi leo*.
2. ………….. wengi………..
   **Mfano:** *Bata wengi wanaogelea bwawani*.
3. …………mingine……………
   **Mfano:** *Migomba mingine ilinyauka*.
4. ……………wengine……………
   **Mfano:** *Wachezaji wengine watafika leo*.

## Zoezi la 4 Methali

**Chagua methali sahihi kutoka kwenye kisanduku, kisha iandike mbele ya maelezo yanayoonesha matumizi yake.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.
Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.
Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
Ukiona vyaelea, ujue vimeundwa.
Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

1. Mzee Mdolo alikuwa anatetea tabia ya wizi iliyokuwa inafanywa na mtoto wake hapo kijijini. Siku moja, mtoto wake aliiba mbuzi kwenye zizi la baba yake. Tangu siku hiyo, mzee Mdolo aliamini kuwa ..................

2. Kijiji cha Namile kilivamiwa na chui. Mwenyekiti alipiga mbiu ya mgambo. Wanakijiji walikusanyika haraka wakaenda kumsaka. Baada ya muda mfupi chui alikuwa ameuawa. Sasa nimeamini kuwa ............................

3. Nilikuwa mchezaji mzuri wa mpira wa miguu kwa miaka mingi. Siku moja nilivunjika mguu uwanjani. Wachezaji wote waliniacha uwanjani nikigaagaa kwa maumivu. Kamokene alinionea huruma; alinibeba na kunipeleka hospitalini. Nikakumbuka usemi wa wahenga usemao kuwa ................

4. Shazimwa ni mwanafunzi aliyekuwa na mahudhurio hafifu shuleni. Walimu na wazazi wake walimshauri kuacha tabia hiyo lakini hakuwasikia. Katika matokeo ya kuhitimu elimu ya msingi, Shazimwa ndiye mwanafunzi pekee aliyefeli mtihani. Sasa amejifunza kuwa .....................................

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Herufi zifuatazo zimechanganywa. Zipange ili uunde maneno sahihi.**

**Mfano:** muaa - *maua*

kutabi - *kitabu*

muwali - *walimu*

(i) ngizirama ____________

(ii) diwari ____________



Kiswahil STD 5 New.indd 72 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) pipevoe __________

(iv) lisaa __________

(v) ntuu __________

(vi) dalo __________

(vii) woti __________

(viii) funawanzi __________

(ix) chonima __________

(x) fasi __________

**B. Andika nyakati za sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Ulicheza mpira. *wakati uliopita*

Wote watapatana kesho. *wakati ujao*

Watoto wanakimbia taratibu. *wakati uliopo*

(i) Sisi tulicheza mchana kutwa. __________

(ii) Wananchi wanafanya usafi wa mazingira kwa pamoja. ______

(iii) Mjomba atakupitia shuleni. __________

(iv) Unapanga kazi yako vizuri. __________

(v) Nitafaulu mtihani wangu wa mwisho. __________

(vi) Unauliza kuhusu nini?__________

(vii) Kwa nini ulipigwa?__________

(viii) Nitasoma masomo ya ziada. __________

(ix) Alikuwa mvumilivu sana. __________

(x) Atakusanya vitabu vya masomo yote. __________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 73 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yafuatayo:**

**Mfano:** kidonda – *jeraha*

(i) nusuru __________

(ii) pongezi __________

(iii) jogoo __________

(iv) mkonge __________

(v) katuni __________

(vi) wigo __________

(vii) msitu __________

(viii) hatimaye __________

(ix) ama __________

(x) faulu __________

**D. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano kisha, jaza nafasi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** Mdogo wangu *amelala* tangu asubuhi. (*amerala, amelala*)
Mama amepata *jeraha* mguuni. (*jelaha, jeraha*)

(i) Garimoshi hupita juu ya________. (*reli, leli*)

(ii) Mama amepika_________tangu mchana. (*ugari, ugali*)

(iii) Kaka amefanya kazi ya ________zaidi ya wiki moja. (*ukuri, ukuli*)

(iv) Mjomba ni __________wa miwa. (*mkulima, mkurima*)

(v) Ntula alipika________. (*maharage, mahalage*)

(vi) Kabilo _________mtihani wa Darasa la Nne. (*amefaulu, amefauru*)

(vii) ___________wiki ijayo. (*shule zote zitafungwa, mashule yote yatafunga*)

(viii) Baada ya kufiwa na wazazi wake alipewa_______. (*rambirambi, lambilambi*)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wingi.**

**Mfano:** Anacheza uwanjani kila siku.
*Wanacheza uwanjani kila siku.*

(i) Mwalimu amemwadhibu mwanafunzi.
(ii) Rangi ya ua hili inavutia sana.
(iii) Dada yangu anapenda ua la rangi nyekundu.
(iv) Kipepeo anapenda kuruka kwenye maua.
(v) Nyumbani kwangu nimepanda ua.
(vi) Mgomba umestawi karibu na banda la kuku.
(vii) Kiti anachokalia mwalimu kimevunjika.
(viii) Kijiji chetu kipo nyuma ya mlima.
(ix) Kisima cha shule kimetengenezwa.
(x) Mwanafunzi aliyechelewa amepewa adhabu.

**F. Pigia mstari neno ambalo ni tofauti na maneno mengine.**

(i) treni, baiskeli, pikipiki, bajaji, punda
(ii) kuku, bata, njiwa, kunguru, kanga
(iii) mchungwa, mpira, mpera, mchenza, mfenesi
(iv) gauni, blauzi, kanga, kanzu, sketi
(v) meli, boti, gari, ngalawa, jahazi
(vi) sahani, kijiko, ungo, kikombe, bakuli
(vii) alizeti, pamba, karanga, mawese, maharage
(viii) mshororo, ubeti, mizani, majigambo, vina

## Zoezi la 6 Utungaji

Tunga shairi lenye beti mbili. Kichwa cha shairi kiwe ni **Maua yetu**.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 75 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Shughuli za kila siku

*Katika sura hii, utasoma habari kuhusu shughuli za kila siku. Pia, utaweza kueleza shughuli unazofanya nyumbani na shuleni. Vilevile, utaweza kuandika ratiba ya shughuli za kila siku na habari fupi kwa mpangilio mzuri.*

**Fikiri**

1. Shughuli gani huwa unazifanya unapokuwa shuleni?
2. Umewahi kuona ratiba?
3. Je, wewe una ratiba ya shughuli za kila siku za nyumbani na shuleni?

**Ufahamu**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Chiku anafanya nini kila siku?

Siku moja mwalimu wetu wa Kiswahili alileta redio darasani. Alifungua redio na kutuambia sote tusikilize. Lengo lake lilikuwa tusikilize mazungumzo kati ya mtangazaji wa redio na mshindi wa shindano la uandishi wa insha. Mshindi huyo alikuwa ni mwanafunzi wa Darasa la Tano aitwaye Chiku. Wote tulikaa kimya na kuanza kusikiliza kwa makini mazungumzo hayo yaliyotu**kosha mioyo**.

**Mtangazaji:** Chiku, hongera sana kwa kushinda shindano la uandishi wa insha. Jitambulishe kwa watoto wenzako wanaokusikiliza na uwaeleze **ratiba** yako ya kila siku.

**Chiku:** Kwa jina ninaitwa Chiku Maneno. Ninasoma Darasa la Tano. Huwa ninaamka saa 12:00 asubuhi kila siku.

**Mtangazaji:** Hebu tueleze, ukishaamka unafanya shughuli gani?

**Chiku:** Nikiamka ninakwenda kuwasalimu wazazi wangu. Baada ya hapo, ninasafisha chumba changu. Kisha ninapiga mswaki na kuoga.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 76 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mtangazaji:** Aha! Ni jambo jema sana Chiku kuwasalimia wazazi kabla ya yote. Ukishaoga unafanya nini?

**Chiku:** Ninavaa nguo za shule na kupata kifungua kinywa, kisha ninakwenda shuleni saa 12:45 asubuhi. Nifikapo shuleni, husafisha eneo langu mpaka muda wa kuingia darasani unapo**wadia.**

**Mtangazaji:** Kumbe shule yenu inazingatia sana usafi! Vipindi huwa vinaanza saa ngapi hadi saa ngapi?

**Chiku:** Vipindi huanza saa 2:00 asubuhi. Hapo tunakuwa na vipindi vitatu halafu tunapumzika saa 4:00 mpaka saa 4:30 asubuhi.

**Mtangazaji:** Baada ya mapumziko huwa mnafanya nini?

**Chiku:** Tunaingia tena darasani na kusoma vipindi vitatu. Vipindi hivyo hukamilika saa 6:30 mchana halafu tunapumzika kidogo. Tunacheza nje kwa dakika kumi halafu tunaingia tena darasani kusoma mpaka saa 8:00 mchana. Kuanzia saa 8:00 mpaka saa 8:30 mchana ni muda wa kufanya **shughuli** za usafi wa mazingira.

**Mtangazaji:** Kwa hiyo huwa unarudi nyumbani saa ngapi?

**Chiku:** Huwa tuna**tawanyika** kurudi nyumbani saa 8:30 mchana. Nikifika nyumbani nakula na kupumzika. Ifikapo saa 12:00 jioni, huwa ninawafungia kuku na mabata bandani.

**Mtangazaji:** Asante sana Chiku. Je, siku za Jumamosi na Jumapili huwa unafanya nini? Una**piga usingizi** tu nyumbani?

**Chiku:** Hapana. Sipendi ku**piga usingizi.** Jumamosi na Jumapili siendi shuleni, lakini ninafanya kazi za nyumbani. Jumamosi, kuanzia saa 2:00 mpaka saa 3:00 asubuhi, huwasaidia wazazi shughuli mbalimbali. Shughuli hizo ni kama vile kutunza na ku**mwagilia** bustani ya mbogamboga. Nikitoka bustanini, nafua **sare** zangu za shule na kujisomea.

**Mtangazaji:** Je, kuna ugumu wowote katika kufanya shughuli zote hizo kwa utaratibu?

**Chiku:** Hapana, kwangu hakuna ugumu wowote.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 77 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mtangazaji:** Vizuri sana. Unawezaje kufanya shughuli zako hizo bila kusahau?

**Chiku:** Mimi hutumia **ratiba** niliyoiandaa. Ratiba ni muhimu sana kwa kuwa inaniwezesha kufanya mambo kwa utaratibu bila kusahau.

**Mtangazaji:** Asante sana Chiku. Nakushauri uendelee na tabia hiyo. Bila shaka watoto wanaokusikiliza wamejifunza jambo muhimu sana.

Baada ya mahojiano kuisha mwalimu wetu akazima redio. Alituuliza maswali **kadha wa kadha** na kututaka tuandike insha kuhusu shughuli za kila siku. Mwisho akatu**usia** tuwe na tabia ya kujitengenezea ratiba. Ratiba ni muhimu kwa sababu hutuongoza katika shughuli zetu za nyumbani na shuleni. Sote tuliahidi kuiga mfano wa Chiku.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kwa nini mwalimu alileta redio darasani?
2. Nani alikuwa anahojiwa na mtangazaji?
3. Chiku huamka saa ngapi kila siku?
4. Wanafunzi hufanya nini shuleni kuanzia saa 6:30 mpaka 6:40 mchana?
5. Chiku humaliza vipindi muda gani?
6. Kwa nini ni muhimu kufuata ratiba?
7. Chiku hufanya shughuli gani siku ya Jumamosi kuanzia saa 2:00 mpaka 3:00 asubuhi?
8. Usafi wa mazingira hufanyika muda gani shuleni?
9. Taja siku ambazo Chiku haendi shuleni.
10. Umejifunza nini kutokana na habari ya Chiku?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 78 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. ratiba
2. mwagilia
3. sare
4. shughuli
5. tawanyika
6. wadia
7. usia

## Zoezi la 3 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo, kisha tunga sentensi moja kwa kila nahau.**

**Mfano:** vaa miwani - *kulewa*

*Yeye alitembea kwa kuyumbayumba kwa sababu alikuwa amevaa miwani.*

1. piga usingizi
2. kosha moyo
3. piga mwayo

## Zoezi la 4 Methali

**Chagua jibu sahihi linaloeleza maana ya methali zifuatazo:**

1. Hakuna marefu yasiyo na ncha.
   (a) Hakuna jambo lenye mwanzo mrefu.
   (b) Hakuna jambo lisilokuwa na mwisho.
   (c) Hakuna kitu kisicho kirefu.
   (d) Hakuna jambo lenye mwanzo na mwisho.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 79 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**2.** Mtaka yote kwa pupa hukosa yote.

(a) Anayetaka vitu vingi kwa tamaa hawi na mwisho mzuri.

(b) Mtaka yote anapata mengi kwa pupa.

(c) Asiyetaka yote kwa pupa hukosa yote.

(d) Mtaka yote kwa pupa hana pupa.

**3.** Jungu kuu halikosi ukoko.

(a) Jungu kuu ni kubwa sana.

(b) Tajiri huhifadhi pesa kwenye chungu.

(c) Jungu kubwa halina ukoko mwingi.

(d) Tajiri hawezi kukosa chochote mfukoni.

**4.** Mchumia juani hulia kivulini.

(a) Mchumia juani hutoa machozi kwa sababu ya maumivu.

(b) Mtu anayetafuta kwa shida huyafaidi mavuno yake kwa raha.

(c) Ukichumia juani utaona kivuli.

(d) Anayevuna juani hatakula kivulini kwa raha.

**5.** Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.

(a) Anayekufaa kwenye dhiki ana marafiki wengi.

(b) Rafiki wa kweli ni yule anayekufaa wakati wa raha.

(c) Mtu anayekusaidia wakati wa shida ndiye rafiki.

(d) Rafiki ndiye anayekuletea dhiki.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 80 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.**

**Mfano:** Tunaandika insha kuhusu ratiba ya siku.
*Tutaandika insha kuhusu ratiba ya siku.*

(i) Chiku alihojiwa na mtangazaji wa redio.

(ii) Mwalimu amekuja na redio darasani.

(iii) Yeye humwagilia bustani siku ya Jumamosi.

(iv) Wanafunzi hupumzika saa 4:00 asubuhi.

(v) Kila mmoja wetu aliandaa ratiba yake ya siku.

(vi) Ninawasalimia wazazi wangu asubuhi.

(vii) Ninaamka asubuhi na mapema.

**B. Andika ratiba ya siku ya Jumatano kuhusu shughuli unazozifanya nyumbani na shuleni kuanzia asubuhi unapoamka mpaka usiku unapokwenda kulala.**

**C. Jaza sehemu zilizoachwa wazi katika ratiba ifuatayo kwa kuzingatia maelezo ya Chiku.**

| Siku | Muda | Shughuli |
|---|---|---|
| Jumapili | Saa 12:00 jioni - saa 1:00 jioni | ……………………… |
| Jumatatu | Saa 4:00 asubuhi - saa 4:30 asubuhi | ……………………… |
| Jumanne | Saa ……………… | Kutawanyika kutoka shuleni. |
| Jumatano | Saa……………….. | Kufungia kuku na mabata bandani. |
| Alhamisi | Saa 2:00 asubuhi | ……………………… |
| Ijumaa | Saa 6:30 mchana - saa 6:40 mchana | ……………………...... |
| Jumamosi | Saa ……………… | Kufua sare za shule. |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 81 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6 Utungaji

**Chunguza picha zifuatazo zinazoonesha shughuli za Adamu kwa siku ya Jumamosi. Elezea kila shughuli na muda ambao inafanyika.**



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 82 7/23/21 3:14 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Hali ya hewa

*Katika sura hii, utajifunza kuhusu aina ya hali ya hewa inayopatikana katika mazingira yako. Pia, utajifunza faida za hali ya hewa katika mazingira yako. Vilevile, utajifunza vitu katika umoja na wingi pamoja na ukubwa na udogo.*

### Fikiri

1. Umeshawahi kusikia kuhusu hali ya hewa?
2. Ni aina ipi ya hali ya hewa inayopatikana katika mazingira yako?
3. Unajua faida yoyote ya hali ya hewa?
4. Unadhani mvua na upepo huleta madhara yoyote?

**Ufahamu**

*Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali.*

### Hali ya hewa

**Mvua:** Mimi ni mvua. Mimi ni matone ya maji ambayo hudondoka kutoka kwenye mawingu. Mimi nikinyesha, huwapa maji. Huwapa maji kwa ajili ya **kukata kiu** zenu. Huipa maji mimea na mifugo. Hii husababisha kilimo kuendelea. Hivyo, huongeza pato la taifa. Mimi niki**nyesha** sana, yaani nikizidi kiwango, husababisha **madhara**. Huweza kusababisha vifo vya watu na mifugo. Huweza kuharibu mimea, nyumba, barabara na madaraja. Mimi wakati ninanyesha, mnaweza kunikimbia au kujifunika kwa vitu mbalimbali kwa kuniogopa. Kuna wakati nisiponyesha, husababisha **ukame.** Ukame husababisha mimea kutoota vizuri. Pia, husababisha uhaba wa maji. Hii huweza kusababisha njaa na hata watu au wanyama kufa kabisa. Ndio

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maana nisiponyesha muda mrefu, watu huanza kuniombea ninyeshe. Mimi hupimwa na kipima mvua. Hakuna kama mvua?



**Upepo:** Mimi ni upepo. Mimi ni hewa isiyotulia, na **aghalabu,** huenda kwa **kasi**. Mimi hutokea kwa ku**vuma** pande zote za nchi.Huweza kuvuma Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi. Mimi pia huweza kuwapa nishati ya umeme. Mimi husaidia baadhi ya mimea kuzidi kuzaliana. Pia, huweza ku**peperusha** mbegu mbalimbali za mimea na kusababisha kwenda kuota sehemu nyingine. Hatimaye mimea hukua na kuweza kuwapa chakula. Mimi nikizidi sana, yaani nikiwa mkali sana, huleta madhara. Madhara kama vile kuezua mapaa na kuangusha miti. Hivyo, ninaweza kusababisha vifo vya watu au wanyama kutokana na madhara hayo. Mnabisha? Nije? Mimi huweza kufukuza mvua. Nikizidi sana, huwa mnajifunika nguo nyingi. Mimi hupimwa na kipima upepo. Hakuna kama upepo?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Joto:** Mimi ni joto. Mimi ni hali ya kuwepo na **umotomoto** katika nchi kutokana na jua au moto. Mimi huwaondolea baridi. Ndio maana watu wakipata baridi sana, huota moto ili kupata joto. Wakati mwingine, ninaweza kusababisha **fukuto** na kuleta mvua. Mimi husaidia kukuza mimea mikubwa kwa midogo inayohitaji joto. Mimi nikizidi sana, huleta madhara. Naweza kusababisha ukame ambao huleta uhaba wa maji. Pia, huathiri kilimo kwa sababu ninaweza ku**nyausha** mimea. Ninaweza kusababisha magonjwa ya ngozi. Pia, kupungukiwa na maji mwilini, na hatimaye, kusababisha vifo. Kuna wakati nikizidi, watu hupunguza nguo walizovaa. Mimi ninapimwa na kipima joto. Hakuna kama joto?



**Baridi:** Mimi ni baridi. Mimi ni hali ya hewa isiyokuwa na joto. Mimi huwaondolea joto na kuwafanya mjisikie vizuri. Mimi hustawisha baadhi ya mazao. Mimi nikizidi sana, husababisha watu kuota moto. Pia, mnajifunika nguo nzito na kuvaa masweta kujikinga na mimi. Vilevile, huweza kuwasababishia wengine muugue magonjwa kama vile nimonia na kukohoa. Wengine mnaweza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ku**babuka** na kuharibika ngozi zenu kwa sababu yangu. Hakuna kama baridi?



**Ukungu:** Mimi ni ukungu. Mimi ni mawingu mepesi, meupe yanayotanda angani na kusababisha kutoona vizuri. Mimi huwa na majimaji au **unyevu**. Mimi hutegemea mazingira ya sehemu fulani. Mimi huweza kusababisha mawingu na mvua. Kuna wakati nikitanda huharibu baadhi ya mazao. Ngoja nije muone! Ninaweza kuwazuia msione vizuri baadhi ya vitu katika maeneo yenu. Hakuna kama ukungu?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kati ya mvua, upepo, joto, baridi na ukungu ungependa kuwa nani? Kwa nini?
2. Mvua alijigamba kuwa ana faida gani?
3. Mvua ina madhara gani?
4. Taja faida za joto zilizoelezwa.
5. Taja faida za baridi zilizoelezwa.
6. Upepo una madhara gani?
7. Kwa nini ukungu unaweza kusababisha baadhi ya vitu kutoonekana vizuri?
8. Joto lina madhara gani?
9. Ukungu una madhara gani?
10. Majigambo hayo yanakufundisha nini?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. nyesha
2. madhara
3. ukame
4. aghalabu
5. kasi
6. vuma
7. peperusha
8. umotomoto
9. fukuto
10. nyausha
11. babuka
12. unyevu

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 87 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Nahau

**Tunga sentensi moja kwa kila nahau zifuatazo:**

**Mfano:** lala unono

*Jana Donia alikula akashiba, akalala unono.*

1. kata kiu
2. kula njama
3. kufa maji
4. kufa kikondoo
5. piga winda

## Zoezi la 4 Vitendawili

**Andika vitendawili vyenye majibu yafuatayo:**

1. ugonjwa
2. kujikwaa
3. firigisi
4. njia
5. kuota moto

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Mtoto alilia sana wakati wa usiku.

*Mtoto hakulia sana wakati wa usiku.*

(i) Mvua kubwa imenyesha kuamkia leo.
(ii) Upepo ulivuma sana jana.
(iii) Baridi ilipungua msimu uliopita.
(iv) Joto limeongezeka wiki hii.



Kiswahil STD 5 New.indd 88 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Ukungu unatanda zaidi maeneo ya mlimani.
(vi) Miti mingi mikubwa imeanguka chini.
(vii) Mashamba mengi yatakauka kwa ukame.
(viii) Watoto wengi wanapenda sana michezo.
(ix) Mama alipika chakula kitamu.
(x) Kunjele anafanya fujo darasani.

### B. Andika KWELI au SI KWELI katika sentensi zifuatazo:

**Mfano:** Ukungu unaweza kuitwa unyevu. *SI KWELI*

Baridi husababisha watu wengine kuota moto. *KWELI*

Joto husababisha vitu kutoonekana vizuri. *SI KWELI*

(i) Mvua huweza kusababisha mafuriko. _______
(ii) Joto haliwezi kusababisha magonjwa ya aina yoyote. _______
(iii) Baridi haina faida kabisa. _______
(iv) Upepo huweza kuharibu nyumba na mimea. _______
(v) Ukungu hutanda kila siku angani. _______
(vi) Kuelewa hali ya hewa iliyopo katika mazingira yako ni muhimu. _______
(vii) Upepo huvuma kutoka Kaskazini kuelekea Kusini tu. _______
(viii) Mvua kubwa huweza kusababisha ukame. _______

### C. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku.

kali, mkali, kubwa, mingi, wengi,
mengi, ndogo, kikubwa

**Mfano:** *Mvua kubwa imenyesha juzi.*

(i) Watu ____ hupenda kunywa maji ya mvua.
(ii) Upepo _____ umeharibu makazi.
(iii) Mimea _____ humea kipindi cha mvua.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 89 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Shamba ____ limestawi vizuri.

(v) Joto _____ limekausha mazao mengi.

(vi) Maji_______ yameharibu mimea.

(vii) Kibuyu______ kina maziwa.

(viii) Bustani ______ inatosha kwa mboga za nyumbani.

## D. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wingi.

(i) Mti mkubwa umevunjika usiku wa kuamkia leo.

(ii) Upepo mkali umevuma mchana huu.

(iii) Kiti kimevunjika chote.

(iv) Mtoto anapenda kunywa maziwa.

(v) Mmea umestawi vizuri.

(vi) Daraja limevunjika baada ya mvua kubwa kunyesha.

(vii) Jino la juu linauma.

(viii) Ukuta umebomoka kutokana na ufa.

(ix) Ungo umetengenezwa kwa rangi nzuri.

(x) Gurudumu la baiskeli lilipinda baada ya kugongwa na gari.

## E. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

(i) asubuhi

(ii) mchana

(iii) kubwa

(iv) inama

(v) njaa

(vi) mlimani

(vii) kushoto

(viii) zama

(ix) vaa

(x) faida

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Tunga sentensi kumi (10) tofauti kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *Ndoo kubwa imeanguka chini.*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ndoo | kikubwa | kimeanguka | |
| Mti | kubwa | limeanguka | |
| Embe | kidogo | umeanguka | chini |
| Mimea | mkubwa | imeanguka | |
| Kitabu | mdogo | zimeanguka | |
| | mikubwa | | |
| | ndogo | | |
| | dogo | | |
| | midogo | | |

**G. Kamilisha sehemu B kwa kujaza sifa za majina yaliyoorodheshwa sehemu A.**

**Mfano:** mti *mrefu*

| Na. | Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | mbwa | |
| (ii) | maembe | |
| (iii) | usiku | |
| (iv) | wanafunzi | |
| (v) | kiti | |
| (vi) | twiga | |
| (vii) | meno | |
| (viii) | ukuta | |
| (ix) | karatasi | |
| (x) | kiatu | |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 91 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**H. Tumia herufi za maneno yafuatayo kuunda maneno mengine.**

**Mfano:** toa - *ota*

(i) wazi
(ii) tatu
(iii) tai
(iv) lewa
(v) zoa
(vi) lima
(vii) mbao
(viii) uza
(ix) bisha
(x) ona

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 6 Utungaji

**Andika habari yenye maneno kati ya sabini hadi themanini (70 - 80) kuhusu hali ya hewa katika mazingira yako.**

*Maswali yafuatayo yatakuongoza.*

1. Hali ya hewa ni nini?
2. Eleza hali ya hewa katika mazingira yako.
3. Taja faida za hali ya hewa katika mazingira yako.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Familia yetu

*Katika sura hii, utasoma habari kuhusu familia yetu. Utajifunza umuhimu wa familia. Pia, utaandika insha kuhusu umuhimu wa familia.*

**Fikiri**

1. Familia ni nini?
2. Unaishi na nani nyumbani?
3. Kila mmoja wenu anafanya kazi gani nyumbani?

**Ufahamu**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Umuhimu wa familia

Palikuwepo na familia moja yenye furaha. Watu wa familia hiyo waliishi kwa furaha na kushirikiana kwa kila jambo. Mchana walifanya kazi pamoja, jioni waliketi **upenuni** na kula pamoja. Baada ya chakula, kila mmoja alitoa burudani na kituko chake. Babu ndiye aliyewavutia zaidi kwa michapo yake ya kusisimua na kufurahisha.

Katika familia hiyo, walikuwepo watoto wawili mapacha, Kulwa na Doto. Kulwa alipenda sana kushirikiana na wenzake. Doto alipenda kujitenga na kufanya mambo mengi peke yake. Babu yake alimshauri kuwa ushirikiano katika familia ni muhimu sana. Alisema, “Hakuna binadamu anayeweza kuishi peke yake kwa mafanikio.” Hata hivyo, Doto alimpuuza.

Alipokuwa kijana, nduguze walipozidi kumshauri ashirikiane na wenzake, Doto alikasirika. Akaamua kwenda kuishi porini. Aliondoka nyumbani kwa **makeke.** Huko porini alitembea kwa mwendo wa kibabe na hatua **madhubuti.**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 93 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Alichagua eneo zuri porini akaandaa makazi na kulima shamba kubwa. Alilima kwa nguvu huku akijisifu, “Mimi ni nyati, shujaa, sishindwi kitu na sihitaji msaada. Siku zote shujaa husimama peke yake.”

Miezi mitatu baadaye, mazao aliyolima yakastawi vizuri sana. Alipanda juu ya mti mrefu na kutazama mazao kwenye shamba lake. Yalikuwa mengi na yamestawi vizuri sana. Alitabasamu huku akikuna kidevu kwa jeuri. Akanyoosha mkono na kusema, “Nilisema mimi sishindwi kitu, tazama mali ya shujaa. Nitakula nishibe miaka mingi kwa kadiri nitakavyo. Mungu anipe nini?”

Majuma mawili kabla hajaanza kuvuna, Doto alipatwa na homa kali. Akatafuna mizizi ili kujitibu, lakini homa haikumwacha. Alidhoofika akakosa nguvu. Mara akayaona makundi ya ndege, ngedere na nyani wakila na kuharibu mazao yake. Walikula kwa furaha kama wanafanya sherehe. Wali**kwanyua** mahindi na kung’oa mimea aina kwa aina. Wakairusha huku na huko. Doto alitamani ku**amia** lakini mwili wake ulikuwa **taabani**. Hakuweza hata kuinua mkono juu. Akabaki akiwatazama tu huku machozi yakim**churuzika**.

Aliikumbuka familia yake, akajisemea, “Sasa nimetambua umuhimu wa familia. Ningekuwa na familia yangu, haya yote yasingenitokea. Leo nimeamini maneno ya babu. Ama kweli umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.”

Siku mbili baadaye alipata nguvu kidogo aka**fungasha virago** na kurejea nyumbani kwa unyonge. **Mwondoko** alioondoka nao nyumbani sio aliorudi nao. Sasa alikuwa ameweka mikono yake nyuma. Safari hii hakutembea kwa makeke, bali alitembea kwa unyonge kutokana na afya yake kuwa dhaifu.

Alipokelewa na mdogo wake aliyekuwa akitoka shambani kuamia ndege na kulinda wanyama walao mazao. Walipokaribia nyumbani, alimuona dada yake akitoka porini kukusanya kuni za kupikia. Hapo nyumbani, alimkuta baba yake akiwa anamkamua ng’ombe maziwa, na mama yake akiwa anapika chakula jikoni. Binamu yake, ambaye alikuwa bustanini akimwagilia mboga, alipomwona, ali**piga mbio** akamkumbatia Doto kwa furaha.



Kiswahil STD 5 New.indd 94 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Watu wote nyumbani hapo walimpokea ndugu yao kwa furaha na **moyo mkunjufu**. Mara, Kulwa alifika. Alikuwa ametoka hospitalini kumpeleka babu kupata matibabu. Kulwa alifurahi kumuona ndugu yake. Alimkaribisha kwa kusema, “Karibu ndugu yangu.” Babu naye akamkaribisha kwa kusema, “Karibu mjukuu wangu. Hii ndiyo familia yako.” Doto alijibu, “Asante babu, nimeamini hakuna anayeweza kusimama peke yake. Familia ni muhimu sana; iwe kubwa ama ndogo.”

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kulwa na Doto walikuwa na tofauti gani za kitabia?
2. Kwa nini Doto aliamua kwenda kuishi porini peke yake?
3. Doto alipofika porini, alifanya shughuli gani?
4. Kwa nini Doto alishindwa kuamia ndege?
5. Doto alipougua, alikumbuka jambo gani?
6. Doto alipofika nyumbani, alipokelewa na nani?
7. Doto alipofika nyumbani, alikuta baba yake anafanya kazi gani?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 95 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Babu alimpokea Doto kwa kumwambia nini?
9. Familia ina umuhimu gani kwa binadamu?
10. Umejifunza nini kutokana na habari hii?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Eleza maana ya maneno yafuatayo:**

1. mwondoko
2. makeke
3. upenuni
4. madhubuti
5. kwanyua
6. amia
7. taabani
8. churuzika

## Zoezi la 3 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo:**

1. fungasha virago .......................
2. kaza roho .......................
3. moyo mkunjufu .......................
4. kata maini .......................
5. piga chenga .......................

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Andika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:**

(i) Bupe alirejea nyumbani akiwa ameweka mikono mbele.

(ii) Nenda nyumbani ukashirikiane na ndugu zako.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 96 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Mtoto anacheka chumbani.

(iv) Leo nimekumbuka kuandika insha niliyoambiwa na mwalimu.

(v) Simwiko na Kufakunoga wanapendana.

(vi) Hii ndiyo familia yako.

(vii) Doto aliondoka nyumbani kwa makeke.

(viii) Kaka alikubali tuhuma hizo.

**B. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopita.**

(i) Hadithi hiyo itatusaidia kujua umuhimu wa familia.

(ii) Kulwa amepokelewa vizuri na pacha wake.

(iii) Babu anayumbayumba kwa kudhoofu.

(iv) Nitakula na kushiba miaka mingi.

(v) Tutaandaa makazi yetu porini.

(vi) Wote tutapanda mlima hadi kileleni.

(vii) Wanafunzi watapanga madawati yao kwa ajili ya mtihani wa muhula.

**C. Andika sentensi zifuatazo katika wingi.**

(i) Mgonjwa amelala kitandani tangu jana.

(ii) Kikombe cha babu kimevunjika.

(iii) Jiwe limeporomoka kutoka mlimani.

(iv) Shati lake limechanika.

(v) Panya alijificha uvunguni mwa kitanda.

(vi) Simu ya mkononi ya mama imeibwa.

(vii) Ugonjwa huu umeenea katika kata zote.

(viii) Mwalimu anaandika ubaoni.

(ix) Hadithi hii ina funzo zuri.

(x) Huyu kijana ana adabu sana.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 97 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Kanusha sentensi zifuatazo:**

(i) Mjomba alikwenda kisimani kuchota maji.

(ii) Shangazi anafinyanga vyungu vizuri.

(iii) Binamu alichinja beberu mkubwa.

(iv) Baba mdogo amemnyoa nywele mdogo wangu.

(v) Bibi anasuka kikapu chenye rangi mbalimbali.

(vi) Dereva wa basi hili anaendesha taratibu.

(vii) Msua ni mfinyanzi mzuri wa vyungu.

(viii) Mtoto analilia chakula.

(ix) Wachuuzi wameongezeka sana.

(x) Shani amefaulu mitihani yake vizuri.

**E. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.**

(i) Mimi ninakwendaga shule kila siku.

(ii) Mwalimu Kagete analifundisha Shule ya Msingi Lumwani.

(iii) Chaku analioshapo banda la kuku.

(iv) Baba yake Sima huzilima mpunga na mahindi.

(v) Kazi huwasaidiana wanafamilia kuinua kipato.

(vi) Alitaka amkutage amefika stendi.

(vii) Baba yangu alikuja kesho.

(viii) Pendo amehamishiwaga Kiteto.

FOR ONLINE USE ONLY

**F. Andika KWELI au SI KWELI katika sentensi zifuatazo:**

(i) Shangazi ni mtoto wa mjomba. ___________

(ii) Binamu ni mtoto wa mjomba au shangazi. _________

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Mpwa ni mtoto wa mjomba. __________

(iv) Bibi ni dada yake mama. __________

(v) Shangazi ni dada yake baba. __________

(vi) Kitukuu ni mjukuu wa mtoto wako. __________

(vii) Wifi ni mke wa baba. __________

(viii) Mjomba ni kaka wa mama. __________

(ix) Mjukuu ni mtoto wa mwanangu. __________

(x) Babu ni kaka yake baba. __________

## G. Chagua neno sahihi kwenye kisanduku ili ukamilishe sentensi.

alitozwa, turubai, taji, radi, posta, kifani, dhahiri, pancha, kuwapongeza, tumeazimia, shada

(i) Tuliandaa sherehe ya _____ wanafunzi waliofaulu mitihani.

(ii) Mwaka huu _______ kupanua shamba letu la maharage.

(iii) Malkia alivaa _________ lililotengenezwa kwa dhahabu.

(iv) Nenda ________ ukatazame kama kuna barua zetu.

(v) Wakati wa mvua, _______ ilipiga na kuangusha miti.

(vi) Magunia ya mahindi yalifunikwa na __________ ili yasinyeshewe na mvua.

(vii) Dereva _______ faini kwa kuendesha gari kwa mwendokasi.

(viii) Aliziba _______ zote kwenye tairi la mbele.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Utungaji

**Andika insha fupi yenye maneno kati ya sabini na themanini (70 - 80) inayohusu umuhimu wa familia. Andika kwa kuzingatia vipengele vya insha na matumizi sahihi ya alama za uandishi. Vidokezo vifuatavyo vikuongoze.**

1. Jina lako ni nani?
2. Ni mtoto wa ngapi kuzaliwa?
3. Taja majina ya wazazi wako.
4. Eleza kazi unazofanya kila siku.
5. Eleza kazi wanazofanya wazazi au walezi wako.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 100 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Barua rasmi

*Katika sura hii, utajifunza jinsi ya kuandika barua rasmi. Utajifunza muundo wa barua rasmi. Pia, utaandika barua rasmi kwa kuzingatia mtiririko wa vipengele vya uandishi wa barua hiyo.*

**Fikiri**

1. Je, umewahi kuandika barua?
2. Ulimwandikia nani?
3. Barua hiyo ilikuwa inahusu nini?

**Ufahamu**

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

### Kabonza amuuguza mama yake

Kabonza anaishi na mama yake katika kijiji cha Kashule. Anasoma Shule ya Msingi Tumaini iliyopo Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara.

Wakati wa likizo, Kabonza alimsaidia mama yake kufanya shughuli mbalimbali. Alimsaidia kazi za shambani pamoja na za nyumbani. Muda wa likizo ulipokaribia kuisha, mama yake ali**ugua** na kulazwa hospitalini. Kwa kuwa hali yake ilikuwa mbaya, aliwekwa chini ya uangalizi maalumu wa daktari.

Daktari alishauri awepo mtu wa kukaa na mgonjwa. Kwa kuwa Kabonza na mama yake waliishi peke yao, Kabonza alimwambia daktari kuwa, yuko tayari kumwangalia mgonjwa. Kabonza alianza kumuuguza mama yake. Aliendelea kumuuguza mpaka mwisho wa likizo. Licha ya huduma nzuri aliyoipata, Mama Kabonza hakupata nafuu. Hivyo, Kabonza alitakiwa kuendelea kumuuguza. Kutokana na hali hiyo, aliamua kuomba ruhusa kwa Mwalimu Mkuu. Aliandika barua ifuatayo:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Kijiji cha Kashule,*
*S.L.P. 60,*
*Masasi,*
***Mtwara.***

*08/07/2018.*

*Mwalimu Mkuu,*
*Shule ya Msingi Tumaini,*
*S.L.P. 60,*
*Masasi,*
***Mtwara.***

*Ndugu,*

***YAH: OMBI LA RUHUSA YA KUMUUGUZA MAMA***

*Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.*

*Mimi ni mwanafunzi wa Darasa la Tano. Mama yangu anaumwa na amelazwa hospitalini. Hivyo ninaomba ruhusa ya kumuuguza kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 9 Julai mpaka tarehe 22 Julai, 2018.*

*Nitashukuru iwapo ombi langu litakubaliwa.*

*Ni mimi mtiifu,*

*K.Digo*
*Kabonza Digo*

FOR ONLINE USE ONLY

Baada ya kuandika barua, aliituma kwa Mwalimu Mkuu, ambaye aliipokea na kuisoma. Baada ya kuisoma barua hiyo, Mwalimu Mkuu aliwaeleza walimu wenzake yaliyom**sibu** mwanafunzi wao.

Kesho yake, walimu walikwenda kumuona mama yake Kabonza hospitalini. Mama alifurahi alipowaona walimu wa mwanaye wamekuja kumuona. Aliwashukuru sana.



Kiswahil STD 5 New.indd 102 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baada ya wiki mbili kupita, mama yake Kabonza alipata **nafuu**. Aliruhusiwa na kurudi nyumbani. Kabonza naye alipata **mwanya** wa kwenda shule. Alipofika shuleni, alipokelewa vizuri na walimu. Walimu walimsaidia sana katika masomo yaliyompita. Pia, walimu walimpongeza sana Kabonza kwa kuandika barua ya kuomba ruhusa kwa Mwalimu Mkuu.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kabonza ni mwanafunzi wa darasa la ngapi?
2. Shule ya Msingi Tumaini iko mkoa gani?
3. Kabonza anaishi na nani?
4. Kwa nini Kabonza alimwandikia Mwalimu Mkuu barua?
5. Kabonza aliandika barua kuhusu nini?
6. Kabonza aliomba ruhusa kuanzia tarehe ngapi hadi tarehe ngapi?
7. Walimu walikwenda hospitalini kumwona nani?
8. Kwa nini mama yake Kabonza alifurahi?
9. Kwa nini walimu walimpongeza Kabonza?
10. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. ugua
2. sibu
3. nafuu
4. mwanya

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Andika KWELI au SI KWELI.**

(i) Barua rasmi inatakiwa iwe na anwani nne. ________
(ii) Barua rasmi sharti iwe na salamu. ________
(iii) Siyo muhimu kuweka kichwa cha barua kwenye barua rasmi. ________
(iv) Barua uliyoisoma ina jina la mwandishi wa barua. ________
(v) Tarehe 22/07/2018 ni tarehe ya barua uliyoisoma. ________
(vi) Haitakiwi kuweka saini kwenye barua rasmi. ________

**B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

(i) ugua __________
(ii) tuma __________
(iii) ruhusu __________
(iv) nuka __________
(v) kasirika __________
(vi) gumu __________

**C. Panga vipengele vifuatavyo kwa kufuata muundo sahihi wa barua rasmi.**

(i) Doto Jumanne
(ii) Yah: Ombi la kushiriki mchezo wa kirafiki
(iii) Wako mtiifu,
(iv) 30/4/2018.
(v) Mwalimu Mkuu,
Shule ya Msingi Malugala,
S. L. P. 257,
Meatu.
(vi) Mimi ni mwanafunzi wa Darasa la Tano. Ninaomba kwenda kushiriki mchezo wa kirafiki katika Shule ya Msingi Malugala. Mchezo huo utafanyika tarehe 28/05/2018 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana, katika viwanja vya shule hiyo.
(vii) S.L.P. 257, Meatu.
(viii) Ndugu,
(ix) Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.
(x) D. Jumanne
(xi) Nitashukuru kama ombi langu litakubaliwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 104 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Tumia vipengele vilivyomo kwenye kisanduku kujaza muundo wa barua rasmi uliyopewa.**

anwani ya mwandikiwa, jina kamili la mwandishi, anwani ya mwandishi, saini ya mwandishi, tarehe ya kuandika barua, mwanzo wa barua, salamu ya awali, mwisho wa barua, kiini cha barua, kichwa cha barua, salamu ya mwisho

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

(vi)

(vii)

(viii)

(ix)

(x)

(xi)

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 4 Utungaji

**Andika barua rasmi kwa mwalimu wa darasa ukiomba msamaha kwa kosa la kufanya fujo darasani. Anwani yako iwe Shule ya Msingi Bombambili, S.L.P. 335, Songea.**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Igizo

*Katika sura hii, utasoma na kuigiza igizo. Pia, utaeleza wazo kuu na fundisho katika igizo hilo. Utajifunza matumizi ya nafsi na nyakati katika kauli halisi na kauli taarifa. Utaweza pia kuandika habari kwa kutumia nafsi na nyakati.*

**Fikiri**

1. Je, ulishawahi kuangalia igizo? Lilikuwa linahusu nini?
2. Wahusika walikuwa kina nani?
3. Je, wewe ulishawahi kushiriki katika igizo?

**Ufahamu**

*Soma igizo lifuatalo, kisha jibu maswali.*

### Maskini Tukutu

*Sauti ilisikika ikituarifu kuwa tayari* ***igizo*** *linaanza. Watu wote walikuwa kimya kabisa. Mara pazia lilifunguliwa. Wahusika wote wa igizo hilo walionekana jukwaani wakiwa wameganda kwa mitindo tofautitofauti. Watazamaji wakapiga kelele za shangwe kwa walichoona.*



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 106 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kiongozi:** Igizo letu linahusu mtoto **mtukutu** aitwaye Tukutu. Tukutu alikuwa hawasikilizi wazazi wake, walimu na hata wanafunzi wenzake. Nini kitatokea? Tusimalize utamu. Tujionee wenyewe.

**Waigizaji Wote:** Tunawakaribisha wote kujionea mambo mazuri tuliyoandaa. Karibuni sana. (*Wahusika wote wanajitambulisha uhusika wao na pazia linafungwa.*)

**Watazamaji:** (*Wote walipiga makofi, vigelegele na **mbinja**. Muda huohuo pazia linafunguliwa.*)

**Mama:** Tukutu! Tukutu! Amka uende shule.

**Tukutu:** Aaa! Mama! Mambo gani hayo? Mbona unaniharibia usingizi?

**Mama:** Mwanangu, mbona siku hizi umebadilika? Tabia yako imekuwa ya ajabu!

**Tukutu:** Mama, nitakwenda shuleni baadaye.

**Mama:** Wewe! Unasemaje! Haya, oga haraka, kunywa chai nenda shule. (*Tukutu anakubali. Anakwenda kuoga, anakunywa chai na kuondoka kwenda shuleni.*)

**Mwalimu:** Tukutu, kwa nini umechelewa?

**Tukutu:** Mwalimu nilikuwa naumwa tumbo.

**Mwalimu:** Haya, ingia darasani haraka; kisha andika maswali yaliyopo ubaoni. Ni ya somo nililowafundisha jana.

**Tukutu:** Mwalimu, mimi sina kalamu. Siwezi kuandika kwa sababu sioni ubaoni. (*Tukutu anatoa sababu nyingi.*)

**Mwalimu:** Haya kalamu hii hapa. Sasa ninataka ujibu maswali katika daftari lako. (*Mwalimu anaondoka. Tukutu anabaki akiwasumbua wenzake darasani.*)

**Tukutu:** Kisa, ninataka unijibie maswali yote. Usipofanya hivyo, nitakupiga.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kisa:** Jibu mwenyewe. Siwezi kukujibia. (*Tukutu anafanya fujo darasani; anawa**nyang'anya** madaftari ili anakili majibu ya wenzake. Wenzake wanakataa. Yeye anaanza kuwapiga.*)

**Masikitiko:** (*Masikitiko akielekea ofisi ya walimu kutoa taarifa kwa mwalimu.*) Mwalimu, Tukutu anatusumbua darasani. Anatupiga na kutunyang'anya madaftari.

**Mwalimu:** (*Mwalimu anaingia darasani.*) Tukutu njoo ofisini haraka. (*Tukutu anamfuata mwalimu.*) Tukutu una nini wewe? Kwa nini unawasumbua wenzako darasani? (*Mwalimu anamfokea Tukutu.*)

**Tukutu:** Mwalimu, mimi sitaki kusoma. (*Tukutu anarusha mikono.*)

**Mwalimu:** Nenda nyumbani kamwite mzazi wako. (*Tukutu anarudi nyumbani. Njiani anakutana na rafiki yake Kiduku.*)

**Kiduku:** Aaa! Tukutu unakwenda wapi? Twende huku ukatulize akili.

**Tukutu:** Sasa rafiki yangu Kiduku unataka twende wapi?

**Kiduku:** Twende nikupeleke sehemu moja ukafurahie ulimwengu. (*Tukutu anakubali na kumfuata Kiduku.*)

**Tukutu:** Sehemu hiyo ina nini cha kunifurahisha?

**Kiduku:** Wewe **fuata nyuki ule asali**; utafurahi tu. (*Wote wanacheka, haa! Haa! Haa! Wanafika uchochoroni sehemu iliyojificha ambayo Kiduku hukutania na vibaka wenzake.*)

**Tukutu:** Hapa umepajuaje? Mbona panatisha?

**Kiduku:** Sasa uko hatarini, kwa usalama wako toa ulicho nacho.

(*Kiduku anam**kwida** na kutaka kum**nyang'anya** begi la shule. Lakini, Tukutu analing'ang'ania begi lake. Kiduku anapatwa na hasira anampiga mateke na vichwa. Tukutu anaanguka chini. Kiduku anachukua begi, anatupa madaftari chini, na anaondoka nalo. Tukutu anabaki amelala pale chini. Wanafunzi wakiwa wanarudi nyumbani, njiani wanakutana na mbwa mkali; anawafukuza. Wanakimbia



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 5 New.indd 108 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*pande tofautitofauti. Mmoja wao, ambaye ni Shauri, anajikuta kwenye kichochoro ambako Tukutu ameachwa.)*

**Shauri:** (*Anashtuka na kuanza kuita.*) Tukutu! Tukutu! Umefanya nini? Amka! (*Aliita kwa sauti.*)

**Tukutu:** (*Akiinuka.*) Loo! Kiduku amenipiga na kuninyang'anya begi. Ama kweli **usilolijua ni kama usiku wa giza**!

**Shauri:** Twende upesi nikupeleke nyumbani. Hapa si mahali salama kabisa. (*Wanaondoka wote kwenda nyumbani huku Tukutu akichechemea na uso wote ukiwa umevimba.*)

**Shauri:** Rafiki yangu Tukutu, umekuwa m**kaidi** sana. Humsikilizi mama yako, walimu na hata wanafunzi wenzako. Tabia yako hii italeta madhara katika masomo yako na maisha yako kwa ujumla. Kuanzia sasa, anza kusoma kwa bidii kama mimi. Watu watakupenda.

**Tukutu:** Asante sana kwa ushauri wako. Nitawaomba msamaha mama, walimu, Kisa na wanafunzi wote niliowakosea. Ama kweli **akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli**. (*Pazia linafungwa na watu wanapiga makofi na vigelegele.*)

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Igizo hili linahusu nini?
2. Tukutu alikuwa na tabia gani?
3. Tukutu alinyang'anywa nini na Kiduku?
4. Nani aliyemkuta Tukutu kichochoroni?
5. Kama wewe ungekutana na Kiduku, ungemwambia nini?
6. Wahusika gani majina yao yanaendana na matendo yao? Kwa nini?
7. Katika igizo hili, ungependa kuwa kama nani? Kwa nini?
8. Igizo hili linatufundisha nini?

## Zoezi la 2 Kazi ya kufanya

**Igiza na wenzako igizo ulilolisoma.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kila neno.**

1. igizo
2. mtukutu
3. mbinja
4. nyang'anya
5. kwida
6. kaidi

## Zoezi la 4 Methali

**Andika maana za methali zifuatazo:**

1. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.
2. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
3. Kawaida ni kama sheria.
4. Fuata nyuki ule asali.
5. Usiandikie mate, na wino ungalipo.

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yafuatayo:**

(i) kelele ____________

(ii) ondoka ____________

(iii) mbinja ____________

(iv) mtukutu ____________

(v) lukuki ____________

(vi) nyang'anya ____________

(vii) kwida ____________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika wingi wa sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Chura anafurahia maji bwawani.
*Vyura wanafurahia maji bwawani.*

(i) Mwanafunzi hodari alifaulu vizuri masomo yake.

(ii) Mimi nilikwenda kumwona simba katika mbunga ya wanyama ya Manyara.

(iii) Ulimpokea mgeni wako kwa shangwe.

(iv) Sikuamini kama timu yetu ingefungwa magoli mengi.

(v) Wewe unajivunia nini?

**C. Tunga sentensi kumi na tano (15) kutokana na jedwali lifuatalo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wiki ijayo | tulicheza mpira wa miguu | kwa | bibi |
| Kila siku | tutakwenda likizo | kabla ya | kuingia darasani |
| Jana | tunaimba wimbo wa Taifa | ya | Pugu |
| Leo | tutatembelea stesheni ya reli ya kati | | uwanjani |
| Kesho | | | |
| Mwaka jana | | | |

**D. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika kauli taarifa.**

**Mfano:** "Simulia hadithi," Baraka aliniambia.
*Baraka aliniambia kuwa nisimulie hadithi*.

(i) "Fungeni chandarua ili msipatwe na Malaria," Bwana Afya alisema.

(ii) Mwalimu alisema, "Wanafunzi ni lazima mfuate ratiba ya shule."

(iii) Dada alituambia, "Kuleni chakula bora ili muwe na afya njema."

(iv) "Nimechoka," babu alilalamika.

(v) "Je, umemuona Halima?" Kiroboto aliuliza.

(vi) "Kumbe hamuogopi upupu!" Mwalimu alishangaa.

(vii) "Kila mmoja awepo kwenye mkutano," kiongozi alisema.

(viii) "Yamenikuta," Juma alikiri.



Kiswahil STD 5 New.indd 111 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Jaza fumbo lifuatalo kwa kutumia maelekezo ya kwenda chini na kwenda kulia.**




**Kwenda chini**

1. Kifaa kinachotumika kulalia (7)
2. Kifaa kinachotumika kuandikia (6)
4. Sehemu inayotumika kuhifadhia vitabu na kujisomea (7)

**Kwenda kulia**

2. Kazi ya maandishi iliyochapwa yenye kurasa na kugundishwa pamoja na kuwekewa jalada (6)
3. Silabi zinazolingana kati na mwishoni mwa mstari wa shairi (4)
5. Chumba au mahali wanaposomea wanafunzi (6)
6. Kipande cha mti kilichochongwa mfano wa kijiko kinachotumika kupikia chakula (5)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Chagua jibu lililo sahihi kisha, uiandike herufi yake katika kisanduku.**

(i) Mapunda alisafiri siku nzima kutoka Songea kwenda Arusha. Silabi iliyopigiwa mstari inawakilisha nini?

(a) wakati
(b) nafsi
(c) hali
(d) awali

(ii) "Hakika leo mtakiona cha mtema kuni." Kaka alituambia. Sentensi hii iko katika kauli gani?

(a) taarifa
(b) halisi
(c) amri
(d) kawaida

(iii) Kaka alituambia kwamba hakika tutakiona cha mtema kuni. Sentensi hii iko katika kauli gani?

(a) taarifa
(b) halisi
(c) amri
(d) kawaida

(iv) Tausi ataingia kwenye mashindano ya kuogelea. Sentensi hii iko katika wakati gani?

(a) uliopita
(b) uliopo
(c) ujao
(d) hali timilifu

(v) Walimu wanafundisha masomo yetu kwa bidii. Mwaka jana walimu walifanya nini?

(a) Walimu watafundisha masomo yetu kwa bidii.
(b) Walimu walifundisha masomo yetu kwa bidii.
(c) Walimu wanafundisha masomo yetu kwa bidii.
(d) Walimu wamefundisha masomo yetu kwa bidii.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**G. Unda maneno mapya yanayoanza na maneno yafuatayo:**

**Mfano:** mbwa *mbwamwitu*

(i) askari ____________

(ii) bata ____________

(iii) gari ____________

(iv) mwendo ____________

(v) zima ____________

(vi) pima ____________

(vii) pembe ____________

(viii) mali ____________

(ix) kanda ____________

**H. Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopo au ujao.**

| Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|
| (i) ........................ | Wanafunzi watatuimbia nyimbo nzuri. |
| (ii) Ng'ombe wetu wanatoa maziwa mengi. | ............................................... |
| (iii) ........................ | Utakula chakula kingali moto. |
| (iv) Mtoto anamlilia mama yake. | ............................................... |
| (v) ........................ | Siku nzima nitasafiri kuelekea kwa babu. |
| (vi) Leo tunakula wali na maharage. | ............................................... |
| (vii) ........................ | Mdogo wangu atang'oa jino la pili. |

## Zoezi la 6 Utungaji

**Malizia hadithi ifuatayo kwa maneno kati ya sitini na themanini (60 - 80).**

Miale ya jua ilinikurupusha kitandani. Nilizoea kuamshwa na sauti ya kuvutia ya ndege wangu aitwaye Tose. Nilikimbia kuangalia katika kiota chake. Sikumkuta Tose na kiota kilikuwa wazi. Nili…



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 5 New.indd 114 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tano

## Shairi

*Darasa la Nne, ulisoma mashairi na kujibu maswali kuhusu mashairi hayo. Katika sura hii, utasoma shairi la **Yai au kuku**. Utaweza kuonesha na kueleza vina, mizani, beti, vituo, na mawazo makuu kwenye shairi hilo.*

### Fikiri

1. Umewahi kuimba shairi?
2. Shairi hilo lilihusu nini?
3. Ulilimba wapi?

**Ufahamu**

*Soma na ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.*

### Yai au kuku

1. *Inashangaza dunia, kwa hiki kitendawili,*
*Yupi mwanzo kutokea, kuku yai ndilo swali,*
*Sote yai twalijua, suraye na yake hali,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha **jadi**?*

2. *Kuku fundi ku**pekua**, ardhi na jalalani,*
*Je, ndiye katangulia, kuja hapa duniani?*
*Huenda li**ibukia**, akiwa **tembe** yakini,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 115 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**3.** *Kuku, Yai wanazoza, kila mmoja asema,*
*Ni wa mwanzo kutokeza, Yai asema ni mama,*
*Nuru yake yapendeza, tena mleta uzima,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

**4.** *"Bila mimi hupo Kuku, ni mimi nimekuzaa,*
*Kuku huwezi ni**piku**, hata kama 'me**komaa**,*
*Tangu zama za masiku, duniani nimekaa,"*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

**5.** *Kuku naye akasema, "E' Yai acha mikogo,*
*Umepatapi uzima? Punguza yako ma**zogo**,*
*Mimi ndiye wako mama, tangu ukiwa mdogo,"*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

**6.** *"Kweli Yai umekwama, kwa fikira za dharau,*
*Akilizo zimehama, umejijaza sahau,*
*Nakukumbusha heshima, wazazi usidharau,"*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

**7.** *Yai, Kuku kwa maringo, wajidai hadharani,*
*Nani katika **miongo**, aliwahi duniani?*
*Nauliza wenye **bongo**, mliomo darasani,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

**8.** ***Chapuchapu** lete jibu, nazo sababu nipeni,*
*Tuimalize **sulubu**, nyoyo ziwe na amani,*
*Tuwaondolee tabu, Yai, Kuku **mzozo**ni,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

9. *Ikiwa ni huyu Kuku, tueleze chanzo chake,*
*Ikawaje aje huku, mpekua kwa mateke,*
*Kama wa mwanzo ni Kuku, tuikiri **rai** yake,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

10. *La, kama Yai kawahi, ni wapi alitokea?*
*Mpime nawanasihi, kwa haki kesi amua,*
*Amua kwa usahihi, bila ya kuwaonea,*
*Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?*

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Shairi hili linahusu nini?
2. Katika ubeti wa tatu, Kuku na Yai wanabishania nini?
3. Yai anasema nini katika ubeti wa nne?
4. Je, Yai anaongea kwa adabu na kuku?
5. Kuku alifurahi kusikia maneno ya Yai?
6. Kuku anasema nini katika ubeti wa tano?
7. Kuku anaposema “Nakukumbusha heshima, wazazi usidharau” ana maana gani?
8. Katika ubeti wa tisa, mshairi anaposema Kuku ni “mpekua kwa mateke” ana maana gani?
9. Katika ubeti wa kumi, mshairi anawaambia nini walio darasani?
10. Unadhani “kitendawili” katika shairi kitateguliwa? Toa sababu ya jibu lako.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 117 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. pekua
2. ibukia
3. tembe
4. piku
5. zogo
6. bongo
7. chapuchapu
8. mzozo
9. jadi
10. sulubu
11. rai
12. komaa
13. miongo

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 3 Methali

**Malizia methali zifuatazo:**

1. Kuku havunji, .....................
2. Teke la kuku, ......................
3. Kuku mgeni, .......................
4. Mwana wa kuku, ................
5. Uchungu wa mwana, .........

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Chagua jibu sahihi kwa kuandika herufi katika kisanduku.**

(i) Idadi ya silabi katika mstari mmoja wa shairi unaitwa_____.

(a) mshororo

(b) vina

(c) urari

(d) mizani

(ii) Kila mshororo katika shairi hili una mizani ngapi?

(a) minne

(b) nane

(c) kumi na sita

(d) kumi

(iii) Vina vya katikati na mwishoni katika ubeti wa tano ni_____.

(a) **ma** na **go**

(b) **go** na **e**

(c) **go** na **di**

(d) **go** na **ku**

(iv) Kina cha katikati katika ubeti wa kwanza ni kipi?

(a) **a**

(b) **a** na **e**

(c) **a** na **di**

(d) **li**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 119 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Katika shairi mshororo ni nini?

(a) aya ya shairi

(b) mstari wa mwisho katika ubeti wa shairi

(c) mstari mmojawapo kwenye kila ubeti

(d) idadi ya mistari yote katika shairi

(vi) Shairi hili lina beti ngapi?

(a) nne

(b) kumi na sita

(c) kumi

(d) sita

(vii) Kituo katika shairi hili ni:

(a) Tuimalize sulubu, nyoyo ziwe na amani,

(b) Amua kwa usahihi, bila ya kuwaonea,

(c) Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

(d) Nani katika miongo, aliwahi duniani?

(viii) Ni beti zipi katika shairi la “Yai au kuku” zinafanana vina vyake vya kati?

(a) 6 na 7

(b) 4 na 5

(c) 3 na 4

(d) 5 na 6

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika kirefu cha maneno haya yaliyotumika katika shairi.**

(i) suraye ______________
(ii) liibukia ______________
(iii) umepatapi ______________
(iv) akilizo ______________

**C. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

| | Neno | Kinyume |
|---|---|---|
| (i) | swali | _______ |
| (ii) | nuru | _______ |
| (iii) | mwanzo | _______ |
| (iv) | punguza | _______ |
| (v) | uhai | _______ |
| (vi) | kwama | _______ |
| (vii) | sahau | _______ |
| (viii) | dharau | _______ |
| (ix) | tega | _______ |
| (x) | nyingi | _______ |

**D. Andika neno lenye maana sawa na maneno yafuatayo:**

**Mfano:** maringo – *madaha*

(i) piku
(ii) dharau
(iii) pendeza
(iv) tangulia
(v) uzima
(vi) shindwa
(vii) idhini
(viii) kauli

## Zoezi la 5 Utungaji

**Tunga beti mbili za shairi kuhusu "Kifaranga na kuku."**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 121 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Sita

## Kuipenda nchi

*Katika sura hii, utaimba* ***Wimbo wa kuisifu nchi yetu****, kisha utasoma na kughani shairi la* ***Naipenda nchi yangu****. Utajifunza mambo mbalimbali kuhusu nchi yetu. Pia, utaweza kuonesha na kueleza vina, mizani, beti, vituo, na mawazo makuu katika shairi.*

### Fikiri

#### Wimbo wa kusifu nchi yetu

**1.** *Tazama ramani utaona nchi nzuri,*
*Yenye mito na mabonde mengi ya nafaka,*
*Nasema kwa kinywa halafu kwa kufikiri,*
*Nchi hiyo mashuhuri huitwa Tanzania.*

Kibwagizo: *Majira yetu haya,*
*Yangekuwaje sasa,*
*Utumwa wa nchi Nyerere ameukomesha.*

**2.** *Chemchemi ya furaha amani nipe tumaini,*
*Kila mara kwako niwe nikiburudika,*
*Nakupenda sana hata nitakusitiri,*
*Nitalalamika kukuacha Tanzania.*

Kibwagizo: *Majira yetu haya,*
*Yangekuwaje sasa,*
*Utumwa wa nchi Karume ameukomesha.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 122 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**3.** *Nchi yenye Azimio lenye tumaini,*
*Ndiwe peke yako mwanga wa Watanzania,*
*Ninakuthamini hadharani na moyoni,*
*Unilinde nami nikulinde hata kufa.*
Kibwagizo: *Majira yetu haya,*
*Yangekuwaje sasa,*
*Utumwa wa nchi TANU imeukomesha.*

(a) Nchi nzuri inayotajwa katika wimbo huu ni nchi gani?
(b) Ni uzuri upi uliotajwa katika wimbo huu?
(c) Nani alikomesha utumwa katika kibwagizo cha ubeti wa kwanza?
(d) Je, mwandishi anafurahia kuishi katika nchi yake?
(e) Mwandishi anaahidi nini kwa nchi yake?

**Ufahamu**

*Soma na ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.*

## Naipenda nchi yangu

**1.** *Naipenda nchi yangu, yenye wingi wa* ***neema****,*
*Ni bora* ***maumbile****ye, popote ukitazama,*
***Miinuko*** *na ma****bonde****,* ***tambarare*** *na milima,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**2.** *Ina maziwa makubwa, Nyasa pia Tanganyika,*
*Na ziwa kubwa kabisa, ni Nyanza lafahamika,*
*Pia maziwa madogo, ni mengi kuhesabika,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*




**3.** *Yenye mlima mrefu, Afrika watajika,*
*Waitwa Kilimanjaro, duniani wasifika,*
*Watu wengi huupanda, **kilele**ni wakafika,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 124 7/23/21 3:15 PM

4. *Mito mikubwa midogo, ni mingi kuhesabika,*

*Mingi yao maziwani, baharini humwagika,*

*Na* ***vijito*** *kiangazi, kifikapo hukauka,*

*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*



5. *Ina mbuga za wanyama, na misitu ya hifadhi,*

*Urithi wa kupendeza, nchi yangu ya u**hodhi**,*

*Kuyaona haya yote, ninataka kwa* ***ghaidhi****,*

*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*





FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**6.** *Utajiri ardhini, ni mwingi kupindukia,*
*Lo! madini **tumbitumbi**, ardhini kuzamia,*
*Tanzanaiti dhahabu**,** almasi rubi pia,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*



**7.** *Ni nchi ya utamaduni, murua unaokua,*
*Wa sasa na wa zamani, haki unazingatia,*
***Wigo** ni mpana sana, kwa aina za **sanaa**,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**8.** *Ni nchi ya Kiswahili, lugha yetu asilia,*
*Lugha yetu ya taifa, na pia ya Jumuia,*
*Na Umoja wa Afrika, lugha hii hutumia,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*




**9.** *Ni nchi ilo**nuia**, kupiga nyingi hatua,*
*Kukuza kilimo chetu, tuwe na **hadhi murua,***
*Sayansi tukazanie, uchumi tutainua,*
*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*




FOR ONLINE USE ONLY

**10.** *Wasifu wa nchi yangu, sasa ninamalizia,*

*Sifa hizi zimetosha, ni nyingi kwa wasojua,*

*Kesho nitaziongeza, kisha nitawaghania,*

*Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.*



## Zoezi la 1 Ufahamu

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Shairi hili linahusu nini?
2. Ziwa Nyanza lililotajwa kwenye ubeti wa pili linafahamika pia kwa jina gani?
3. Taja mito miwili ya Tanzania unayoifahamu.
4. Mlima Kilimanjaro una sifa gani barani Afrika?
5. Mshairi anasema utamaduni wa Tanzania unazingatia nini?
6. Lugha ya Kiswahili inazungumzwa wapi?
7. Taja aina nne za madini ambayo mshairi ameyasifia kwenye shairi lake.
8. Taja mbuga tatu za wanyama unazozifahamu hapa nchini.
9. Mshairi anasema nchi yake imenuia kufanya nini?
10. Umejifunza nini kutokana na shairi ulilolisoma?



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. neema
2. maumbile
3. miinuko
4. tambarare
5. kilele
6. hodhi
7. ghaidhi
8. tumbitumbi
9. bonde
10. hadhi
11. murua
12. wigo
13. sanaa
14. vijito
15. nuia

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) kijito | (a) tanzanaiti, dhahabu, almasi, rubi |
| (ii) Nyasa, Tanganyika na Nyanza | (b) sifa |
| (iii) madini | (c) mito mikubwa zaidi |
| (iv) sanaa | (d) maziwa makubwa Tanzania |
| (v) wasifu | (e) vinyago, ngoma, nyimbo |
| (vi) wigo | (f) mto mdogo unaotiririsha maji |
| (vii) kiangazi | (g) lugha yetu ya taifa |
| (viii) Kiswahili | (h) msimu wa jua linapokuwa kali |
| | (i) mpaka |
| | (j) lugha yetu ya kigeni |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.**

**Mfano:** Mshairi aliandika shairi la kusisimua.

*Mshairi ataandika shairi la kusisimua.*

(i) Niliamka asubuhi na kuisifu nchi yangu.

(ii) Niliongeza sifa, kisha nikawaghania.

(iii) Wanafunzi wanafanya ziara kwenda kutazama ziwa Tanganyika.

(iv) Mito hupeleka maji baharini na kwenye maziwa.

(v) Vijito hukauka wakati wa kiangazi.

(vi) Umoja wa Afrika hutumia lugha ya Kiswahili.

(vii) Nchi yetu inakuza kilimo ili kuwa na hadhi murua.

(viii) Tulitangaza utajiri wa nchi yetu ya Tanzania.

## Zoezi la 4 Utungaji

**Tunga beti mbili za shairi kuhusu darasa lako.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Saba

## Utenzi

*Katika sura hii, utasoma na kughani utenzi unaohusu usafi. Utajifunza kuhusu vina, mizani na vituo vya beti. Pia, utaeleza mawazo makuu na ujumbe katika utenzi.*

**Fikiri**

1. Ulishawahi kusoma utenzi wowote?
2. Utenzi huo ulikuwa na ujumbe gani?
3. Unaelewa nini kuhusu vina na mizani?

**Ufahamu**

*Soma na ghani utenzi ufuatao, kisha jibu maswali.*

### Usafi

1. *Leo nashika kalamu,*
   *Kusema jambo muhimu,*
   *La kukazia nidhamu,*
   *Usafi ku**zingatia**.*

2. *Wameshafunza walimu,*
   *Usafi mada muhimu,*
   *Bali hili somo gumu,*
   *Nami nitaongezea.*

3. *Usafi huwa ni **kinga**,*
   *Ya maradhi yano**zonga**,*
   *Ni waganga wame**longa**,*
   *Walimu wamekazia.*

4. ***KWANZA, usafi wa kinywa,***
   *Ni muhimu kuambiwa,*
   *Hukinga mengi magonjwa,*
   ***Rihi** mbaya kuzuia.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 131 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**5.** *Ukiamka 'subuhi,*
*Kupiga mswaki wahi,*
*Kabla ya **staftahi**,*
*Meno kwa dawa sugua.*

**6.** *Unapopiga mswaki,*
*Safisha yote mabaki,*
*Ya chakula yalo**saki**,*
*Menoni yakagandia.*

**7.** *Yasafishe meno sawa,*
*Uchafu wote suguwa,*
*Kwao mswaki na dawa,*
*Meno ya nyuma anzia.*

**8.** *Pia ulimi sugua,*
*Kisha kinywa **sukutua**,*
*Watu watakukimbia,*
*Kama harufu watoa.*

**9.** ***PILI, usafi mwilini,***
*Oga tumia sabuni,*
*Dodoki liku**auni**,*
*Mwilio kusugulia.*

**10.** *Uchafu haupendezi,*
*Oga ondoa **kutuzi**,*
*Sehemu zote za ngozi,*
*Na za siri zingatia.*

**11.** *Mwili ukiwa **nadhifu**,*
*Viungo huwa **kunjufu**,*
*Nawe huwa furahifu,*
*Usafi kufurahia.*

**12.** ***TATU, usafi wa nguo**,*
*Ni muhimu kwa afyayo,*
*Sabuni ndo kifulio,*
*Nguozo kuzifulia.*

**13.** *Nguo safi kivutio,*
*Nguo chafu kichefuo,*
*Usafi **kila uchao,***
*Ni ada ya kuania**.***

**14.** *Kijana utapendeza,*
*Usafi ukitimiza,*
*Lakini utachukiza,*
*Nguo chafu ukivaa.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**15.** ***NNE, usafi shuleni,***
*Darasani na vyooni,*
*Mazingira ya shuleni,*
*Yawe nadhifu sikia.*

**16.** *Fyeka nyasi viwanjani,*
*Fagia taka njiani,*
*Pawe safi vivulini,*
*Nawe utafurahia.*

**17.** *Bustani za maua,*
*Vema kuzipangilia,*
*Pia kuzimwagilia,*
*Mimea itachanua.*

**18.** ***TANO, usafi nyumbani,***
*Wazazi wape auni,*
*Bafu, jiko na chooni,*
*Usafi iwe tabia.*

**19.** *Kiwe safi chumba chako,*
*Ufue mashuka yako,*
*Tandika kitanda chako,*
*Unadhifu zingatia.*

**20.** *Usafi kuzingatia,*
*Ni nidhamu ya murua,*
*Wazazi kusaidia,*
*Ni ya kuiga tabia.*

**21.** *Mengi nimezungumza,*
*Bali mengi nimesaza,*
*Usafi nimehimiza,*
*Muhimu kuzingatia.*

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Jambo muhimu linalozungumziwa katika utenzi huu ni nini?
2. Ukiamka asubuhi unafanya nini kwanza?
3. Usipofanya usafi wa kinywa nini kitatokea?
4. Mwandishi anasema kabla ya kula chochote unapaswa kufanya nini?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Utenzi huu unasema nguo chafu zina sifa gani?
6. Je, usafi unafanyikaje shuleni?
7. Unapaswa kufanya nini kuhusu chumba chako?
8. Unadhifu ni nini?
9. Bustani za maua zisipomwagiliwa nini kitatokea?
10. Je, mshairi amesema mambo yote yanayohusu usafi?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. zingatia
2. kinga
3. zonga
4. longa
5. rihi
6. staftahi
7. saki
8. sukutua
9. auni
10. kutuzi
11. nadhifu
12. kunjufu

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 3 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Macho …………………
2. Meno ya mbwa …………………
3. Ulimi unauma …………………..

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Mwenye mdomo ..................
5. Ulimi ............................
6. ............ faraja.
7. ............ si chururu.
8. ............, utajenga ukuta.
9. ............, mauti nyuma.
10. ............ halina ubani.

## Zoezi la 4 Nahau

**Tumia vifungu vya maneno vilivyopo kwenye kisanduku kutoa maana ya nahau zifuatazo:**

> kujitia matatani, fuata mawazo ya wakati uliopo,
> kaa kimya, kuwa kigeugeu, kuwa na wasiwasi

1. kuwa popo ............
2. fuata upepo ............
3. kuwa tumbo moto ............
4. fyata mkia ............
5. kujipalia mkaa ............

## Zoezi la 5 Vitendawili

**Tegua vitendawili vifuatavyo:**

1. Mgeni kachungulia dirishani ................
2. Popoo mbili zavuka mto .............
3. Kwetu sisi sote ni weusi .....................
4. Nyumba yangu ndogo imejaa askari tele ................
5. Hakika sirudi tena kwa mjomba ........................

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

**A. Kamilisha sentensi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku.**

tasa, hasha, njuga, mvuke, naam au abee, kwaheri, maziwa, anarina, ukiwa, sonara, mwanafunzi, mchafu

(i) Mtu anayesoma shule anaitwa ___________.

(ii) Mtu akifiwa anakuwa na ___________.

(iii) Mwenye mzinga alikuwa __________asali.

(iv) Huyu ng'ombe hazai, hivyo ni ___________.

(v) Ukiitwa itikia kwa kusema ___________.

(vi) Mtu ambaye si msafi ni ___________.

(vii) Huyu ng'ombe anakamuliwa ________.

(viii) Wanapocheza ngoma wanavaa _________miguuni.

(ix) Ukiondoka aga kwa kusema _________.

(x) ______ anatengeneza pete, mikufu na hereni za dhahabu.

**B. Andika umoja au wingi wa maneno yafuatayo:**

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| (i) | mwili | _______ |
| (ii) | ugonjwa | _______ |
| (iii) | _______ | vinywa |
| (iv) | mswaki | _______ |
| (v) | _______ | meno |
| (vi) | ulimi | _______ |
| (vii) | ngozi | _______ |
| (viii) | _______ | madarasa |
| (ix) | _______ | bustani |
| (x) | mazingira | _______ |

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 7 Utungaji

**Tunga beti mbili za utenzi kuhusu "Usafi wa nyumba."**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nane

## Kupata taarifa muhimu

*Katika sura hii, utasoma na kueleza taarifa muhimu katika matangazo, ratiba na vifungu vya habari. Pia, utasoma na kutaja mawazo makuu katika vifungu vya habari na kufanya ufupisho.*

**Fikiri**

1. Je,umewahi kuona tangazo?
2. Uliliona tangazo hilo wapi?
3. Tangazo hilo lilikuwa linahusu nini?

**Ufahamu**

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

### Nia na mdogo wake

Nia ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ushindi katika Wilaya ya Bora, mkoani Sanya. Baba yake Nia anaitwa Bwana Fukama na mama yake anaitwa Bibi Sokota. Nia ana mdogo wake aitwaye Bute. Nia na mdogo wake wanaishi katika kijiji cha Kibeta, kilometa tatu kutoka Shule ya Msingi Ushindi. Nia anasoma Darasa la Tano lakini Bute anasoma Darasa la Kwanza. Siku za shule, Nia humuamsha mdogo wake mapema ili ajiandae na kunywa chai kabla ya kwenda shuleni.

Siku moja Nia alichelewa sana kuamka. Alipoamka, alimuamsha mdogo wake kisha wakajiandaa harakaharaka ili waweze kuwahi kwenda shuleni. Baada ya kunywa chai, waliwaaga wazazi wao. Walianza safari yao ya kwenda shuleni. Wakiwa njiani, Nia alitangulia mbele na Bute alimfuata nyuma. Nia alitembea harakaharaka huku akimu**himiza** Bute kuongeza mwendo. Kadiri muda ulivyozidi kusogea, Nia aliongeza mwendo bila kugeuka nyuma.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 137 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nia na Bute walifika kwenye daraja la Kitunda. Walipofika hapo, Bute alivutiwa na vipepeo wa rangi mbalimbali. Vipepeo hao waliruka huku na huko wakifurahia maua yaliyokuwa yamezunguka daraja la Kitunda. Baada ya kuvuka daraja, Bute alisimama na kuwatazama vipepeo hao akitamani kumkamata mmojawapo. Huku Bute akiwa amesimama, Nia aliendelea na safari bila kujua kwamba, mdogo wake alikuwa akishangaa vipepeo.



Bute alianza kuwafuata vipepeo. Vipepeo waliruka wawezavyo, kukwepa kukamatwa. Bute aliendelea kuwakimbiza. Bila kujua alijikuta katikati ya msitu mnene. Hakuweza kutambua alikotokea. Alisimama na kuanza kumwita dada yake pasipo mafanikio. Alijaribu kutafuta njia ya kurudi darajani bila mafanikio. Baada ya kutembea kwa muda mrefu, alichoka sana. Aliamua kupumzika chini ya mti na kuanza kulia. Baada ya muda, alipitiwa na usingizi; aka**lala fofofo**.

Nia, bila kujua, aliendelea na safari ya kuelekea shuleni. Alipokaribia, aligeuka nyuma kumtazama mdogo wake lakini hakumuona. Alishituka akaanza kurudi nyuma huku akiita kwa sauti, "Bute! Bute! Buteeee...!" Nia aliendelea kuita kwa sauti huku akikimbia kurudi darajani. Njiani alikutana na watoto wawili. Akawauliza, "Mmemuona mwanafunzi wa kiume mwenye begi lenye rangi nyeusi?" Watoto walijibu, "Hapana dada." Nia aliendelea na safari ya kurudi nyumbani akidhani kwamba angemkuta mdogo wake.



Kiswahil STD 5 New.indd 138 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Alipofika nyumbani, aliwakuta wazazi wake wakijiandaa kwenda shambani. Nia alikuwa ame**lowa** jasho mwili mzima. Alikuwa aki**hema** na alionekana amechoka sana. Wazazi wake wali**shituka** na kumkimbilia. Walimuuliza, "Vipi mbona umerudi mapema?" Nia alijibu, "Bute amepotea." Wazazi wake walipatwa na **hofu** na wasiwasi. Kila mmoja alishika njia yake kumtafuta Bute.

Nia alipoanza kuondoka, **ghafla** alikumbuka kuwa mwalimu wake wa Kiswahili aliwafundisha kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa. Alikumbuka kuwa mwalimu aliwafundisha namna ya kuandika tangazo. Alirudi na kuingia chumbani kwake, kisha akachukua kalamu na karatasi kwenye begi lake. Aliandika hivi:

TANGAZO MUHIMU

BUTE FUKAMA AMEPOTEA

Bute ni mtoto mwenye umri wa miaka saba. Ni mwanafunzi wa Darasa la Kwanza katika Shule ya Msingi Ushindi, iliyoko Wilaya ya Bora, mkoani Sanya. Bute amepotea tarehe **22/04/2018** saa **1:15** asubuhi. Mara ya mwisho alionekana katika daraja la Kitunda akiwa amevaa sare ya shule yenye rangi ya bluu na nyeupe na begi la rangi nyeusi mgongoni. Kwa yeyote atakayemuona apige simu **2550123/2550321** au atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baada ya kuandaa tangazo, alikumbuka kuwa alihitaji kuwa na **nakala** nyingi. Aliandika nakala kumi. Alipokamilisha kazi yake, alifungua mlango na kuelekea nje. Ali**piga mbio** kuelekea vijiji vya jirani. Alisambaza matangazo yake kwa umakini. Baadhi aliyaweka kwenye kuta za majengo na mengine kwenye miti iliyokuwa karibu na njia.

Baada ya kazi yake kukamilika, alianza safari ya kuelekea shuleni. Alipofika shuleni, aliwaeleza walimu kilichotokea. Walimu walimpa pole na kumtia moyo kwamba mdogo wake atapatikana. Walisisitiza kwamba kama hatapatikana, saa tisa mchana walimu wangetawanyika kwenda kumtafuta. Nia aliingia darasani.

Ilipofika saa nane, Nia alikwenda kwa mwalimu kumuuliza kama amepata taarifa zozote kuhusu mdogo wake. Alipofika ofisini, alishangaa kumuona Bute ameketi ofisini. Alimkuta mwalimu akizungumza na kijana mmoja aliyetambulishwa kwa jina la Bahati. Bahati alisema, “Nimemkuta mtoto amelala chini ya mti wakati ninakata kuni. Niliondoka naye kuelekea nyumbani. Nikiwa njiani, niliona tangazo lililotaja jina la shule hii. Niliamua kumleta hapa shuleni.” Nia alifurahi sana kumpata mdogo wake. Walimu walifurahi pia. Walim**pongeza** Nia kwa kutumia vyema maarifa aliyoyapata darasani.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Nia na Bute waliishi katika kijiji gani?
2. Bute alikuwa mwanafunzi wa darasa la ngapi?
3. Bute alipofika daraja la Kitunda alivutiwa na nini?
4. Nia alipokuwa akirudi nyumbani alikutana na nani?
5. Nia alikumbuka mwalimu wake wa Kiswahili alimfundisha kuhusu nini?
6. Nia alifanya nini ili mdogo wake aweze kupatikana?
7. Nani alimleta Bute shuleni?
8. Vitu gani vilimtambulisha Bute kwenye tangazo?
9. Eleza taarifa muhimu kutokana na tangazo ulilolisoma.
10. Habari hii inakufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Oanisha maneno ya sehemu A na sehemu B ili kuleta maana.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) hema | (a) tia moyo mtu ili afanye jambo upesi |
| (ii) shituka | (b) kitu kama vile maandishi, mchoro au picha kilichonakiliwa |
| (iii) nakala | (c) tokwa na pumzi kwa nguvu |
| (iv) lowa | (d) kumpa mtu hongera kwa mafanikio aliyoyapata |
| (v) hofu | (e) kuwa na wasiwasi juu ya jambo fulani |
| (vi) pongeza | (f) bila kutarajia |
| (vii) himiza | (g) kusudia kufanya jambo |
| (viii) ghafla | (h) pata maji na kuwa chepechepe |
| | (i) kuwa na woga |

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi nane (8) kwa kutumia muundo ufuatao:**

Alipo__................

**Mfano:** *Alipofika alichukua panga lake na kuelekea darajani.*

*Alipoamka alipiga mswaki na kwenda shuleni.*



Kiswahil STD 5 New.indd 141 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Nahau

**A. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia nahau zilizomo kwenye kisanduku.**

lala fofofo, kata roho,
piga mbio, unga mkono

(i) Watoto walihuzunika kwa sababu mzazi wao ali...................

(ii) Ali............... kuelekea nyumbani ili akamchukue mdogo wake.

(iii) Wali.................. mapendekezo ya wazazi wao kuhusu malezi bora.

(iv) Usiku ule ali.................. kwa kuwa alikuwa amechoka sana.

**B. Tunga sentensi tatu kwa kila nahau.**

(i) tia moyo

(ii) piga mbio

(iii) kata roho

## Zoezi la 5 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Maji yakimwagika, ……………………………………….
2. Penye nia, ……………………………………………….
3. Mchumia juani ……………………………………….
4. Akiba ………………………………………………….
5. Haba na haba ……………………………………….

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

**A. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

(i) panga ______________

(ii) juu ______________

(iii) funga ______________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 142 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) washa ______________

(v) kubwa ______________

(vi) mnene ______________

(vii) sukuma ______________

(viii) tema ______________

(ix) fukia ______________

(x) pakia ______________

**B. Andika umoja na wingi wa maneno yafuatayo:**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (i) | ____________ | matangazo |
| (ii) | ratiba | ______________ |
| (iii) | mti | ______________ |
| (iv) | daraja | ______________ |
| (v) | shughuli | ______________ |
| (vi) | ____________ | vicheko |
| (vii) | chuo | ______________ |
| (viii) | jengo | ______________ |
| (ix) | ufa | ______________ |
| (x) | ____________ | masomo |

## Zoezi la 7 Utungaji

**A. Andika habari fupi yenye maneno kati ya sabini na themanini (70 – 80) kuhusu shughuli unazozifanya nyumbani. Zingatia muda wa kufanya shughuli hizo.**

**B. Andaa tangazo fupi kwa kufuata vipengele vifuatavyo:**

(i) Kichwa cha habari kiwe, "Mitihani ya Darasa la Nne."

(ii) Tarehe ya kuanza na kumalizika kwa mitihani ya Darasa la Nne.

(iii) Mahali itakapofanyika mitihani hiyo.

(iv) Taarifa kwa wanafunzi wa madarasa mengine kutohudhuria shuleni siku za mitihani.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 143 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ufahamu**

***Soma kifungu cha habari, kisha jibu maswali.***

Sheku ni mtoto wa pili katika familia ya Bwana Shenya na Bibi Pachu. Kwa bahati mbaya, wazazi wake wali**aga dunia** akiwa na umri wa mwaka mmoja. Alipoanza masomo yake ya sekondari, mjomba wake aliamua kumueleza jambo alilokuwa nalo kwa kipindi kirefu. Jambo hilo lilihusu kifo cha wazazi wake. Mjomba wake Sheku alimueleza jambo hilo kwa upole sana. Alimwambia, "Sheku mwanangu, wazazi wako walipata ajali ya gari mwaka 1990 na kufariki papo hapo. Nimekulea tangu ukiwa na umri wa mwaka mmoja hadi leo. Nilishindwa kukuambia jambo hili kwa sababu ulikuwa bado mdogo. Hata hivyo, nitaendelea kukulea na kukusomesha mwanangu."

Sheku ali**sikitika** sana baada ya kufahamishwa habari hizo za kuhuzunisha. Alifikiri na kutafakari kuhusu maisha yake bila wazazi. Alikumbuka maneno ya mjomba wake kuwa maji yakimwagika hayazoleki. Alielewa kuwa, hana uwezo wa kuwarejesha wazazi wake duniani. Ali**azimia** moyoni mwake kusoma kwa bidii ili awe na maisha mazuri. Kama **wahenga** wasemavyo kuwa, penye **nia** pana njia, Sheku alisoma kwa bidii na kufaulu masomo katika ngazi zote. Kwa sasa ni daktari. Ana watoto na wanaishi maisha ya furaha. Hakika mchumia juani hulia kivulini.

## Zoezi la 8 Ufahamu

1. Kifungu hiki cha habari kinahusu nini?
2. Kifungu cha habari kinaeleza nani alifariki?
3. Sentensi "Wazazi wake waliaga dunia" ina maana gani?
4. Wazazi wa Sheku waliaga dunia lini?
5. Kwa nini mjomba hakumweleza Sheku kuhusu kifo cha wazazi wake mapema?
6. Kwa nini Sheku aliazimia kusoma kwa bidii?
7. Kwa nini Sheku alifaulu masomo katika ngazi zote?
8. Je, Sheku anafanya kazi gani?
9. Umejifunza nini kuhusu kifungu hiki cha habari?
10. Pendekeza kichwa cha habari uliyoisoma.



Kiswahil STD 5 New.indd 144 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 9 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. azimia
2. wahenga
3. nia
4. sikitika

## Zoezi la 10 Miundo

**Kamilisha miundo ifuatayo:**

1. …………….. akiwa…………………
   **Mfano:** *Mama mkubwa alipata mtoto akiwa na umri mkubwa.*

2. . ……………… kwamba ……………
   **Mfano:** *Baba aliniambia kwamba niwahi kurudi nyumbani.*

3. ……………… kuwa ………………
   **Mfano:** *Rafiki yangu alisema kuwa niende nyumbani kwao wakati wa likizo.*

4. ………………… ili……………………..
   **Mfano:** *Mwalimu alitufundisha vizuri ili tuweze kuelewa somo.*

5. ………………ingawa ………………
   **Mfano:** *Wote tulilala usingizi mnono ingawa vyura walitupigia kelele.*

## Zoezi la 11 Mazoezi ya lugha

**A. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika uyakinishi.**

**Mfano:** Hapendi kucheza mpira wa miguu.
Anapenda kucheza mpira wa miguu.

Mtoto huyu si mtukutu.
Mtoto huyu ni mtukutu.

Sisi hatukula matunda.
Sisi tulikula matunda.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Sheku si mtoto wa pili kuzaliwa.

(ii) Yeye hakusoma kwa bidii.

(iii) Maji yote hayajamwagika.

(iv) Kaka hafundishi chuo kikuu.

(v) Wao hawataishi maisha ya furaha.

(vi) Hamtaanza masomo mwaka kesho.

(vii) Babu hatanisomesha.

(viii) Sikushindwa kukwambia jambo hili.

(ix) Tausi hapendi kusoma vitabu.

(x) Sheku hatakuwa mwanafunzi bora.

**B. Badili vitendo vifuatavyo kuwa majina.**

**Mfano:** pika – *mpishi*

(i) linda ____________

(ii) lima ____________

(iii) fuga ____________

(iv) soma ____________

(v) chora ____________

(vi) jenga ____________

(vii) tamka ____________

(viii) saka ____________

FOR ONLINE USE ONLY

**C. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopita.**

**Mfano:** Dada anafua nguo.

*Dada alifua nguo.*

(i) Babu anavuna mazao shambani.

(ii) Rafiki yangu atanipeleka nyumbani kwao.

(iii) Sheku ameazimia kusoma kwa bidii.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Wazazi wake watamnunulia zawadi.

(v) Shangazi atatutembelea wakati wa likizo.

(vi) Mama yake anasaga karanga.

(vii) Wanafunzi watatunga shairi zuri.

(viii) Wanamichezo wamefanya mazoezi uwanjani.

**D. Andika maneno sahihi kutokana na herufi zilizochanganywa.**

**Mfano:** vuko - *kovu*

takasira - *karatasi*

rafuha - *furaha*

(i) reshehe ____________

(ii) baou ____________

(iii) pimra ____________

(iv) antesa ____________

(v) zezoi ____________

(vi) tiraba ____________

(vii) ngotaza ____________

(viii) yunga ____________

(ix) jomba ____________

(x) opekipe ____________

## Zoezi la 12 Ufupisho

**Fupisha habari ya "Nia na mdogo wake" kwa maneno kati ya thelathini mpaka arobaini (30 – 40).**

## Zoezi la 13 Utungaji

**Andika kifungu cha habari chenye maneno sitini (60) kuhusu somo unalolipenda.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tisa

## Sifa za wanyama

*Katika sura hii, utasoma majigambo yanayohusu wanyama. Pia, utajifunza kuhusu sifa na faida za wanyama wanaokula majani na wanyama wanaokula nyama. Vilevile, utatamba majigambo hayo.*

**Fikiri**

1. Mnyama gani unampenda?
2. Anakula nini?
3. Kwa nini unampenda?

**Ufahamu**

*Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali.*

### Sifa zangu



Mimi ni simba,

Mnyama ninayesifika sana,

Ninapatikana mbugani porini,

Nyama ni chakula changu,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ninayo **ngurumo** ya kutisha,
Nikiwa jike sina manyoya marefu,
Nikiwa dume nina manyoya marefu yenye kuvutia,
Wenyeji na wageni hunifurahia,
Huja kunitazama kwa mshangao,
Mimi ni mfalme wa porini.



Mimi ni mbwa,
Ninasifika sana kwa ukali,
Ninapenda kuishi na binadamu,
Ninakula vyakula vingi,
Lakini nyama kwangu ni muhimu,
Ni  mlinzi na mwindaji **mashuhuri,**
**Machonge** yangu ni silaha hatari,
Niwindapo hukamata na ku**buruza,**
Sauti yangu husikika kote,
Ninamlinda binadamu na mali zake,
Mimi ni mnyama muhimu zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mimi ni kondoo,
Ninasifika kwa upole wangu,
Chakula changu kikuu ni nyasi,
Ninapenda kuishi na binadamu,
Ninampatia **samadi** kwa ajili ya kilimo,
Manyoya yangu yanavutia sana,
Manyoya yangu hutengeneza **sufu,**
Hutengeneza nguo, matandiko na blanketi,
Binadamu hunipenda sana,
Mimi ni mnyama muhimu.



Mimi ni ng'ombe,
Chakula changu ni majani,



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ninapokula hu**cheua,**

Ninaishi na binadamu,

Ninampatia maziwa kwa afya na samadi kwa kilimo,

Mimi ni mnyama muhimu zaidi ya wote.



Mimi ni twiga,

Chakula changu ni majani,

Upole wangu huwavutia  watu wengi,

Ninakula majani mazuri kwa sababu ya urefu wangu,

Mimi ni mrefu kuliko wanyama wote,

Nina miguu  mirefu na shingo ndefu,

Ninatembea kwa **madaha,**

Watalii huvutiwa na uzuri wangu,

Huja nchini kunitazama,

Mimi ni mnyama mzuri sana.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mimi ni tembo,

Ninaishi msituni,

Ninasifika kwa ukubwa kuliko wanyama wote,

Mimi hula majani,

Nina masikio makubwa yanayopepea **mithili** ya **tanga**,

Nina uwezo wa kusikia  kuliko viumbe wengi,

Mimi ni kivutio cha **watalii,**

Wenyeji na wageni huja kuniona,

Kwa uzuri na umaarufu wangu,

Mimi ni mfalme wa **nyikani.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mimi ni paka,

Ni rafiki wa binadamu,

Ninapenda nyama, samaki na maziwa,

Ninakula mijusi na panya,

Nina roho ngumu, kuniua ni vigumu,

Mimi ni mnyama muhimu zaidi.



Mimi ni pundamilia,

Chakula changu ni majani,

Ninasifika kwa usafi na mvuto,

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 153 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Milia** yangu myeusi na myeupe inavutia sana,
Wenyeji na wageni huja kunitazama kwa shauku,
Mimi ni mnyama muhimu sana.



Mimi ni kiboko,
Chakula changu ni majani,
Ninaishi majini na nchi kavu,
Meno yangu ni makubwa sana,
Ngozi yangu haina manyoya,
Miguu yangu ni mifupi lakini mwili wangu ni mkubwa,
Nina nguvu kuliko wanyama wote mtoni na ziwani,
Mimi ni mnyama muhimu sana.



Mimi ni nyoka,
Ninasifika kwa kuwa na sumu kali,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ninaogopwa na binadamu,

Kila mara naonekana mpya,

Kwa kujivua gamba langu,

Sina shida na miguu.

Tumbo langu lanitosha,

Ninaishi mafichoni, shimoni na vichakani,

Chakula changu kitamu ni wadudu na panya,

Mimi ni kivutio cha watalii,

Mimi ni mnyama muhimu sana.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Katika majigambo uliyoyasoma mnyama yupi ni mkubwa kuliko wote?
2. Mnyama yupi ni mrefu kuliko wote?
3. Mnyama gani anaishi majini na nchi kavu?
4. Taja majina ya wanyama wanaokula majani.
5. Taja majina ya wanyama watano wanaokula nyama.
6. Mnyama yupi ana nguvu kuliko wanyama wote wa mtoni na ziwani?
7. Taja majina na faida za wanyama kutokana na majigambo uliyoyasoma.
8. Taja na eleza faida za wanyama watano ambao hawakutajwa kwenye majigambo.
9. Eleza tofauti kati ya simba na kiboko kwa kuzingatia majigambo uliyoyasoma.
10. Kwa kutumia majigambo uliyoyasoma, linganisha sifa za kondoo na ng'ombe.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**A. Oanisha maneno ya sehemu A na sehemu B kwa kuandika jibu sahihi.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) mapato……… | (a) manyoya ya kondoo yanayotumika kutengenezea nguo |
| (ii) thamani……… | (b) kitu au dawa inayodhuru au kuua |
| (iii) mbuga……… | (c) anakula nyama |
| (iv) watalii……… | (d) kinyesi cha wanyama ambacho hutumika kama mbolea |
| (v) samadi……… | (e) matendo na mwendo wa maringo au mbwembwe |
| (vi) madaha…… | (f) mali au fedha inayopatikana baada ya kazi au biashara |
| (vii) sumu……… | (g) mistari myeupe na myeusi iliyoko kwenye ngozi ya pundamilia |
| (viii) sufu……… | (h) eneo la nchi lenye ardhi tambarare, nyasi na misitu myepesi |
| (ix) milia……… | (i) kitambaa kikubwa kinachofungwa kwenye jahazi ili kupunguza nguvu ya upepo |
| (x) mithili......... | (j) gharama au ubora wa kitu |
| (xi) tanga…….. | (k) kama |
| | (l) meno makali yenye ncha |
| | (m) mlio wa mnyama kama simba |
| | (n) watu waendao kwenye nchi ya kigeni au eneo wasilolifahamu kwa mapumziko |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

**Mfano:** *Baba yangu alikuwa kiongozi mashuhuri.*

(i) mashuhuri
(ii) thamani
(iii) cheua
(iv) samadi
(v) madaha
(vi) sufu
(vii) ngurumo
(viii) buruta
(ix) rarua
(x) machonge

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

**1.** …………. lakini…………

**Mfano:** Tembo ni bingwa wa kusikia lakini haoni mbali.

**2.** ………….kuliko…………

**Mfano:** Tembo ni mkubwa kuliko simba.

**3.** ………….kama…………

**Mfano:** Wewe unacheka kama mama yangu.

**4.** ………….zaidi ya……………..

**Mfano:** Twiga ni mnyama mpole zaidi ya wanyama wengine.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Andika KWELI au SI KWELI.**

(i) Kiboko ni mnyama mwenye miguu mifupi. ________

(ii) Kiboko hana manyoya. _________

(iii) Twiga ni mnyama mrefu kama tembo. _________

(iv) Nyoka na paka hawapendi panya. _________

(v) Wanyama wa porini wote hula majani lakini wanyama wafugwao hula nyama. ________

(vi) Tembo hana masikio makubwa. _________

(vii) Kiboko anapenda maji kuliko pundamilia. _______

(viii) Mbuzi, chui na fisi ni wanyama wanaokula nyama. ________

(ix) Simba ni mkali kama twiga. _________

(x) Manyoya ya simba hutengeneza sufu. _________

**B. Andika majina kumi (10) ya wanyama kwa kutumia herufi zilizomo kwenye jedwali. Majina matano (5) yawe ya wanyama wanaokula majani na mengine matano (5) ya wanyama wanaokula nyama.**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | K | F | A | R | U | N | T | F |
| I | I | P | A | K | A | G | E | A |
| M | B | U | Z | I | F | A | M | R |
| B | O | N | N | S | I | M | B | A |
| W | K | D | Y | W | S | I | O | S |
| A | O | A | O | A | I | A | M | I |
| W | B | J | K | L | CH | U | I | I |
| K | E | P | A | N | Y | A | N | I |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wanyama wanaokula majani

(i) ____________________

(ii) ____________________

(iii) ____________________

(iv) ____________________

(v) ____________________

Wanyama wanaokula nyama

(i) ____________________

(ii) ____________________

(iii) ____________________

(iv) ____________________

(v) ____________________

**C. Tunga sentensi kwa kutumia majina ya wanyama yaliyomo kwenye kisanduku.**

1. paka 2. fisi 3. sungura 4. kobe 5. mbuzi,
6. ngedere 7. chui 8. kiboko 9. farasi 10. punda

**Mfano:** *Nyumbani kwetu tunafuga ng'ombe.*

**D. Pigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.**

(i) fisi, mbuzi, kondoo, ng'ombe

(ii) paka, mbwa, nyoka, chui

(iii) tembo, nyati, simba, pundamilia

(iv) kiboko, sungura, mamba, nyangumi

(v) kasa, konokono, kobe, ngamia

**E. Andika vinyume vya maneno yafuatayo:**

(i) zoa ______________

(ii) ficha ______________

(iii) fumba ______________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 159 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) laini ______________

(v) fuma ______________

(vi) kunja ______________

(vii) pinda ______________

(viii) unganisha ______________

## Zoezi la 5 Utungaji

**Tunga habari fupi kuhusu mnyama unayempenda kwa kuzingatia yafuatayo:**

1. Kichwa cha habari
2. Jina la mnyama
3. Sifa za mnyama
4. Chakula anachokula
5. Kwa nini unampenda

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Ishirini

## Miti yetu

*Katika sura hii, utasoma habari kuhusu msitu wa Mzee Sunga na mazimwi. Utajifunza kuhusu aina mbalimbali za miti. Utaweza kueleza faida za miti na kuandika habari fupi kuhusu umuhimu wa miti.*

**Fikiri**

1. Taja majina ya miti unayoifahamu.
2. Miti ina faida gani kwa binadamu?
3. Miti hupatikana wapi?

**Ufahamu**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Msitu wa Mzee Sunga na mazimwi

Palitokea mazimwi matatu; baba, mama na mtoto wao. Yalihangaika sana kutafuta mahali pa kuishi. Hayakufanikiwa kwa sababu, katika nchi ya Azania, misitu mingi ya asili ilikuwa imekatwa na binadamu kwa matumizi mbalimbali. Misitu michache iliyobaki, ililindwa vikali na askari wa maliasili. Mazimwi hayo yalipojaribu kuingia kwenye misitu ya serikali, yalitimuliwa na askari hodari walioilinda.

Yakiwa katika mahangaiko ya kutafuta makazi, ghafla yalijikuta kwenye msitu mzuri na mkubwa sana. Ulikuwa msitu unaopendeza, wenye miti mingi, mirefu na mifupi, ma**pango** makubwa ya kale, vichaka na miti ya matunda ya aina mbalimbali. Pia, kulikuwa na bonde la maji, asali ya asili, na mizinga ya kisasa upande mmoja wa msitu.

Mazimwi yalichekelea sana kuuona msitu huo unaopendeza. Yakashukuru miungu yao kwa bahati hiyo. Yalianza kupanga namna ya kuishi msituni humo. Yakaanzisha makazi kwenye pango moja kubwa msituni humo.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 161 7/23/21 3:15 PM

Hayakujua kuwa mmiliki wa msitu huo alikuwa Mzee Sunga ambaye aliishi kando kidogo ya msitu wake. Siku mbili baadaye, Mzee Sunga alipitapita msituni kukagua miti yake kama ilivyo **ada** yake. Ghafla, alisikia vicheko vya ajabu vikitoka ndani ya pango mojawapo. Alinyata kuelekea pangoni humo ili ajue vicheko hivyo vilitolewa na viumbe gani.

Yakiwa ndani ya pango, mazimwi yakasikia **mchakacho** wa kiumbe kinachoelekea langoni mwa pango. Muda huohuo, yakanusa harufu ya binadamu. Mazimwi yaka**kaa ange.** Yalipomwona mtu akiingia ndani ya pango, yalishituka! Yakatoweka kwa kutumia **hirizi** ya urithi ili binadamu asiyaone.



Baada ya kuingia pangoni, Mzee Sunga hakuona kiumbe yeyote ndani. Hata hivyo, aliona dalili za wazi kwamba kulikuwemo na viumbe muda mfupi uliopita. Ingawa kulikuwa na giza pangoni humo, aliona sehemu kubwa ya sakafu iliyoonesha kuwa kuna viumbe waliolala hapo usiku. Sehemu hiyo ilikuwa imetandikwa nyasi nyingi kutoka upande mmoja wa pango hadi mwingine. Pia, kulikuwa na mabaki ya **kokwa** na asali. Akajua kwamba kuna wavamizi wa ajabu ndani ya msitu wake. Akaanza kuwa na wasiwasi na hofu kubwa. Akatafuta huku na huko ili ajue ni wageni gani waliovamia msitu wake. Hakuona kiumbe yeyote.



FOR ONLINE USE ONLY DO NOT DUPLICATE
Kiswahil STD 5 New.indd 162 7/23/21 3:15 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mazimwi yale yalipotoweka kwa hirizi ya urithi, yalikwenda kujibanza kwenye pango jingine jirani. Yalikuwa yameshituka na kujaa **taharuki.** Yalipofika katika msitu huu, yalidhani yamepata mahali pa amani. Yalidhani ni msitu huru, kumbe huenda sivyo. Yakaanza kujiuliza, “Sasa huyu binadamu anahusianaje na msitu huu? Alionekana mzee, lakini kwa nini alikuja msituni?” Yakataka kujua zaidi. Hata hivyo, yote yakawa yameupenda msitu. Yakaamua kuwa, kwanza, yapeleleze kuhusu nani mmiliki wa msitu huu. Pili, kama si serikali, yam**shawishi** yaununue msitu. Asiposhawishika, yatumie **ulaghai,** mabavu na **miujiza**. Kwa hiyo, yakaandaa mabunda ya fedha. Kisha, yakaamua kujigeuza kuwa binadamu na kwenda kumtafuta yule mzee.

Mazimwi yakamkuta yule mzee ukingoni mwa msitu. Huu ulikuwa upande wa kijiji ambapo wananchi walijenga makazi. Mazimwi yalimsabahi na kujitambulisha kuwa ni watu kutoka kijiji cha mbali kidogo.

“Sisi ni watafiti wa misitu. Tunatafiti utaalamu wa kupanda na kutunza miti. Tuna hamu ya kuwa na msitu mzuri kama huu. Hivi huu ni msitu wa nani?” Zimwi dume liliuliza. “Huu ni msitu wangu,” alijibu Mzee Sunga.

Mazimwi yalishangaa na kufurahi kusikia kuwa msitu huo ni wa binadamu mmoja tu na si wa serikali. Tamaa ikayajaa mioyoni. Yakauliza kwa mshangao, “Kumbe! Hongera! Una bahati na una utajiri mkubwa sana wa **rasilimali**. Uliupataje msitu huu?” “Niliurithi kutoka kwa babu yangu ambaye naye aliurithi kutoka kwa babu yake. Na babu yake huyu aliu**rithi** kutoka kwa babu yake. Kila mrithi amekuwa akipanua eneo la msitu kwa kupanda miti mbalimbali.”

“Ahaa! Tunaona miti ya aina nyingi sana. Mingine hatujawahi kuiona maishani. Waijua yote kwa majina?” Mazimwi yalizidi ku**dadisi**.

Mzee Sunga akajibu, “Naam! Naijua kwa majina kama niijuavyo mistari ya kiganja changu. Humu kuna mninga, mkongo, mvule, mpodo, mpingo, mkunguru, mtiki, na mingine mingi.”

“Natamani kupata msitu kama huu. Miti hii inakufaidisha nini?” Zimwi mtoto aliuliza. Mzee Sunga akajibu, “Miti hii hutoa mbao za kujengea na kutengenezea samani mbalimbali. Mipingo hutumika kutengenezea vinyago, na mitiki hutumika kuundia majahazi na mitumbwi. Mnaona? Humu ndani pia nimening’iniza mizinga na nyuki hutengeneza asali kwa wingi.”

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

“Kuna harufu nzuri humu msituni.” Zimwi la kike lilisema likigeuza pua pembeni kuvuta harufu nzuri ya miti. Mzee Sunga akasema, “Kuna hewa safi na upepo **mwanana** humu kutokana na miti mbalimbali. Licha ya kusaidia kuleta mvua, miti pia huvutia ndege na wadudu wa aina mbalimbali. Wadudu na ndege hawa hupenda kurukaruka kwenye maua ya miti yanayovutia kwa harufu **murua**.”

Baada ya kusikia sifa na manufaa yote hayo, mazimwi yaliwaka tamaa. Yakaanza kumshawishi Mzee Sunga ayauzie msitu huo. Yalitoa mabunda lukuki ya pesa kumshawishi, lakini yeye alikataa akisema, “Siwezi kuuza urithi wangu **adhimu** huu. Ninawashauri mkaanzishe msitu wenu. Baada ya miaka michache mtafaidika. Mimi nimezaliwa na kukuzwa kwa faida za msitu huu. **Katu** siwezi kuuuza.”

Mazimwi yalipoona Mzee Sunga ana **msimamo mkali,** yalianza kumtishia yakisema, “Sikiliza wewe mzee. Sisi tupo watatu, na wewe u peke yako tu. Unawezaje kutukatalia? Hujionei huruma mzee?” Sauti zao zilianza kubadilika. Mzee Sunga alianza kujaa hofu. Akaanza kurudi nyuma huku akitetemeka.

Zimwi dume likasema, “Usiogope mzee. Sisi ni watu wema tu. Tuuzie msitu huu tafadhali.”

Zimwi mtoto lilipogeuka kupenga kamasi pembeni, Mzee Sunga akaona kijimkia kimechomoza kidogo ndani ya kaptula. Akazidi kujaa hofu, huku akiendelea kurudi nyuma bila kujua afanye nini zaidi. Akiwa amekata tamaa, Mzee Sunga akajikwaa na kudondoka chini. Mazimwi yakamsogelea, lakini kabla hayajamfikia, sauti za ngurumo za magari zikasikika kwa nguvu. Askari wa maliasili walikuwa wamekuja msituni hapo kwa ajili ya kusaka mazimwi ambayo yalimuua mzee mmoja ambaye alikataa kuyauzia shamba lake kwenye kijiji cha kumi kutoka hapo.

Yalipowaona askari na silaha zao, mazimwi yaka**taharuki**. Nguvu za kizimwi zikayaingia. Yakaanza kubadilika na kuwa mazimwi yanayotisha. Askari waliposogea zaidi, mazimwi yakatoweka mahali hapo. Yaka**tokomea** msituni na hayakuoneka tena kwenye msitu huo.

Tangu siku hiyo, Mzee Sunga alipatiwa askari wa kuulinda msitu huo, na akaendelea kufaidika na manufaa yaliyotokana na kupanda miti.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Habari uliyoisoma inahusu nchi gani?
2. Viumbe gani waliingia katika msitu wa Mzee Sunga?
3. Kwa nini mazimwi yalikuwa yakihangaika kupata msitu wa kuishi?
4. Taja aina za miti inayopatikana kwenye msitu wa Mzee Sunga.
5. Nani walimuokoa Mzee Sunga mikononi mwa mazimwi?
6. Manufaa gani Mzee Sunga huyapata kutokana na msitu wake?
7. Mbao hutumika kutengenezea vitu gani?
8. Kwa nini Mzee Sunga alikataa kuuza msitu?
9. Mzee Sunga alipata msaada gani kutoka kwa maofisa wa maliasili?
10. Umejifunza nini kutokana na habari hii?

## Zoezi la 2 Msamiati

**A. Tunga sentensi moja kwa kila neno ulilopewa.**

(i) mchakacho
(ii) kokwa
(iii) ada
(iv) tokomea
(v) hirizi
(vi) taharuki
(vii) shawishi
(viii) dadisi
(ix) murua
(x) pango
(xi) rasilimali
(xii) rithi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Oanisha maneno ya sehemu A na maana zake sehemu B.**

| Sehemu A | | Sehemu B | |
|---|---|---|---|
| (i) | adhimu | (a) | danganya |
| (ii) | katu | (b) | jambo lisilo la kawaida |
| (iii) | laghai | (c) | enye ubora wa pekee |
| (iv) | mninga | (d) | hata kidogo, kamwe |
| (v) | muujiza | (e) | mti unaotoa mbao ngumu za kutengenezea samani |

## Zoezi la 3 Nahau

**Tunga sentensi mbili kwa kila nahau.**

1. piga moyo konde
2. kaa ange
3. mkono wa birika
4. angua kilio
5. ona fahari

## Zoezi la 4 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Zimwi likujualo ………………..
2. ………………… hakivunji chawa.
3. Mchumia juani, …………………..
4. ……………………, kiatu chake dawa.
5. Chema chajiuza, ……………………

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yafuatayo:**

(i) stawi ____________________
(ii) idhini ____________________
(iii) penda ____________________
(iv) tembelea ____________________
(v) samani ____________________
(vi) tunza ____________________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) vuta ________________
(viii) kwea ________________
(ix) pasua ________________
(x) toweka ________________

**B. Andika neno moja badala ya kikundi cha maneno.**

(i) mpodo, mpingo, mkunguru, mvule, mninga, mtiki _________
(ii) viti, meza, kabati, dawati, kitanda _________
(iii) nyuki, kipepeo, siafu, panzi, sisimizi, ng'e _________
(iv) tembo, swala, chui, simba, pundamilia, twiga _________
(v) chungwa, chenza, fenesi, papai, parachichi _________
(vi) mahindi, mtama, uwele, ngano _________
(vii) gauni, suruali, shati, sketi, koti, sweta _________
(viii) mkuki, rungu, sime, gobore, bunduki _________

**C. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika KWELI au SI KWELI.**

(i) Misitu ni sehemu ya mazingira. _________
(ii) Vichaka, nyasi, miti mifupi na mirefu ni msitu. _________
(iii) Viumbe wote huishi msituni. _________
(iv) Jangwa ni sehemu iliyojaa maji. _________
(v) Binadamu hutegemea misitu katika maisha yake. _________
(vi) Misitu hutupatia vyakula kama vile matunda. _________
(vii) Misitu huleta mvua ambayo hustawisha mazao. _________
(viii) Kazi ya kutunza na kulinda misitu ni ya serikali peke yake. ___

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Chagua jibu sahihi kujaza nafazi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** Kitabu ______ kimeibwa. (*lake, changu, vyao*)

*Kitabu <u>changu</u> kimeibwa.*

(i) Msitu ______ umestawi. (*wangu, yenu, hao*)

(ii) Alipovuna miti ______ alipasua mbao. (*kile, yake, ule*)

(iii) Shamba ______ la miti lilikuwa kubwa. (*lake, changu, chetu*)

(iv) Kipato ______ kilitokana na kuuza mbao. (*lao, langu, chake*)

(v) Wachongaji huuza vinyago ____kwa bei kubwa. (*chetu, chake, vyao*)

(vi) Askari ______ wa maliasili walilinda misitu. (*wetu, ake, vyake*)

(vii) Mbao ______ ni za mkaratusi. (*yenu, yake, zake*)

(viii) Tuitunze misitu _____ kwa sababu ina faida nyingi. (*yetu, letu, chao*)

**E. Chagua neno kutoka kwenye mabano lenye maana sawa na sentensi uliyopewa.**

(i) Kitu kinachotengenezwa ili kukamata mnyama au ndege. ______ (*jiwe, mtego, kamba*)

(ii) Fundi anayetengeneza vifaa vya mbao. ______ (*fundi cherehani, fundi seremala, dobi*)

(iii) Mtu anayeongoza meli majini. ______ (*nahodha, rubani, dereva*)

(iv) Mtu anayeendesha ndege. ______ (*dereva, nahodha, rubani*)

(v) Mtu anayepanda minazi ili aangue nazi. ______ (*mkwezi, mpandaji, mvunaji*)

(vi) Mtu anayefanya kazi ya kupeleka au kuchukua barua posta au katika ofisi nyingine. ______ (*sekretari, mtumishi, mesenja*)

(vii) Mtu anayetengeneza vitu vya udongo. ______ (*mhunzi, mfinyanzi, fundi udongo*)

(viii) Kifaa kinachotumika kukusanyia nyasi shambani au bustanini. ____ (*rato, reki, kwanja*)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Panga herufi zilizochanganywa ili kupata majina ya miti.**

(i) lumve ________________

(ii) komko ________________

(iii) muyub ________________

(iv) mnpogi ________________

(v) nnamgi ________________

(vi) umkung ________________

(vii) ngelom ________________

(viii) njevim ________________

## Zoezi la 6 Ufupisho

**Andika habari uliyoisoma kwa maneno hamsini (50).**

## Zoezi la 7 Utungaji

**Andika insha fupi kuelezea umuhimu wa miti ukiongozwa na vidokezo vifuatavyo:**

1. Miti hupatikana wapi?
2. Aina za miti unazozifahamu.
3. Faida za kutunza miti.
4. Hasara za uharibifu wa miti.
5. Toa ushauri kuhusu miti.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 5 New.indd 169 7/23/21 3:15 PM

Vitabu kutoka
Taasisi ya Elimu Tanzania

## Darasa la Tano

























ISBN 978-9976-61-816-7

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano